# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII MHE. PROF. DAVID HOMELI MWAKYUSA, MBUNGE, KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA MWAKA 2009/10

## UTANGULIZI

1 ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2008/09 na Malengo ya Wizara katika Bajeti ya mwaka 2009/10. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Mipango ya Maendeleo kwa ajili ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2009/10.

2 ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge; Charles Nyanguru Mwera wa Tarime, Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale wa Mbeya Vijijini, Lolensia Jeremiah Bukwimba wa Busanda na Oscar Mukasa Rwegasira wa Biharamulo Magharibi kwa kuchaguliwa kuwa wabunge wa majimbo yao.

3 ***Mheshimiwa Spika***, ninawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, (Mb.), Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba yake nzuri ya Hali ya Uchumi nchini, Mipango ya Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/10.

Ninampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake inayoonesha jinsi Serikali ya Awamu ya Nne itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2009/10. Ninampongeza Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambaye tunashirikiana kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii kwa wananchi. Napenda pia kuwapongeza Mawaziri wote wa Wizara zilizokwisha wasilisha bajeti zao ambazo kwa namna moja au nyingine zinachangia katika utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba zilizotangulia, michango yao imesaidia sana kuboresha hotuba yangu. Ninawaahidi kwamba Wizara itazingatia ushauri wao katika kutekeleza majukumu na kazi zilizopangwa.

4 ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuungana na Mawaziri wenzangu waliotangulia kusoma hotuba zao kutoa masikitiko na salamu za pole kwa familia, ndugu na jamaa kwa vifo vya Waheshimiwa Wabunge; Chacha Zakayo Wangwe wa Tarime, Richard Nyaulawa wa Mbeya Vijijini, Kabuzi Faustine Rwilomba wa Busanda na Phares Kabuye wa Biharamulo Magharibi. Aidha, ninatoa salamu za pole kwa familia ya Hayati Adam Sapi Mkwawa, aliyekuwa Spika wa Bunge la Tanzania, kwa kifo cha mke wake, mama Aisha Hassan Mkwawa. Vilevile, natoa salamu za pole kwa familia zote zilizopoteza ndugu zao kutokana na ajali mbaya za magari zilizotokea humu nchini, ajali katika mgodi wa dhahabu Geita kwa wachimbaji wadogo saba

na ajali ya kulipuka kwa mabomu katika Kambi ya Jeshi ya Mbagala, Dar es Salaam. Namuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Amina.

5 ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Huduma za Jamii ya Bunge lako Tukufu, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini kwa ushauri iliyoutoa ambao umeboresha matayarisho ya Bajeti ya Wizara ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

6 ***Mheshimiwa Spika***, hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu mawili kama ifuatavyo: Kwanza ni Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 na Majukumu kama yalivyoidhinishwa katika Bajeti ya mwaka 2008/09; na pili ni Mipango, Majukumu na Maombi ya Fedha ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2009/10.

## UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM 2005 NA MAJUKUMU YALIYOIDHINISHWA KATIKA BAJETI YA MWAKA 2008/09

7 ***Mheshimiwa Spika,*** ifuatayo ni taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 na majukumu ya Wizara kama yalivyoainishwa katika Bajeti ya mwaka 2008/09. Utekelezaji huu ulifanyika kwa kutumia fedha zilizotengwa katika Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Mipango ya Maendeleo.

## MATUMIZI YA KAWAIDA

8 ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2008/09, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi **221,196,976,501.00** kwa Wizara kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2009, kiasi cha shilingi **184,897,329,103.07** kilikuwa kimekwishapokelewa na Wizara kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo yanajumuisha Matumizi Mengineyo na Mishahara. Fedha hizi zimetumika kutekeleza kazi zifuatazo:

## UTAWALA NA UTUMISHI

9 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara iliajiri jumla ya watumishi 110 wa kada mbalimbali za afya baada ya kupata kibali cha kuajiri watumishi 234 wa kada za afya. Aidha, Wizara iliajiri watumishi 95 wa kada nyingine zisizo za afya baada ya kupata kibali cha kuajiri watumishi 122 wasio kada za afya. Vilevile, Wizara ilipata kibali cha ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma cha kuwapangia wataalam 5,241 wa kada za afya ili waajiriwe katika Halmashauri, Sekretarieti za Mikoa na Wizara mbalimbali. Hata hivyo, ni wataalam 3,010 waliopangiwa ambao ni sawa na asilimia 57 ya kibali kilichotolewa. Wizara pia iliwapandisha vyeo watumishi 234, wakiwemo Madaktari 125, Tabibu 14, Fundi Sanifu 11, Maafisa Ugavi watatu, Mkutubi mmoja, Makatibu Mahsusi wanne, Wahasibu watano, Maafisa Ustawi wa Jamii 62 na Wasaidizi wa Kumbukumbu tisa. Watumishi wengine wataendelea kupandishwa vyeo kwa utaratibu wa kawaida katika mwaka ujao.

## Kielelezo Na. 1




10 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilikamilisha Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa Kada za Afya ambao ulipitishwa rasmi na Baraza Kuu la Wafanyakazi na utaanza kutumika mwaka 2009/10. Muundo huu umejumuisha kada ambazo awali hazikuwamo katika Muundo huo ambazo ni; Wauguzi wenye Shahada; Maafisa Afya na Wazoeza Viungo ngazi ya Shahada; Matabibu Wasaidizi; Wasaidizi wa Maabara, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Afya Wasaidizi na Wahandisi Vifaa Tiba. Aidha, Muundo huu mpya umetenganisha ngazi za Madaktari wa Kawaida na Madaktari Bingwa ili kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) ambao unalenga kuwa na zahanati katika kila kijiji na vituo vya afya kwa kila kata. Muundo pia, umeongeza kada ya Maafisa Lishe ambayo imeanzishwa ili kukabiliana na tatizo la lishe nchini; tatizo hili linachangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa utapiamlo na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari na magonjwa ya moyo.

11 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliandaa taratibu za uendeshaji wa huduma za afya nchini ili kuboresha utoaji wa huduma hizo. Aidha, Wizara iliunda Baraza la Majadiliano ya pamoja la Sekta ya Afya kwa lengo la kuimarisha ufuatiliaji wa maslahi ya watumishi wa afya nchini. Baraza limewezesha watumishi wa Hospitali Teule na za Hiari wanaolipwa mishahara kutokana na ruzuku, kulipwa mishahara moja kwa moja na Wizara ya Fedha na Uchumi. Vilevile, Wizara ilipokea na kushughulikia malalamiko 189, kati ya hayo 175 yalishughulikiwa na kukamilika, 10 yanaendelea kufanyiwa kazi na manne yalikatiwa rufaa.

12 ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika mwaka 2008/09, Wizara ina changamoto ya upatikanaji wa watumishi wa Sekta ya Afya ili kukidhi mahitaji katika zahanati,vituo vya afya na hospitali za kawaida, za rufaa na hospitali maalum. Aidha, Wizara ina changamoto ya upatikanaji wa kumbukumbuku sahihi za watumishi kwa wakati ili ziweze kutumika katika upandishaji wa vyeo katika muda unaotakiwa na hivyo kuondoa malalamiko ya watumishi. Vilevile, changamoto nyingine ni namna ya kuwahamasisha watumishi wachache waliopo ili waweze kukabili uwingi wa kazi, mabadiliko ya Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) na kufanya kazi katika maeneo yaliyo na mazingira magumu.

13 ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto hizi**,** Serikali inaongeza mishahara kwa wafanyakazi, kutoa motisha, kuwajengea nyumba,

kuharakisha kuwaingiza katika '*payroll*' na kutoa mikopo kwa waajiriwa wapya kabla ya kuanza kupokea mishahara. Hatua hizi zinahamasisha wahitimu katika taaluma za afya na nyinginezo wavutiwe kujiunga na ajira katika Sekta ya Afya. Vilevile utaratibu huu utapunguza idadi ya watumishi wanaokimbia ajira katika Sekta ya Afya. Aidha, utekelezaji wa Muundo wa Maendeleo ya Utumishi Kada za Afya ulioboreshwa na kupitishwa na Baraza Kuu la Wafanyakazi utaongeza motisha kwa wafanyakazi wa Sekta ya Afya. Vilevile, Wizara inaendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kuweza kuwaajiri watumishi na kuwapeleka katika maeneo yenye mazingira magumu. Wizara pia, inawahamasisha waajiri mbalimbali kutenga fedha katika bajeti zao ili kuwalipa watumishi malipo ya muda nje ya masaa ya kazi, inaajiri wataalam wastaafu ambao bado wana nguvu na uwezo wa kufanya kazi na inaboresha uwekaji wa kumbukumbu za watumishi kwa kutumia teknolojia ya kompyuta ambayo imerahisha uwekaji na upatikanaji wa kumbukumbu kwa wakati.

## USIMAMIZI WA FEDHA ZINAZOELEKEZWA KATIKA SEKTA YA AFYA

14 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilifanya maboresho ya usimamizi wa fedha katika Sekta ya Afya. Maboresho hayo yalihusisha mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa Wahasibu 24 ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya ndani kwa Wahasibu 50 yaliyolenga kuwajengea uwezo wa kitaaluma katika usimamizi na udhibiti wa fedha na mali za Serikali. Vilevile, Wizara iliboresha ukusanyaji wa mapato yanayotokana na

Sera ya uchangiaji wa huduma za afya. Kutokana na maboresho hayo makusanyo ya uchangiaji yaliongezeka kutoka shilingi **1,452,315,060.61** mwaka 2007/08 hadi shilingi **1,718,334,085.04** mwaka 2008/09.

15 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilihimiza Taasisi na Miradi yote inayosimamiwa na Wizara kuingia kwenye Mfumo wa malipo kwa njia ya Mtandao "*Intergrated Financial Management System-IFMS*" wenye lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa fedha za umma. Aidha, Wizara iliandaa hesabu zake za mwaka 2007/08 kwa kutumia viwango vya Kimataifa "*International Public Sector Accounting Standards-IPSAS*" ili kurahisisha ulinganishaji wa hesabu zetu na viwango vya Kimataifa.

## UKAGUZI WA NDANI

16 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliendelea kuimarisha mfumo wa udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali, kwa kuandaa mwongozo maalum wa malipo unaozingatia sheria na kanuni mbalimbali za fedha na ununuzi. Ukaguzi wa dawa ulifanyika katika vituo 19 vilivyoko katika mikoa tisa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Mbeya, Ruvuma, Iringa, Morogoro, Dodoma na Singida. Ukaguzi huo ulizingatia utaratibu wa upokeaji, utunzaji na utoaji wa dawa mbalimbali zikiwemo dawa za kupunguza makali ya UKIMWI – "ARV's". Wizara ilitoa maelekezo ya namna ya kuboresha usimamizi wa dawa, vifaa na vifaa tiba. Aidha, Wizara ilifuatilia matumizi ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya kampeni ya upimaji wa

hiari wa virusi vya UKIMWI katika mikoa mitatu ya Mtwara, Ruvuma na Lindi. Vilevile, Wizara ilihakiki taarifa za utekelezaji –"*Performance Audit*" kwa mwaka 2007/08 kwa Idara zilizoko chini ya Wizara ili kupima utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa. Uhakiki huo ulibaini kuwa Idara zilifikia malengo kwa wastani wa asilimia 75.

**UNUNUZI NA UGAVI**

17 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilifanya ununuzi kwa kuzingatia Mpango wa Ununuzi wa mwaka 2008/09. Aidha, Wizara ilikasimu majukumu ya ununuzi kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Taasisi mbalimbali ambazo zipo chini ya Wizara ili wasimamie zabuni za ujenzi kupitia Bodi zao za Zabuni. Mikoa yote ambayo ina Taasisi zilizo chini ya Wizara ikijumuisha vyuo, hospitali za rufaa, makazi ya wazee na mahabusi za watoto inafanya ununuzi kwa niaba ya Wizara. Vilevile, Taasisi zinazojitegemea na Wakala wa Serikali zilizo chini ya Wizara zinafanya ununuzi kwa utaratibu huu. Wizara pia, imeunda Kikosi Kazi cha kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mikataba iliyopitishwa chini ya utaratibu huu.

18 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilitekeleza maelekezo na ushauri wa kitalaam wa ununuzi uliotolewa na wakaguzi kuhusiana na miradi mbalimbali. Aidha, Wizara iliingia mikataba mbalimbali ya ununuzi ikiwemo ya vyandarua, viuatilifu na zabuni ya kufunga Mtandao wa Mawasiliano - "*internet*". Wilaya 37 zimekwisha funga Mtandao wa Mawasiliano na wilaya 62 zinaendelea kufunga Mtandao huo

chini ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria. Ufungaji huu katika Wilaya 62 utakapokamilika mwezi Septemba 2009 utafanya jumla ya wilaya zitakazofaidika na huduma hii kufikia 99. Vilevile, Wizara iliingia mkataba kwa ajili ya kutoa huduma ya matengenezo kinga na matengenezo ya vifaa vya uchunguzi wa magonjwa. Utekelezaji wa mikataba hiyo umewezesha ununuzi na usambazaji wa vyandarua na viuatilifu katika mikoa yote Tanzania Bara, matengenezo kinga na matengenezo ya vifaa vya uchunguzi wa UKIMWI.

19 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliingia mikataba ya huduma mbalimbali za ushauri wa kusambaza vyandarua, viuatilifu, na uhamasishaji wa matumizi yake. Aidha, Wizara imeboresha daftari la kuweka kumbukumbu za vifaa vya kudumu. Daftari hilo limewezesha Wizara kuwa na taarifa muhimu za mali za Wizara.

**MAWASILIANO**

**20** ***Mheshimiwa Spika***, kitengo cha Mawasiliano ni kiungo kati ya Wizara na vyombo vya habari pamoja na wananchi katika kuelezea na kufafanua masuala mbalimbali yanayotekelezwa na Wizara.

21 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilifafanua masuala mbalimbali kwa wananchi kupitia mikutano na vyombo vya habari, kama vile kutoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya vitendanishi vinavyotumika kupima VVU. Aidha, Wizara ilitoa taarifa za magonjwa ya kuambukiza kwa wananchi ambayo yanaweza kuingia nchini kutoka nchi nyingine kama vile mafua makali ya ndege, mafua

ya nguruwe, Marburg na Ebola. Vilevile, Wizara ilianzisha utaratibu wa kuweka taarifa mbalimbali katika tovuti ya Wizara ili wananchi waweze kupata taarifa hizo kwa haraka na ufanisi zaidi.

## SERA NA MIPANGO

### Sheria za Kusimamia Utoaji wa Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii

22 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara iliajiri Mshauri Mwelekezi ambaye kwa kushirikiana na Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa mapendekezo muhimu "*Key features*" ya kuwa na Sheria moja ya kusimamia huduma za afya nchini. Sheria hii pia itasimamia huduma za damu salama. Mapendekezo ya Sheria hii tayari yamewasilishwa Serikalini kupitia Waraka wa Baraza la Mawaziri. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeandaa kanuni za Sheria mbalimbali zilizopitishwa mwaka 2007. Pendekezo la kuanzisha Sheria ya kuunganisha Mabaraza ya taaluma za afya yaliyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii limewasilishwa Tume ya kurekebisha Sheria kwa ajili ya hatua zaidi.

23 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Bunge lako Tukufu lilipitisha Miswada ya Sheria ya Afya ya Akili 2008, Afya ya Jamii 2008 na ya Kudhibiti na Kusimamia Matumizi ya Teknolojia ya DNA ya Binadamu 2009. Aidha, Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu na Azimio la Kuridhia Mkataba wa Nyongeza Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu yalipitishwa. Vilevile, mapendekezo ya

Sheria inayohusu Haki za Watu Wenye Ulemavu yamekamilika na kuwasilishwa Serikalini ili baada ya kuidhinishwa, Muswada husika uweze kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu. Wizara pia, imefanya mapitio ya Sheria mbalimbali za Afya na Ustawi wa Jamii.

24 ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika mwaka 2008/09, Wizara ina changamoto ya upatikanaji wa wataalam wa kutosha wa masuala ya Sheria katika Sekta ya Afya wa kuandaa na kupitia Sheria mbalimbali. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali inaendelea kuajiri wataalam wa masuala ya Sheria katika Sekta ya Afya.

## OFISI YA MGANGA MKUU WA SERIKALI

25 ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali inaratibu na kusimamia huduma za Kinga, Tiba, Mafunzo na Utengamao katika Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii. Aidha, Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali inasimamia maadili kwa kutumia mabaraza ya kitaaluma kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma vilivyo chini ya Sekta ya Afya. Vilevile, Ofisi inasimamia viwango vya ubora wa huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo inayoandaliwa na Wizara pamoja na kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

### Huduma ya Uuguzi na Ukunga

26 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliboresha huduma za Uuguzi na Ukunga kwa

kufanya mapitio ya Mwongozo wa Uuguzi wa kutoa Huduma za Msingi kwa Wagonjwa "*Basic Nursing Procedure Manual*" na Mwongozo wa Viwango vya Ubora wa Huduma za Uuguzi "*Minimum Standards for Nursing Practice in Tanzania*". Miongozo hii itasaidia kuboresha utendaji kazi za kiuguzi na kubaini wauguzi watakaotoa huduma kinyume na miongozo hii ili hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

27 ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina changamoto ya kukabiliana na upungufu wa Wauguzi na Wakunga katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini hasa vilivyo vijijini. Katika kukabiliana na changamoto hii**,** Serikali inaendelea kuajiri Wauguzi na Wakunga, kujenga nyumba za watumishi hasa vijijini katika kila zahanati na vituo vya afya.

**Ukaguzi na Ubora wa Huduma za Afya**

28 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara imewajengea uwezo wataalamu 120 kutoka timu 15 za Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mikoa katika kukinga na kudhibiti maambukizi, utumiaji wa sindano kwa usalama, usimamizi shirikishi, ukaguzi na uboreshaji wa huduma za afya. Timu hizo ni za mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Morogoro, Mtwara, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Singida na Tanga. Pia wakufunzi 38 walipata mafunzo hayo.

29 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara imefanya usimamizi shirikishi na ukaguzi kwa Timu 8 za Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mikoa ya Arusha, Dodoma,

Iringa, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Morogoro na Mwanza. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya kukinga na kudhibiti maambukizi katika utoaji wa huduma za afya na utumiaji wa sindano kwa usalama kwa watumishi 451 kutoka katika hospitali za mikoa za Maweni - Kigoma, Kitete - Tabora, Mara, Mbeya, Sekou-Toure - Mwanza, Shinyanga na hospitali za Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke za mkoa wa Dar es Salaam.

**Huduma za Dharura na Maafa**

30 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilishiriki katika kukabiliana na majanga mbalimbali nchini. Aidha, ushauri na maelekezo ya kitaalamu yalitolewa kwa watumishi 66 katika hospitali za mikoa ya Tanga, Morogoro na Dodoma, juu ya namna ya kuwahudumia majeruhi wengi kwa pamoja na mbinu za kukabiliana na majanga mbalimbali ili kuboresha huduma za afya wakati wa kukabiliana na dharura na maafa pindi yanapotokea. Vilevile, Wizara ilitoa mafunzo ya namna ya kukabiliana na ugonjwa hatari wa homa ya Ebola kwa Timu za Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mikoa na Wilaya katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Kigoma, Kagera na Mwanza. Wizara pia, ilitoa mafunzo kwa Watumishi wa afya hospitalini, mamlaka mbalimbali katika vituo vya mpakani (Afya, Uhamiaji, Polisi, Mamlaka ya Mapato-*TRA*) na baadhi ya watu mashuhuri katika jamii kwenye maeneo ya mikoa inayopakana na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo.

31 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilifuatilia na kufanya tathmini ya madhara yatokanayo na moshi na vumbi la mlipuko wa

volkano uliotokea mwaka 2008 katika mlima wa Oldonyo Lengai ulioko mkoa wa Arusha. Wizara ilitoa ushauri wa namna ya kukabiliana na madhara ya moshi na vumbi hilo, kwa uongozi, watalaam wa mkoa wa Arusha na Idara ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, Wizara ilifuatilia na kuratibu huduma za wagonjwa na wahanga kutokana na mlipuko wa mabomu yaliyotokana na ajali iliyotokea kwenye ghala la silaha, Mbagala jijini Dar es Salaam.

**Mabaraza ya Kitaaluma**

**32** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilikamilisha mfumo wa takwimu za usajili wa madaktari katika Kompyuta – *"Data-Base"* na Mpango Mkakati wa Baraza la Madaktari. Aidha, Wizara ilikamilisha Mwongozo wa kuanzisha vyuo na utoaji mafunzo, usimamizi na ukaguzi wa Vyuo na Taasisi zinazotoa mafunzo ya taaluma ya udaktari. Vilevile, Wizara imesimamia maadili ya madaktari na kutoa onyo dhidi ya malalamiko yanayoelekezwa kwao ya ukiukwaji wa maadili.

**33** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilifanya usimamizi shirikishi kwa Wauguzi Wafawidhi wa hospitali moja ya wilaya kwa kila mkoa na katika hospitali za mikoa yote 21. Aidha, Wizara iliandaa na kusambaza miongozo ya kufundisha somo la maadili kwa Wauguzi hapa nchini. Vilevile, Wizara ilichapisha jumla ya nakala 6,000 za miongozo ya huduma za ukunga na nakala hizo zinaendelea kusambazwa nchi nzima.

**34** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilishughulikia tuhuma mbalimbali za

kimaadili za Wauguzi na adhabu kali zilitolewa dhidi ya watuhumiwa ikiwa ni pamoja na kuwafuta katika daftari la usajili. Aidha, Wizara iliendelea kudhibiti ubora wa taaluma ya uuguzi kwa kutoa leseni rejea 20,500 na leseni mpya 1,500 kwa Wauguzi.

35 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliandaa kanuni za Usajili wa Wafamasia wageni "*Foreign Pharmacists Registration Regulations*", kanuni za namna ya kuendesha mashtaka ya kitaaluma "*Conducting Inquiries Regulations*" na kanuni za ukusanyaji wa maduhuri "*Fee and Charges Rules*". Aidha, Wizara ilikamilisha Mpango Mkakati wa Baraza la Famasi na kufanya ukaguzi na ufuatiliaji kwa wanataaluma katika mikoa ya Dar es Salaam na Mbeya. Vilevile, Wizara ilifanya ukaguzi na ufuatiliaji wa vituo vitano vya kutolea mafunzo ya vitendo kwa Wafamasia katika hospitali za Mount Meru, Bombo, KCMC, Mbeya Rufaa na Bugando. Wizara pia, iliwasajili wafamasia 64 waliomaliza mafunzo na kutoa mafunzo ya maadili na miiko ya taaluma kwa Wafamasia 100 kwa awamu ya kwanza katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma.

36 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara iliunda na kuzindua mabaraza mapya ya wataalamu wa radiolojia na maabara. Aidha, maandalizi ya utengenezaji wa kanuni za usajili, miiko na maadili ya mabaraza ya radiolojia na maabara yalikamilika. Vilevile, Wizara iliandaa mwongozo utakaotumika kutathmini mitaala ya kufundisha wataalamu wa Upeo wa Macho Kuona "*Optometrists*".

37 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilikamilisha kutafsiri katika kiswahili kanuni za Usajili wa Waganga, Wakunga, Wauza dawa na Vituo vya Tiba Asili na Tiba Mbadala, kanuni za usajili wa dawa za asili na kanuni za miiko na maadili. Aidha, Wizara iliandaa kanuni za ukusanyaji wa maduhuri, na kanuni za uendeshaji wa mashtaka. Vilevile, Wizara ilichapisha miongozo ya utoaji huduma katika vituo vya tiba asili na tiba mbadala, ufuatiliaji na usimamizi na kufundishia urasimishaji. Nakala 304 kwa kila mwongozo zilichapishwa. Wizara pia, ilikamilisha uandaaji wa fomu za usajili na kutoa maelekezo kwa kila Mganga Mkuu wa Mkoa na Wilaya kuteua Mratibu wa Tiba Asili ngazi ya Wilaya nchi nzima. Kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji la Tanzania na Radio Uhuru, Wizara ilirusha hewani vipindi 10 vya kuelimisha jamii kuhusu sheria na kanuni za tiba asili na tiba mbadala na imani potofu zinazosababisha vitendo viovu vya ubakaji wa watoto, uchunaji wa ngozi za binadamu na mauaji ya vikongwe na Albino.

38 ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina kabiliwa na changamoto ya kudhibiti ukiukwaji wa maadili miongoni mwa wanataaluma wa Sekta ya Afya na kukabiliana na imani potofu miongoni mwa jamii ambayo imesababisha mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino). Katika kukabiliana nazo Serikali inaendelea kutoa mafunzo ya maadili, mwenendo na utendaji kwa wanataaluma wa Sekta ya Afya na kutoa adhabu kali dhidi ya watuhumiwa ikiwa ni pamoja na kuwafuta katika daftari la usajili na kutoa elimu kwa jamii ili waondokane na imani potofu zinazohusisha mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino).

## HUDUMA ZA KINGA

### Udhibiti wa Magonjwa

39 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Udhibiti wa Magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza. Mafunzo yalitolewa kwa Wataalam wa afya katika ngazi za Mikoa na Wilaya juu ya ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa. Aidha, mikoa na wilaya zote pamoja na hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini vimeendelea kutoa taarifa za wiki za magonjwa ya milipuko na taarifa za mwezi za magonjwa mengine. Magonjwa hayo ya milipuko ni pamoja na Kipindupindu, Surua, Tauni, Homa ya Uti wa Mgongo, Homa ya Manjano, Kichaa cha Mbwa, Homa ya Bonde la Ufa, Mafua Makali ya Ndege, Ebola na Marburg. Vilevile, Wizara ilianzisha vituo vitano maalumu vya ufuatiliaji "*sentinel surveillance sites*" wa Mafua Makali ya Ndege katika hospitali za Mwananyamala, Dodoma, Sekou Toure, Hydom na Kibondo pamoja na maabara maalumu ya kupima ugonjwa huo "*National Influenza Centre*" iliyopo kwenye Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu- Dar es Salaam. Maabara hii maalumu ina uwezo wa kupima magonjwa ya Mafua Makali ya Ndege, Homa ya Bonde la Ufa, Mafua ya Nguruwe, na magonjwa mengine yanayosababishwa na virusi. Wizara pia, kwa kushirikiana na wadau ilianzisha programu mahsusi ya mafunzo ya uzamili katika fani za epidemiolojia na maabara kwa nia ya kuwa na wataalamu mahiri na wenye stadi na uzoefu wa kukabiliana na magonjwa ya milipuko na magonjwa mapya yanayojitokeza na matukio ya hatari yasiyo ya kawaida.

40 **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Idara ya Maafa, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, na Wizara ya Maliasili na Utalii iliendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya magonjwa yanayoathiri binadamu na wanyama. Elimu hiyo ilitolewa kwa njia ya mabango, vipeperushi, radio na Televisheni. Aidha, Mpango Mkakati wa kuzuia ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa uliandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ambapo utekelezaji wake umelenga katika utoaji chanjo kwa wanyama wanaoeneza ugonjwa na elimu kwa wananchi ili kuzuia ugonjwa huo kwa binadamu. Katika kukabiliana na magonjwa ya milipuko nchini, Wizara ilipeleka katika mikoa na wilaya dawa na vifaa na ilifanya uchunguzi wa milipuko.

41 **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2008/09, Wizara ilitoa chanjo za kuzuia ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa, Homa ya Manjano na Homa ya Uti wa Mgongo. Aidha, Wizara ilipeleka wataalamu kusaidiana na wataalamu walioko katika mikoa ya Mara na Kigoma ili kudhibiti milipuko ya Kipindupindu katika mikoa hiyo. Vilevile, Wizara ilipeleka wataalam kusaidiana na wataalamu walioko katika mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa katika kuzuia ugonjwa wa Ebola na Marburg kutoka nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na Uganda.

42 **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2008/09, Wizara ilifuatilia mwenendo wa magonjwa yanayoenezwa na wadudu ya Tauni na Homa ya Malale. Wizara ilidhibiti ugonjwa wa Tauni katika wilaya za

Lushoto, Karatu na Mbulu na hakuna mgonjwa hata mmoja aliyejitokeza. Juhudi za kuwaelimisha wananchi juu ya ugonjwa huu zinaendelea. Aidha, uchunguzi wa ubora wa viuatilifu vinavyoua viroboto wanaoeneza Tauni ulifanyika. Matokeo yameonesha kuwa kiuatilifu aina ya *Carbarly* 5% kinachotumika bado kinafaa katika kuua viroboto. Vilevile, Wizara ilifuatilia Homa ya Malale katika wilaya ya Urambo. Ufuatiliaji huu ulisisitiza utoaji wa takwimu za wagonjwa wa homa hiyo katika ngazi zote. Wizara pia, ilitoa mafunzo ya namna ya kutambua vimelea vya Ugonjwa wa Malale kwa watumishi 12 katika wilaya hiyo.

43 ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina kabiliwa na changamoto ya kudhibiti magonjwa yanayohusisha nchi zaidi ya moja kunakotokana na mwingiliano wa shughuli za kibinadamu kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine na utandawazi; kukabiliana na ongezeko la magonjwa ya kuambukiza yanayoweza kuenea haraka na kudhibiti milipuko ya magonjwa ya kuambukiza kwa wakati ili kupunguza athari zake. Ili kukabiliana na changamoto hizi**,** Serikali inaendelea kufanya ufuatiliaji wa magonjwa yanayohusisha nchi zaidi ya moja ikijumuisha kuwaweka wataalamu na vifaa katika vituo vya mipakani na viwanja vya ndege ili kuwatambua wageni wenye magonjwa wanayoweza kuingia nayo. Aidha Wizara inafanya ufuatiliaji na kutoa elimu kwa jamii juu ya kujikinga na magonjwa ya kuambukiza na kuweka dawa na vifaa vya dharura wakati wote.

**Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria**

44 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilitekeleza mikakati mbalimbali ya kinga

dhidi ya Malaria ikiwa ni pamoja na kuelimisha wananchi juu ya usafi wa mazingira, matumizi ya chandarua chenye viuatilifu, uangamizaji wa vimelea vya mbu kwenye mazalia na unyunyiziaji wa dawa ndani ya nyumba. Matumizi ya vyandarua nchi nzima yamefikia asilimia 30 kwa kutumia mfumo wa Hati Punguzo kwa wanawake wajawazito na watoto kwa utaratibu wa kawaida. Jumla ya vyandarua 945, 892 vimegawiwa kwa mfumo huu kwa nchi nzima. Aidha, katika kuboresha matumizi ya vyandarua, Wizara ilitekeleza Kampeni ya Kitaifa ya kugawa vyandarua vyenye viuatilifu vya muda mrefu ambavyo vinatolewa bila malipo kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano. Ugawaji wa vyandarua 337,200 ulifanyika katika mkoa wa Tanga wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kudhibiti Surua na vyandarua 112,210 katika wilaya ya Mpanda mkoani Rukwa wakati wa kampeni ya kuongeza kasi ya matumizi ya vyandarua. Ugawaji wa vyandarua 435,112 ulifanyika katika mikoa ya Lindi na Mtwara, kati ya hivyo, vyandarua 253, 753 viligawiwa katika mkoa wa Lindi na vyandarua 181, 359 viligawiwa katika mkoa wa Mtwara.

45 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ilipulizia kiuatilifu aina ya ICON katika wilaya zote za mkoa wa Kagera. Aidha, Wizara ilifanya maandalizi ya upuliziaji wa kiuatilifu aina ya "*Dichloro-diphenyltrichloroethane - DDT*" katika wilaya ya Mkuranga ili kupata uzoefu.

46 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara iliandaa mwongozo wa kutumia kipimo

cha haraka cha uchunguzi wa Malaria kinachotoa majibu ndani ya dakika 15 – "*Rapid Diagnostic Test for Malaria* – RDT" na utaanza kutumika nchi nzima. Aidha, kipimo hiki kimeanza kutumika katika mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Iringa na Kagera na kitasambazwa katika mikoa yote nchini. Vilevile, utoaji wa tiba sahihi ya Malaria kwa kutumia dawa Mseto ya "*Artimether Lumefantrine -ALu*" umeendelea katika vituo vya kutolea huduma za tiba vya Serikali, Mashirika ya Dini, Majeshi na vituo binafsi vinavyotoa huduma ya mama na mtoto na tiba ya Kifua Kikuu na UKIMWI.

47 ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango huu, Wizara ina kabiliwa na changamoto ya **k**udhibiti mazalia ya mbu katika maeneo mbalimbali nchini; kufikia muafaka wa mitazamo mbalimbali kuhusu matumizi ya viuatilifu hasa DDT kama suluhisho la kudumu la kupambana na mbu waenezao malaria. Katika kukabiliana na changamoto hizi**,** Serikali inaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu malaria na namna ya utunzaji wa mazingira na kujikinga kwa kutumia vyandarua na kufanya majaribio ya Kisayansi ya kunyunyizia viuatilifu hasa DDT ndani ya nyumba kulingana na mazingira ya nchi yetu yatakayo weza kuthibitisha usalama wa matumizi yake.

**Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma**

48 ***Mheshmiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilipokea msaada wa dawa zenye thamani ya shilingi 2,720,000,000.00 ambazo ziliwanufaisha wagonjwa wa Kifua Kikuu nchini kote. Jumla ya wagonjwa 63,363 waliopimwa waligundulika kuugua Kifua Kikuu na kati yao asilimia 87.4 walipewa matibabu

na kupona kabisa, kiwango ambacho ni zaidi ya kiwango cha kimataifa cha kupona ambacho ni asilimia 85. Aidha, wagojwa 47,843 sawa na asilimia 76 ya wagonjwa wote walipimwa Virusi Vya UKIMWI na kati yao wagonjwa 19,488 sawa na asilimia 41 waligundulika kuambukizwa UKIMWI. Vilevile, Wizara iliendelea kukamilisha maandalizi ya kutoa matibabu ya Kifua Kikuu sugu katika hospitali ya Kibong'oto kwa kupeleka vifaa maalum vya maabara na kutoa mafunzo kwa watumishi 58. Wizara pia, iliandaa mwongozo wa kutoa huduma kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu. Mwongozo huu unalenga kuelimisha wafanyakazi juu ya namna ya kuukabili ugonjwa huu. Wizara iliagiza dawa za Kifua Kikuu sugu zenye thamani ya shilingi 150,960,000.00 kwa wagonjwa 30 wa kwanza.

49 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilipanua huduma shirikishi za Kifua Kikuu na UKIMWI nchi nzima. Aidha, Wizara ilishirikisha vikundi vya wagonjwa wa zamani wa Kifua Kikuu kama vile kikundi cha Mapambano ya UKIMWI na Kifua Kikuu – Temeke - MUKIKUTE kutoka Temeke katika kuongeza uelewa wa dalili za Kifua Kikuu ndani ya jamii. Vilevile, Wizara ilishirikisha vituo vya afya binafsi katika mikoa saba ya Manyara, Shinyanga, Arusha, Iringa, Mwanza, Singida na Dar es Salaam nchini katika kuongeza uelewa wa Kifua Kikuu. Wizara pia, ilifanya maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu duniani ambapo kilele kilikuwa Singida. Maadhimisho haya yalilenga kuelimisha jamii juu ya Kifua Kikuu kupitia vyombo vya habari na vielelezo mbalimbali.

50 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, watumishi wa afya 2,175 walipata mafunzo ya

utoaji wa huduma shirikishi za Kifua Kikuu na UKIMWI, ugonjwa wa Kifua Kikuu sugu, stadi za mawasiliano na uratibu wa takwimu za Kifua Kikuu na Ukoma kwa mfumo wa kompyuta. Watumishi hawa walitoka katika mikoa ya Mara , Kigoma, Kagera, Rukwa, Dar es Salaam, Manyara, Dodoma, Lindi, Mtwara, Iringa, Ruvuma, Tanga, Singida, Morogoro, Tabora na Shinyanga. Aidha, Wizara iliendelea kutoa dawa za mseto za Kifua Kikuu bila malipo na hakuna upungufu uliojitokeza.

51 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilikamilisha kampeni maalum ya kupambana na Ukoma katika Halmashauri za Wilaya za Kigoma na Geita na Manispaa ya Temeke. Jumla ya wagonjwa wapya 246 wakiwemo watoto 139 waligundulika na kuanzishiwa matibabu. Aidha, Wizara iliadhimisha siku ya Ukoma Duniani katika wilaya ya Nkasi, mkoani Rukwa kwa mafanikio na wagonjwa wapya 26 wakiwemo watoto wa shule 18 waligundulika kuwa na Ukoma na kuanzishiwa matibabu. Vilevile, Wizara ilitengeneza viatu jozi 7,200 na kuchongesha viatu maalum jozi 13 pamoja na miguu bandia 37 kwa watu waliopata ulemavu kutokana na athari za Ukoma. Wizara pia, ilisaidia kuunda vikundi maalum saba vya watu walioathirika na Ukoma katika mikoa ya Tabora, Singida na Morogoro ili kutunza afya zao wenyewe. Sambamba na hayo, Wizara ilisaidia kufanyika kikao cha Baraza Kuu la Chama cha Watu wenye Ukoma Tanzania ambapo mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar iliwakilishwa.

52 ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango huu, Wizara ina kabiliana na changamoto ya

kudhibiti maambukizo mapya ya Kifua Kikuu na Kifua Kikuu Sugu; kukabiliana na unyanyapaa miongoni mwa jamii kwa wagonjwa wa Ukoma na kuondoa hofu miongoni mwa jamii kuhusu kupima ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa woga wa kuhusishwa na ugonjwa wa UKIMWI. Wizara inakabiliana na changamoto hizi kwa kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu Kifua Kikuu na Kifua Kikuu Sugu; kutambua mapema watu wenye Kifua Kikuu na Kifua Kikuu Sugu na kutoa rufaa; kuhamasisha jamii kujitokeza kupima Kifua Kikuu kwa hiari pale wanapoona dalili na kutoa elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa wa Ukoma

**Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI**

***53*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilielimisha wananchi juu ya mbinu mbalimbali za kinga na dalili na hatari za ugonjwa wa UKIMWI kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, huduma za ushauri nasaha na upimaji wa hiari zilipanuliwa na kusambazwa nchi nzima mpaka katika ngazi ya jamii. Wizara iliimarisha huduma za dawa za kupunguza makali ya UKIMWI na kuzifikisha mpaka ngazi za vituo vya afya na pia iliimarisha huduma za uchunguzi na tiba ya magonjwa nyemelezi katika vituo vyote vya tiba nchini.

***54*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa hiari kutoka vituo 1,035 vilivyokuwepo mwaka 2007 hadi 1,757 mwezi Juni 2009, lengo ni kufikia vituo 2000. Kuanzia Januari 2008 hadi Juni 2009 watu wapato 656,858 walipata ushauri nasaha na

kupewa majibu. Kati ya hao watu 78,645 walikutwa na maambukizi ya VVU. Maambukizi ya virusi vya UKIMWI yalishuka kutoka asilimia saba kwa mujibu wa – "*Tanzania HIV Indicator Survey-2003-2004*" hadi kufika asilimia 5.6 "*Tanzania HIV/Malaria Indicator Survey-2007-2008*" na asilimia 4.8 kwa takwimu za upimaji wa hiari kufuatia kampeni ya taifa ya kupima UKIMWI kwa hiari 2007/2008.

**55** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto katika kliniki za afya ya uzazi na mtoto kutoka 1,374 mwaka 2007, hadi kufikia 3,029 mwaka 2008. Aidha, idadi ya akina mama waliopata huduma iliongezeka kutoka 713,506 Desemba, mwaka 2007 na kufikia 958,103 Desemba, mwaka 2008.

**56** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliongeza idadi ya wanaopata dawa za UKIMWI kutoka 145,000 mwezi Aprili 2008 hadi 242,290 mwezi Juni 2009 sawa na asilimia 80.7 ya lengo la wagonjwa 300,000.

**Kielelezo Na. 2: Ongezeko la Huduma za UKIMWI zinazotolewa**

| Aina ya Huduma | 2007 | 2008/09 | Ongezeko |
|---|---|---|---|
| Idadi ya vituo vinavyopima Virusi vya UKIMWI kwa hiari | 1035 | 1,757 | 722 |
| Idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda mtoto | 1374 | 3029 | 1,655 |
| Idadi ya akina mama waliopata huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda mtoto | 713,506 | 958,103 | 244,597 |
| Idadi ya wagonjwa wanaopata dawa za kutibu UKIMWI | 23,951 | 242,290 | 219,339 |
| Idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya kuzuia maambukizo ya UKIMWI kwa mama mjamzito kwenda kwa mtoto | 544 | 2,474 | 1,930 |

**Kielelezo Na. 3: Idadi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa ngazi ya huduma hadi kufikia Desemba 2008**




57 ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango huu, Wizara ina changamoto ya kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyopo ya kupungua kwa maambukizi ya UKIMWI katika sehemu mbalimbali ya nchi yanakuwa endelevu. Aidha, inakabiliana na unyanyapaa miongoni mwa jamii kwa wagonjwa wa UKIMWI. Vilevile, inakabiliana na jinsi ya kuondoa hofu miongoni mwa jamii kuhusu kupima Virusi Vya UKIMWI na pia kuwafikia wananchi wengi katika kutoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Wizara inakabiliana na changamoto hizi kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI, kuhamasisha jamii kujitokeza kupima Virusi Vya UKIMWI kwa

hiari, kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kuongeza vituo vinavyotoa tiba na matunzo kwa watu wenye ugonjwa wa UKIMWI na kuongeza bajeti ya huduma za UKIMWI

**Mpango wa Taifa wa Huduma za Macho na Udhibiti wa Ugonjwa wa Usubi**

58 ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango unatoa ushauri kuhusu huduma za macho, kupanga Sera za uagizaji wa dawa na matumizi ya vifaa vya macho ikiwemo miwani na vilevile kuangalia ubora wa tiba zitolewazo katika Hospitali na vituo vya huduma za afya hapa nchini. Mpango huu unafanya ufuatiliaji utoaji wa huduma za macho katika mikoa na wilaya na kuangalia kama zinaoana na viwango vinavyokubalika.

59 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilifuatilia utekelezaji wa Mipango ya Dira 2020 ya kutokomeza upofu unaozuilika katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma. Aidha, Wizara kwa kupitia Bohari ya Dawa ilisambaza dawa ya Zithromax kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa wa vikope katika wilaya 32 ambapo jumla ya wananchi 9,755,000 walipata dawa hiyo. Vilevile, dawa ya Mectizan kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa wa Usubi ilisambazwa katika wilaya 17 zilizoathirika na ugonjwa huo; wilaya hizo ni Lushoto, Korogwe, Muheza, Mkinga, Morogoro, Mvomero, Kilombero, Ulanga, Kilosa, Songea, Mbinga, Namtumbo, Tunduru, Rungwe, Kyela, Ileje na Ludewa.

**Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto**

60 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilitekeleza mpango maalum wa kuboresha

huduma na kuongeza kasi ya kupunguza vifo vya wanawake wajawazito, watoto wachanga na watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 112 kwa watoto hai 1,000 mwaka 2004-05 hadi 91 kwa watoto hai 1,000 mwaka 2007-08. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ilinunua magari 14 ya kubeba wagonjwa, gari moja kwa kila wilaya za Kibaha, Mafia, Ruangwa, Rungwe, Nkasi, Mpanda, Kondoa, Mpwapwa, Bahi, Chamwino, Kongwa, Manispaa ya Dodoma, Hospitali ya Mkoa wa Dodoma na Hospitali ya Mvumi. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Mfuko wa Pamoja ilinunua vifaa mbalimbali vitakavyosambazwa katika hospitali 86 na vituo vya afya 50 hapa nchini. Wizara pia, ilinunua na kusambaza dawa za uzazi wa mpango nchi nzima.

61 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilitoa mafunzo kwa Wahudumu wa Afya katika maeneo mbalimbali yanayolenga kuwaongezea ujuzi watumishi wanaotoa huduma za mama na mtoto. Watumishi 327 kutoka katika vituo vya afya na zahanati za mikoa ya Kigoma, Dodoma, Mtwara, Iringa, Singida, Tabora, Kilimanjaro, Ruvuma, Arusha na Pwani walipatiwa mafunzo ya stadi za kuokoa maisha na utoaji wa huduma ya dharura kwa matatizo yatokanayo na uzazi. Aidha, Wahudumu 125 kutoka katika vituo vya afya na zahanati za mikoa ya Dodoma, Mtwara, Iringa, Tabora, Arusha na Pwani walipatiwa mafunzo kuhusu Malaria na Kaswende katika utoaji wa huduma kwa mama wakati wa ujauzito. Waratibu 21 ngazi ya mkoa wa huduma za afya ya

uzazi na mtoto walipatiwa mafunzo ya usimamizi na ufuatiliaji wa huduma kwa masuala yahusuyo afya ya uzazi hasa kwa mama wajawazito.

62 ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kazi zilizopangwa, Wizara ina changamoto ya upatikanaji wa vituo vya huduma za afya, wataalam na vifaa vya kutosha, kudhibiti ukiukwaji wa maadili miongoni mwa wauguzi na wakunga na kupanua huduma za dharura za uzazi ili kuwafikia wanawake wajawazito wengi. Ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali inaendelea kuongeza vituo vya kutolea huduma za uzazi, vifaa na wataalam, kuendelea kutoa elimu ya maadili, mwenendo na utendaji kwa wauguzi na wakunga, kuimarisha vituo vya afya ili viweze kutoa huduma za upasuaji wa kutoa mtoto, kutekeleza Mpango Mkakati wa Kuongeza Kasi ya Kupunguza Vifo vya Wanawake Wajawazito na Watoto Wachanga na kuongeza bajeti ya huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto

**Udhibiti wa Magonjwa ya Watoto kwa Uwiano**

63 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilitekeleza mkakati wa udhibiti wa magonjwa ya watoto kwa uwiano na mikakati ya kupunguza vifo vya watoto wachanga. Aidha, kuna mwelekeo mzuri wa kupungua kwa vifo vya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja kutoka vifo 68 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2004-05 hadi vifo 58 mwaka 2007-08. Mwongozo wa matibabu ya magonjwa ya kuharisha kwa watoto uliboreshwa na uzinduzi wake kufanyika rasmi Aprili mwaka 2009 na kusambazwa nchini. Matibabu mapya ya kutumia ORS yaliboreshwa kwa kuongeza vidonge vya zinki na yameanza kutumika nchini kote. Dawa hizi zimesambazwa katika vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya. Ili kuboresha huduma

zinazotolewa kwa watoto ngazi ya hospitali, mafunzo yalitolewa kwa watoa huduma 208 kutoka hospitali za mikoa na wilaya katika mikoa kumi ya Mwanza, Kagera, Mtwara, Lindi, Pwani, Tabora, Mbeya, Dodoma, Kigoma na Morogoro. Pia mafunzo ya huduma za dharura yalitolewa kwa watoa huduma 180 kutoka Wilaya 44 za Mikoa iliyotajwa.

**Kielelezo Na. 4: Mwelekeo wa Vifo vya Watoto wachanga, watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja na watoto wenye umri chini ya miaka mitano**




Chanzo: **(DHS 1992, 1999, 1996, 1999, 2004 & Tanzania HIV and Malaria Indicator Survey 2007/08)**

64 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilizindua kitabu kinachoonesha hali ya

watoto wachanga nchini na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ili kupunguza vifo vya watoto hao. Aidha, miongozo ya kutoa huduma muhimu kwa watoto wachanga "*Essential Newborn Care*" iliandaliwa kwa lengo la kupunguza vifo vya watoto hao. Pia miongozo ya mafunzo ya huduma kwa watoto wenye uzito pungufu "Kangaroo Mother Care" iliandaliwa. Huduma ya watoto wenye uzito pungufu ilianzishwa katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro na Kituo cha Afya Mlandizi. Vilevile, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa huduma zinazotolewa kwa watoto ngazi ya vituo vya afya katika wilaya sita za mkoa wa Dodoma na ufuatiliaji ngazi ya jamii ulifanyika katika Wilaya za Biharamulo, Korogwe na Sengerema.

65 ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mkakati huu, Wizara ina changamoto ya upatikanaji wa vituo vya huduma za afya, wataalam na vifaa vya kutosha, kudhibiti ukiukwaji wa maadili miongoni mwa wauguzi na wakunga na kupanua huduma za dharura na rufaa kwa watoto. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu utambuzi wa watoto wanaohitaji huduma za dharura ndani ya saa 24, kuongeza vituo vya kutolea huduma za watoto, vifaa na wataalam, kuendelea kutoa elimu ya maadili, mwenendo na utendaji kwa wataalam wa afya, kuendelea kutoa mafunzo kwa wataalam wa afya kuhusu kukabiliana na magonjwa ya watoto kwa uwiano. Hatua nyingine zinazochukuliwa na Wizara ni pamoja na kutekeleza Mpango Mkakati wa Kuongeza Kasi ya Kupunguza Vifo vya Wanawake Wajawazito na Watoto Wachanga na kuongeza bajeti ya huduma za Afya ya Mtoto

**Mpango wa Chanjo wa Taifa**

66 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilitoa huduma za chanjo nchini ili kuwakinga watoto wote wenye umri chini ya mwaka mmoja, dhidi ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo. Kampeni ya Kitaifa ya chanjo ya surua ilitekelezwa nchini kote kuanzia Agosti 30 hadi Septemba 01, 2008. Kampeni hii ilijumuisha utoaji wa matone ya Vitamini A, dawa ya minyoo, matone ya chanjo ya polio na ugawaji wa vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu. Jumla ya watoto 12,300,340 wenye umri wa miezi 6 hadi miaka 10 walilengwa kupata chanjo ya surua, watoto 1,768,885 wa umri 0 hadi miaka 5 katika wilaya 18, walilengwa kupatiwa matone ya chanjo ya polio, watoto 6,492,618 wa umri wa miezi 6 hadi miaka 5 walilengwa kupata Vitamini A; watoto 5,708,402 walilengwa kupata dawa ya minyoo na watoto 350,000 walilengwa kupatiwa vyandarua katika uzinduzi uliofanyika mkoani Tanga. Matokeo ya kampeni hiyo yalionesha viwango vilivyofikiwa ni Chanjo ya surua asilimia 86; matone ya chanjo ya polio asilimia 82; matone ya vitamini A asilimia 97; dawa ya minyoo asilimia 96 na vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu asilimia 95. Aidha, chanjo mpya ya '*Haemophilus Influenza type B*' (HIB) kwa ajili ya kuzuia Homa ya Uti wa Mgongo na Kichomi iliziduliwa rasmi tarehe 30 Machi 2009 na kuanza kutolewa tangu tarehe 1 Aprili 2009 kwa watoto wote wenye umri chini ya mwaka mmoja kwenye vituo vyote vya huduma za afya ya Uzazi na Mtoto. Chanjo hii imeingizwa kwenye utaratibu wa kawaida kupitia Mpango wa Taifa wa Chanjo.

67 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, katika juhudi za kutokomeza ugonjwa wa

Pepopunda kwa watoto wachanga, Wizara ilitekeleza awamu ya kwanza na ya pili ya utoaji chanjo ya Pepopunda kwa wanawake wenye umri wa kuzaa katika Halmashauri 14, ambazo zina kiwango cha chanjo chini ya asilimia 80. Halmashauri hizo ni Bukombe, Kahama, Kibondo, Mpanda, Hanang, Kiteto, Bariadi, Meatu, Tarime, Simanjiro, Ngara, Mpanda Mjini, Rorya na Bunda.

68 ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango huu, Wizara ina changamoto ya kuinua kiwango cha chanjo nchini kufika zaidi ya asilimia 80, kuinua mwamko wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuwapeleka watoto kupata na kukamilisha chanjo kwa watoto na kudhibiti milipuko ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo hasa sehemu za mipakani kutokana na mwingiliano wa shughuli za binadamu. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inaendelea kuimarisha huduma za chanjo kwa kuhakikisha kuwa mnyororo baridi unafanya kazi na dawa za chanjo, vitamini A na dawa za kutibu minyoo zinapatikana wakati wote, kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuchanja watoto na kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa yanayozuilika kwa chanjo na kuendesha kampeni katika Wilaya za mipakani.

**Huduma za Afya Shuleni**

69 ***Mheshimiwa spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilifanya kampeni ya kuwapatia watoto wa shule za msingi dawa za Minyoo na Kichocho katika mikoa sita ya awamu ya mwisho. Mikoa hiyo ni Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, na Rukwa. Jumla ya wanafunzi 1,490,787 walipata dawa ya Mebendazole kwa ajili ya Minyoo na wanafunzi 1,412,871 walipata dawa za Kichocho.

**Huduma za Afya ya Msingi katika Jamii**

70 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliratibu Huduma za Afya ya Msingi katika jamii ambapo usimamizi wa utekelezaji ulifanyika katika mikoa ya Ruvuma, Rukwa na Mbeya kwenye wilaya tano, zahanati 60, vituo vya afya 30 na Kamati za Afya ya Msingi za vijiji 90.

**Huduma za Afya ya Mazingira**

71 ***Mheshimiwa Spika,*** **a**fya na usafi wa mazingira nchini, afya ya wafanyakazi, usalama wa chakula, kudhibiti milipuko ya magonjwa na kuimarisha afya sehemu za bandari, viwanja vya ndege na maeneo ya mipakani ni miongoni mwa majukumu muhimu ambayo Wizara inayatekeleza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

72 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliitisha mkutano wa wataalam wote wa afya ya mazingira nchini ambao ulifanyika mjini Moshi, kwa kusudi la kujadili kwa kina masuala yahusuyo afya na usafi wa mazingira nchini. Aidha, Wizara iliwajengea uwezo wataalamu wa afya ya mazingira kutoka katika mikoa mitano ya Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Pwani na Dodoma ili kuimarisha shughuli za usimamizi na ufuatiliaji wa masuala yanayohusu afya ya mazingira nchini.

73 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara iliandaa rasimu ya Sera ya Usafi wa Mazingira nchini kwa kushirikiana na wataalam kutoka maeneo mbalimbali. Rasimu hii imeanza kusambazwa kwa wadau ili kupata maoni yao. Aidha, Wizara ilichapisha Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Afya ya Mazingira ya 2007 na kuandaa

Kanuni za utekelezaji wa Sheria hiyo. Vilevile, Wizara iliendelea kuratibu Mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira nchini kwa lengo la kuinua kiwango cha usafi na kupambana na magonjwa yatokanayo na hali duni ya usafi wa mazingira. Mashindano haya yalishirikisha Halmashauri zote nchini. Matokeo ya mashindano hayo yaligawanywa katika makundi makuu manne (4). Kundi la kwanza ni la Halmashauri za Majiji ambapo Jiji la Mwanza liliibuka mshindi, kundi la pili ni la Halmashauri za Manispaa ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Moshi iliibuka mshindi wa kwanza ikifuatiwa na Manispaa ya Iringa na mshindi wa tatu ilikuwa Halmashauri ya Manispaa ya Arusha. Katika kundi la tatu ambalo lilihusisha Halmashauri za Miji, Halmashauri ya Mji wa Njombe iliibuka mshindi wa kwanza ikifuatiwa na Halmashauri ya Mji wa Mpanda na kundi la nne lilikuwa ni Halmashauri za Wilaya ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilikuwa ya kwanza ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meru na Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ikishika nafasi ya tatu. Washindi wote walipewa zawadi kwenye kilele cha sherehe za mazingira zilizofanyika tarehe 5 Juni 2009 mkoani Tabora.

74 ***Mheshimiwa Spika***, hali ya usafi katika shule zetu bado ni duni kwani ni asilimia 38.9 tu ya shule zina vyoo na kutunza usafi. Ili kuinua kiwango cha usafi wa mazingira shuleni, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na wadau wengine, iliandaa Mkakati wa Usafi wa Mazingira Shuleni. Miongoni mwa shughuli zilizopo katika Mkakati huo ni kushindanisha shule katika masuala ya afya na usafi wa mazingira ili kuinua kiwango cha usafi shuleni.

75 ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kazi hizi, Wizara ina changamoto ya kuhamasisha wananchi kuzingatia hali ya usafi na usafi wa mazingira na kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika kutoa huduma za usafi wa mazingira mijini. Katika kukabiliana na changamoto hii**,** Wizara inaendelea kuimarisha elimu kwa jamii kuhusu usafi wa mtu mwenyewe na usafi wa mazingira na kuhamasisha Sekta Binafsi kuingia mkataba na Halmashauri katika kutoa huduma za usafi wa mazingira mijini.

**Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira.**

76 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilisambaza miongozo na viwango vya udhibiti taka za huduma za afya katika Halmashauri na mikoa yote nchini, na kutoa mafunzo kwa waratibu 32 wa udhibiti wa taka zitokanazo na huduma za afya katika ngazi ya mkoa na taifa. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira, Mwongozo wa Udhibiti Taka ulipitiwa na kuboreshwa. Pia wataalam 10 kutoka mikoa ya Dodoma, Singida, Morogoro, Dar es Salaam, Tabora, Tanga na Mtwara walipata mafunzo ili kuwajengea uwezo katika nyanja za tathmini na maandalizi ya mipango ya kudhibiti madhara ya afya yatokanayo na uchafuzi wa mazingira. Aidha, Wizara ilifanya tathmini ya athari za afya zitokanazo na uchafuzi wa mazingira katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza ambapo sampuli za chakula, udongo na maji safi na maji taka zilichukuliwa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchunguzi wa maabara ili kubaini kiwango cha uchafuzi katika maeneo hayo.

**Huduma ya Afya Kazini**

77 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya afya na usalama kazini ilifanya ufuatiliaji na usimamizi wa masuala yahusuyo afya za wafanyakazi katika maeneo ya kazi. Wachimbaji madini wadogo wadogo wapatao 500 waliopo katika machimbo ya Mererani mkoani Manyara walitembelewa na kupatiwa ushauri wa kitaalamu wa namna ya kujikinga na athari zitokanazo na matumizi ya kemikali katika uchimbaji madini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitoa mafunzo kwa wakufunzi 70 yahusuyo kuzuia maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI kwa wafanyakazi katika sekta ya afya kutoka Mikoa ya Tabora, Singida, Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

**Huduma ya Afya Kwenye Vituo vya Kuingia nchini.**

78 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, kwa kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa mipakani, vituo viwili vya Uwanja wa ndege wa Kilimanjaro na Mwanza vilipatiwa gari moja kwa kila kituo na wataalam wanne walipelekwa masomoni.

**Usalama wa Vyakula**

79 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara katika kutekeleza Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003 imeendelea kukasimisha majukumu ya usalama wa chakula kwa wataalam wa afya na usafi wa mazingira waliopo katika ngazi ya Halmashauri.

80 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliboresha hali ya usalama wa chakula

nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na sekta na wadau mbalimbali wa maendeleo, iliandaa rasimu ya Sera ya Chakula Salama. Vilevile, ili kupambana na magonjwa ya kuhara kama vile Kipindupindu, Homa ya Matumbo na Kuhara Damu, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na wadau wengine iliandaa rasimu ya Mpango wa Maji Salama Ngazi ya Kaya. Mpango huu unashirikisha na kuhamasisha jamii na watafiti ili kubuni njia mbalimbali za kuwezesha upatikanaji wa maji salama ngazi ya Kaya/Mtumiaji. Mpango huu utachangia Mpango Mkubwa wa Upatikanaji wa Huduma za Maji Safi na Salama nchini.

**Elimu ya Afya kwa Umma**

81 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliboresha uratibu, uwezeshaji, ufuatiliaji na usimamizi wa utoaji elimu ya afya katika jamii. Wadau wa elimu ya afya, hususan vyombo vya habarí na mashirika yasiyo ya kiserikali, walishirikishwa kikamilifu katika kuelimisha wananchi masuala mbalimbali yanayohusu namna ya kujikinga na magonjwa na kutumia huduma za afya zinazotolewa katika zahanati, vituo vya afya na Hospitali. Wizara ilisisitiza wananchi kwenda na kutumia huduma za afya mapema, mara wanapobaini dalili za ugonjwa au suala jingine la kiafya.

82 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilidurusu na kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili rasimu ya Mwongozo wa Elimu ya Afya kwa Umma. Rasimu hiyo itakamilika katika mwaka wa fedha 2009/10 na kutumika katika utoaji wa huduma za elimu ya afya kwa jamii. Aidha, Wanahabari 24 kutoka mikoa ya Kilimanjaro, Morogoro, Mwanza

na Tanga walipata mafunzo ya kujengewa uwezo katika kuandaa habari zinazohusu afua za afya zenye mafanikio na zinazolenga kufikiwa kwa Malengo ya Milenia, “Malengo namba 4, 5 na 6” katika jamii. Vilevile, Wanahabari wengine 20 walipata mafunzo ya kujengewa uwezo wa kuandaa habari zinazohusu afya nyakati za majanga na matukio ya dharura.

83 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilielimisha jamii kuhusu njia mbalimbali za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza kupitia vipindi 52 vya Siri ya Afya Bora vilivyorushwa na Shirika la Utangazaji Tanzania. Aidha, jamii ilielimishwa na kuaswa ichukue tahadhari kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa Homa ya Nguruwe katika nchi mbalimbali duniani. Vipeperushi 20,000 kuhusu ugonjwa huo vilichapishwa na kusambazwa katika Halmashauri zote nchini. Katika kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa elimu ya afya, mikoa 13 na Halmashauri 69 ziliteua waratibu wa huduma hizo.

84 ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza kazi hizi, Wizara ina changamoto ya kuhakikisha kuwa elimu ya afya inawafikia wananchi wengi. Aidha,katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara inaendelea kuongeza utoaji wa elimu kupitia vyombo mbalimbali vya habari vikijumuisha Radio, Televisheni, Magazeti na Machapisho mbalimbali ya namna ya kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama Mafua Makali ya Ndege, Mafua ya Nguruwe, Homa ya Bonde la Ufa, Kifua Kikuu, Kisukari na Shinikizo la Damu linaloua watu wengi.

## HUDUMA ZA TIBA

### Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

85 ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za tiba zinajumuisha mfumo mzima wa uchunguzi, utoaji matibabu na rufaa kuanzia ngazi ya kaya, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya hadi hospitali za rufaa za mikoa na hospitali maalum "*super speciality*" katika sekta za umma na binafsi. Katika ngazi ya Kaya, huduma zinatolewa na Serikali na Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kwa Mfumo wa Mkoba "*outreach/home based care*". Huduma za Afya ya Msingi zinatolewa na zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya. Huduma za rufaa zinatolewa na hospitali za mikoa.

86 ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inajenga na kupanua Hospitali za Mikoa kwa kuongeza vifaa na wataalam ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake ya rufaa katika mikoa. Hospitali zinazojengwa mpya ni pamoja na za Mikoa ya Pwani na Manyara. Hospitali za Mikoa ya Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga zinapanuliwa ambapo majengo na maabara mpya zinajengwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

87 ***Mheshimiwa Spika,*** Huduma za ubingwa maalum zinatolewa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Taasisi ya Mirembe na Isanga na Hospitali ya Kibong'oto. Hospitali nyingine za ubingwa maalum ngazi ya kanda ni pamoja na Hospitali ya Rufaa Mbeya, Bugando Medical Centre

na Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC). Aidha, Serikali inajenga Hospitali za Kanda ya Kusini, Mtwara na Kanda ya Kati, Dodoma. Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kati, Dodoma unatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Huduma za ubingwa maalum zitapunguza rufaa ya matibabu ya wagonjwa nje ya nchi. Maeneo maalum yanayotiliwa mkazo ni upasuaji wa moyo, usafishaji figo, upasuaji wa ubongo, mgongo na viungo, tiba ya saratani na wagonjwa wa akili.

88 ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika mwaka 2008/09, Wizara ina changamoto za ongezeko la mahitaji ya huduma bora na zinazopatikana karibu zaidi na wananchi, ongezeko la wagonjwa wanaohitaji huduma za ubingwa maalum na upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa III na MMAM. Katika kukabiliana na changamoto hizo**,** Wizara inaendelea kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya kukarabati, kupanua na kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za rufaa za mikoa na hospitali za rufaa maalum. Aidha, Wizara inaendelea kukabiliana na changamoto hizi kwa kuongeza bajeti kwa ajili ya kupanua na kuimarisha hospitali za rufaa na zenye utaalamu wa ubingwa maalum, kujenga kituo cha upasuaji wa moyo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambacho pia kitatumika kutoa mafunzo ya utaalam wa upasuaji wa moyo. Vilevile, Serikali ya India kwa kushirikiana na Wizara inatoa madaktari wa ubingwa maalum wa kuja kutoa huduma za upasuaji wa moyo na kutoa mafunzo

kwa wataalam wetu. Wizara pia, inahamasisha wadau mbalimbali kuchangia bajeti ya Sekta ya Afya ili kukidhi mahitaji yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa III na MMAM na kuhamasisha wananchi kuchangia nguvu kazi katika ujenzi wa zahanati na vituo vya afya katika maeneo yao ikiwa ni mojawapo ya utekelezaji wa MMAM.

**Huduma za Afya ya Kinywa**

89 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilifunga mitambo ya kutoa huduma za tiba ya meno katika Halmashauri za Rufiji, Kondoa, Manyoni, Misungwi, Geita, Ukerewe, Kwimba, Sengerema, hospitali ya Mkoa Mwanza, hospitali ya Tumbi, Kilwa, Ilala, Kilindi, Handeni na Mufindi. Aidha, mitambo 38 ya tiba ya meno ilipelekwa na kufungwa katika Vituo vya kutolea huduma za afya 38 katika mikoa 18 nchini.

**Hospitali za Rufaa na Hospitali Maalumu**

**Hospitali Maalumu "*Super speciality hospitals*"**

**Hospitali ya Taifa Muhimbili**

90 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Hospitali ilitoa huduma kwa wagonjwa 227,634 kati ya hao 78,351 walilazwa. Aidha, mashine nane za kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo zilinunuliwa. Mtaalam aliyemaliza mafunzo maalum ya mfumo wa figo ameanza kazi. Mchakato wa kupata mashine ya kusafisha maji yanayotumika katika mashine za kusafisha damu ili huduma ianze unaendelea. Ufungaji wa

mashine kwenye majengo yaliyokamilika kufanyiwa ukarabati umefikia asilimia 50, ufungaji wa vifaa zaidi unaendelea. Vilevile, wataalamu bingwa sita wamepelekwa kuchukua mafunzo ya uzamivu. Uboreshaji wa idara ya majeruhi na magonjwa ya dharura umekamilika kwa asilimia 70. Hospitali pia, ilianzisha huduma za upasuaji mkubwa wa moyo tangu mwezi Mei, 2008. Hadi kufikia mwezi Juni tarehe 30, 2009 wagonjwa 105 walikuwa wamefanyiwa upasuaji huo.

**Hospitali ya Bugando**

91 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 589,086, na kati ya hao wagonjwa 58,903 walilazwa. Aidha, Hospitali ilihudumia wagonjwa 8,416 walioathirika kwa VVU, kati ya hao, wagonjwa 3,891 walikuwa wanapewa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI. Bugando ni hospitali ya kwanza kutoa huduma ya vipimo maalum kwa watoto wenye umri chini ya miezi 18 wenye virusi vya UKIMWI na mpaka sasa imesajili watoto 712 walioathirika kwa VVU na watoto 349 walianzishiwa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI. Vilevile, hospitali ilianzisha Idara ya Magonjwa ya Saratani na kuanza kutoa matibabu ya dawa kwa wagonjwa wa Saratani za Matiti na Shingo ya Kizazi. Hospitali pia, ilipata mashine ya kupima Saratani ya Matiti. Ukarabati wa jiko na sehemu ya kufulia nguo za wagonjwa umefikia asilimia 50. Hospitali ilikamilisha maandalizi ya kuanza kutoa huduma za upasuaji mkubwa wa moyo. Maandalizi hayo ni pamoja na wataalam, vifaa na vifaa tiba na sehemu ya kutolea huduma hiyo.

**Hospitali ya KCMC**

92 **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008/09, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa wa nje 118,238. Kati ya hao, wagonjwa 11,533 walihudumiwa baada ya kupata rufaa toka hospitali za ngazi za chini, wagonjwa 11,230 walitibiwa bila kuwa na rufaa. Wagonjwa waliolazwa ni 22,099. Aidha, Hospitali imekamilisha jengo la huduma za upasuaji rekebishi kwa asilimia 55. Maandalizi ya ujenzi wa jengo la huduma za kurekebisha viungo vya wagonjwa umekamilika, mkandarasi amekwisha anza kazi.

**Hospitali ya Rufaa Mbeya**

*93* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Hospitali iliendelea kutekeleza majukumu ya kutoa huduma za tiba kwa ngazi ya rufaa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kwa kipindi hicho hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 211,663 na kati ya hao wagonjwa 29,219 walilazwa. Aidha, Hospitali iliendelea na utafiti wa chanjo ya UKIMWI awamu ya pili kwa lengo la kujua kama chanjo hiyo ni salama kwa mtumiaji na kama inatoa kinga. Matokeo yalionesha kuwa chanjo hiyo ni salama na inaongeza kinga.

*94* ***Mheshimiwa Spika,*** utafiti wa ugonjwa wa Kifua Kikuu uliolenga kutumia mkojo ili kupima uambukizo, ulionesha kuwa njia hiyo siyo mahsusi kwa vimelea vya Kifua Kikuu tu, bali na vimelea vya aina nyingine hata vile ambavyo havileti ugonjwa. Kwa sasa utafiti unaendelea ili kupata matibabu ya Kifua Kikuu kwa muda mfupi zaidi. Utafiti huo unafanyika kwa kutumia dawa ya *REMox.*

**Taasisi ya Mifupa Muhimbili**

95 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 15,994. Kati ya wagonjwa hao 3,958 walilazwa. Aidha, Taasisi ilifanya matengenezo kinga ya vifaa vya upasuaji, vyumba vya upasuaji na vyumba vya wagonjwa mahututi kwa asilimia 60 na ukarabati wa majengo umeanza. Vilevile, Taasisi ilitoa mafunzo ya namna ya kuhudumia majeruhi kwa wafanyakazi wa Hospitali za mikoa ya Morogoro, Iringa, Mara na Kagera na hospitali ya wilaya ya Mkuranga.

96 ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ilifanya upasuaji kwa wagonjwa 2,614. Kati ya wagonjwa hao waliohitaji viungo bandia vya nyonga ni 52 na goti 14. Aidha, wagonjwa 81 walifanyiwa upasuaji wa Saratani ya Kichwa/Ubongo, 13 upasuaji wa Uti wa Mgongo na hivyo kuchangia katika kupunguza idadi ya wagonjwa wanaolazimika kupelekwa nje ya nchi kwa matibabu hayo na kuokoa shilingi 1,600,000,000.00. Taasisi iliweza kukusanya shilingi 1,100,000,000.00 kutokana na wagonjwa wanaolipia huduma na hivyo kuongeza vyanzo mbadala vya fedha ya matumizi kwa Taasisi.

**Taasisi ya Saratani Ocean Road**

97 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 12,641. Kati ya wagonjwa hao, wapya ni 3,408 na wagonjwa wa marudio ni 9,233. Idadi hii imekuwa ikiongezeka ikiashiria ufahamu wa wananchi na pia ukuaji wa tatizo la Saratani. Wagonjwa waliolazwa walikuwa 2,751. Aidha, Taasisi ilitoa jumla ya matibabu 29,222 ya mionzi kwa kutumia mashine tatu za mionzi.

**98** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, jumla ya wanawake 12,400 walifanyiwa uchunguzi wa Saratani ya Shingo ya Kizazi. Wanawake 992 kati ya hao ambao ni sawa na asilimia 8, walikutwa na dalili za awali za Saratani ya Shingo ya Kizazi na walitibiwa na kupona. Hii inamaanisha kwamba kama huduma hii isingetolewa, wanawake hawa baada ya miaka mitatu mpaka mitano wangepatwa na Saratani kamili yaani "*invasive cancer*". Huduma hii imetolewa katika mikoa ya Dodoma, Pwani, Manyara, Iringa, Mtwara, Lindi na Dar es Salaam. Halmashauri za Wilaya ambazo zilinufaika na huduma hii ni Bahi, Chamwino, Kongwa, Kondoa, Mpwapwa, Babati, Simanjiro, Kiteto, Mbulu, Hanang, Iringa, Kilolo, Mufindi, Makete, Ludewa, Tandahimba, Mtwara, Newala, Masasi, Njombe, Bagamoyo na Kisarawe. Manispaa zilizonufaika na huduma hii ni pamoja na Lindi, Kinondoni, Temeke, Mtwara, Iringa na Dodoma. Katika uchunguzi huo, wataalam wa afya 143 kutoka katika mikoa hiyo 7 walipatiwa mafunzo ya uchunguzi wa dalili za awali za Saratani ya Shingo ya Kizazi ambapo viongozi wa afya 125 walipatiwa ufahamu kuhusu Saratani ya Shingo ya Kizazi na jinsi ya kuingiza programu ya kinga ya Saratani katika mpango wa afya wa Halmashauri. Aidha, Taasisi ilishirikiana na Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania "*MEWATA*" kutoa huduma katika Manispaa ya Dodoma, Halmashauri za Kondoa na Kongwa na Mkoa wa Manyara. Vilevile, Taasisi kwa kushirikiana na *International Union Against Cancer "UICC"* pamoja na *International Agency on Research for Cancer "IARC",* ilitoa mafunzo ya tiba ya Saratani ya Shingo ya Kizazi kwa njia ya upasuaji mdogo "*LEEP*" kwa wataalamu wa afya 21; kati ya hao, 10 walitoka

Tanzania na 11 walitoka nje ya nchi. Taasisi pia, ilitoa mafunzo ya tiba shufaa kwa wataalamu wa afya 25 kutoka hospitali zote za rufaa nchini na jumla ya wagonjwa 820 walifaidika na huduma hii.

***99*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilitoa dawa za Saratani "*chemotherapy*" kwa watoto wagonjwa wa Saratani 346. Asilimia 78 ya watoto hawa walikuwa wanaugua Saratani ya "*Burkitts lymphoma*". Aidha, Taasisi ilishirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje katika kuimarisha huduma za Saratani nchini, hasa katika kutengeneza Mkakati wa Kitaifa wa kupambana na Saratani.

***100*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilikarabati jengo kwa ajili ya huduma za *Telemedicine* na pia iliandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya litakalokuwa na nafasi kubwa ya wodi, vyumba vya madaktari, vyumba vya matibabu na vyumba vya upasuaji ili kwenda sambamba na kuongezeka kwa wagonjwa wa Saratani.

**Hospitali ya Mirembe na Taasisi ya Isanga.**

**Hospitali ya Mirembe**

***101*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Hospitali ilitoa huduma za uchunguzi na tiba kwa wagonjwa wa akili waliopata rufaa kutoka kote nchini na kuhudumia wagonjwa wenye magonjwa ya kawaida. Ilitoa elimu ya afya ya akili kwa jamii, shuleni, vyuoni na kwenye taasisi mbalimbali kuhusu afya ya akili. Ilitoa mafunzo ya afya ya

akili kwa wanafunzi wa Chuo cha Uuguzi Mirembe na wanafunzi wa vyuo vingine vya afya wanapofika kwenye mafunzo kwa vitendo na kufanya tafiti kuhusu magonjwa mbalimbali na mahusiano yake na magonjwa ya akili. Aidha, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa wa akili 24,591; na wagonjwa wa kawaida 16,745. Wagonjwa wa akili waliolazwa walikuwa 1,957, na wagonjwa wa kawaida 739. Vilevile, Hospitali ilitoa mafunzo ya athari ya dawa za kulevya katika shule za Sekondari nane za mjini Dodoma za Hijra, Dodoma, Central, Bihawana, Nkuhungu, Mazengo, City, na Kikuyu na vipindi vitatu vilitolewa katika televisheni. Taasisi pia, ilitoa mafunzo kwa Matabibu 32 kutoka vituo mbalimbali vya huduma za afya ili kuweza kuwatambua waathirika mapema na kuwapa huduma, ikiwa ni pamoja na rufaa.

**Taasisi ya Isanga**

***102 Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilichunguza, kutibu na kutoa huduma za utengamao kwa wagonjwa wa akili wahalifu. Aidha, ilichunguza watuhumiwa wa makosa ya jinai wanaoshukiwa kuwa walitenda makosa hayo wakiwa wagonjwa wa akili. Vilevile, ilishauri Mahakama kuhusu hali ya afya ya akili ya watuhumiwa wakati walipotenda makosa. Taasisi pia, ilitoa ushauri kwa Magereza na jamii kuhusu namna nzuri na salama ya kuwahudumia wagonjwa wa akili.

***103 Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilihudumia wagonjwa 150. Wagonjwa walioruhusiwa kurudi nyumbani baada ya kuonekana wamepata nafuu ni 90.

**Hospitali ya Kibong'oto**

104 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, hospitali ilitoa huduma za uchunguzi na matibabu kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu waliopata rufaa kutoka mikoa yote nchini na nchi jirani. Hospitali ilihudumia wagonjwa wa Kifua Kikuu 1,843, kati ya hao wagonjwa wa nje ni 883 na waliolazwa ni 960. Wagonjwa wapya waliogundulika kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu walikuwa 480. Aidha, hospitali ilihudumia wagonjwa wa kawaida 8,293, kati ya hao wagonjwa wa nje ni 7,909 na waliolazwa ni 384. Vilevile, wagonjwa 1,694 wanaoishi na VVU waliandikishwa, kati ya hao wagonjwa 963 walianzishiwa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI.

105 ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na huduma zitolewazo na hospitali hizi kwa ujumla wake, kuna changamoto za kuhakikisha upatikanaji wa madaktari bingwa maalum, ongezeko la wagonjwa wanaohitaji huduma za ubingwa maalum, kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya huduma za ubingwa maalum na kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali maalum za rufaa.

106 ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto hizo**,** Wizara inaendelea kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya mafunzo ya ubingwa maalum na ununuzi wa vifaa vya ubingwa maalum kama vile MRI. Aidha, Wizara inahakikisha kuwa kunakuwepo na ushirikiano wa karibu na vyuo vikuu vya fani za tiba vya ndani na nje ya nchi ili kuongeza utaalam wa ubingwa, vifaa na teknolojia mpya na kutoa huduma za mtandao (Telemedicine)

ambao unawawezesha wagonjwa kupata huduma za ubingwa kwa urahisi kwa kuwatumia madaktari bingwa walio mbali na kituo cha huduma. Vilevile, Wizara inatenga fedha katika bajeti kwa ajili ya kukarabati, kupanua na kujenga hospitali za rufaa za mikoa na hospitali za rufaa maalum na kupanua na kuimarisha huduma za mkoba na kiliniki tembezi zinazotolewa na madaktari bingwa maalum.

**Uchunguzi wa Magonjwa**

***107 Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliimarisha karakana za ufundi wa vifaa tiba vya kanda katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, hospitali za rufaa za Bugando, KCMC, Mbeya, na hospitali ya Mkoa ya Mtwara. Aidha, Wizara ilianzisha karakana ya kanda ya magharibi katika hospitali ya mkoa wa Tabora. Vilevile, Wizara ilishirikiana na wadau wengine katika mafunzo ya nadharia na vitendo ili kuimarisha huduma za karakana za mikoa ya Kagera, Tanga, Mtwara na Mbeya sambamba na karakana nyingine za kanda.

***108 Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliimarisha huduma za maabara na radiolojia kwa lengo la kukidhi viwango vinavyokubalika. Wizara kwa kushirikiana na wadau ilijenga maabara za hospitali ya mkoa wa Kagera na hospitali ya Amana katika manispaa ya Ilala. Aidha, Wizara ilikarabati maabara za hospitali ya mkoa wa Dodoma na hospitali ya Bombo katika mkoa wa Tanga ili zifikie ngazi ya rufaa na kutumika katika kufanya tafiti. Vilevile, Wizara ilianza ujenzi wa maabara mpya katika hospitali za mikoa ya Morogoro na

Singida, Manispaa ya Temeke na Tumbi mkoa wa Pwani.

109 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara imeziwezesha maabara za Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, hospitali za rufaa Mbeya, Bugando na KCMC kuingia kwenye mchakato wa kurasimishwa ili zitambuliwe kwa ubora wa viwango vya kimataifa. Mchakato huu unaendelea vizuri na matarajio yetu ni kuwa, kufikia mwishoni mwa mwaka ujao, baadhi ya maabara zitakuwa zimekidhi viwango vya kimataifa na kupata Ithibati ya kimataifa.

110 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na wadau imejenga Maabara ya kisasa ya Afya za Jamii katika eneo la Ocean Road. Maabara hiyo ina majukumu ya kuhakiki ubora wa huduma za maabara nyingine nchini, kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa maabara, kufanya vipimo vya kuhakiki ili kudhibiti ubora wa vipimo vya magonjwa mbalimbali ikiwemo milipuko kama vile Homa ya Bonde la Ufa na Mafua ya Nguruwe.

111 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na Wahisani ilifanya matengenezo kinga na matengenezo ya kawaida ya mashine za X-ray, Ultra Sound, Mashine za Chumba cha Upasuaji na jenereta za umeme za hospitali za Wilaya. Aidha, Wizara imeboresha huduma za radiologia kwa kununua mashine nne kubwa za Ultrasound za rangi kwa hospitali za Rufaa za Muhimbili, Bugando, KCMC, na Mbeya. Vilevile, Hospitali ya Taifa Muhimbili ilipewa Mashine mpya ya “CT Scanner 6 Slice” na Mashine ya kisasa ya “*Magnetic Nucleic Resonance and Imaging – MRI*”.

**112** ***Mheshimiwa Spika***, changamoto zilizopo ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa wataalam wa matengenezo kinga na matengenezo ya mara kwa mara ya vifaa na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kutolea huduma za uchunguzi na tiba. Katika kukabiliana na changamoto hizi**,** Wizara inaendelea kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya kununua vifaa na kwa ajili ya mafunzo ya wataalam wa matengenezo ya vifaa vya kutolea huduma za uchunguzi na tiba na imeweka mfumo wa matengenezo kinga na matengenezo ya mara kwa mara ya vifaa vya uchunguzi na tiba

**Mpango wa Damu Salama**

**113** ***Mheshimiwa Spika,*** niliahidi kujenga kituo cha Damu Salama Kanda ya Kati (Dodoma), kwa msaada wa Serikali ya Norway. Napenda kutoa taarifa kuwa Serikali ya Norway imekwisha toa fedha kwa awamu ya kwanza. Michoro imekamilika na hivi sasa tuko kwenye hatua ya kutangaza zabuni, ili apatikane mkandarasi.

**Huduma za Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**

**114** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilitumia shilingi 76,680,930,000 kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Dawa hizi zilisambazwa katika zahanati 3,754, vituo vya afya 397, Hospitali za Wilaya na Teule 134, Mikoa 20, Manispaa 3, Rufaa za Mikoa 4, Hospitali ya Taifa 1, Hospitali za Rufaa Maalum 4, Jeshi la Wananchi 2 na Polisi 1. Kati ya fedha hizo, Serikali ilitoa shilingi 31,430,460,000, Mfuko wa Pamoja wa Wadau wa Maendeleo "*Basket Fund*"

shilingi 22,000,000,000 na "*Global Fund*" shilingi 23,250,470,000 ni kwa ajili ya ununuzi wa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARV).

**Kielelezo Na. 5: Mwelekeo wa Bajeti ya Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**




**115** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilitoa mafunzo ya uagizaji na utunzaji wa kumbukumbu za dawa na vifaa tiba kupitia mfumo wa "*Integrated Logistics System – ILS*" kwa watumishi 499 kutoka katika zahanati, vituo vya afya, na hospitali za Serikali na za mashirika ya dini na yasiyokuwa ya Kiserikali katika Mikoa ya Singida, Tabora, Kigoma, Mwanza na Kagera pamoja na Halmashauri za Kilosa na Kiteto. Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Shinyanga na Mtwara iliendelea kutumia mfumo wa "*Indent System*".

**116** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika zahanati na vituo vya afya, Wizara ilisambaza mahitaji ya vituo hivyo kwa mfumo wa makasha uliozingatia

mahitaji "*ILS push*" kwa kipindi cha miezi mitatu kati ya mwezi Machi na Juni 2009. Hatua hiyo ilichukuliwa ili kuviwezesha vituo hivyo kuwasilisha maombi ya mahitaji yake halisi Bohari ya Dawa kwa mfumo wa ILS.

***117 Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina changamoto za kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba vya kutosha na kwa wakati na kuhakikisha kuwa dawa zinazopatikana zinawafikia wananchi na zinatumika inavyotakiwa. Aidha, Wizara inakabiliana na changamoto hizi kwa kuendelea kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba vya kutosha, kujenga mfumo wa uagizaji na usambazaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma kulingana na mahitaji na kuimarisha Bohari ya Dawa ili iendelee kutoa huduma zilizo bora za uagizaji, uhifadhi na usambazaji wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba.

**Magonjwa yasiyo ya kuambukiza, Afya ya Akili, na Dawa za Kulevya**

***118 Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliandaa na kusambaza Mpango Mkakati wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo ni Kisukari, Saratani, magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu, athari za ajali, Magonjwa ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu na Magonjwa sugu ya kifua. Aidha, Wizara imeimarisha sehemu inayoshughulikia magonjwa yasiyo ya kuambukiza, Afya ya Akili na Dawa za Kulevya kwa kuongeza idadi ya wataalam, na vitendea kazi. Vilevile, Wizara ilianzisha kamati za ushauri za kufuatilia uimarishaji wa huduma za magonjwa yasiyoambukiza katika Hospitali ya Taifa Muhimbili,

hospitali za rufaa za Mbeya, KCMC na Bugando na hospitali maalum ya Mirembe.

**Huduma za Hospitali za Mashirika ya Kujitolea, Makampuni na Watu Binafsi**

119 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi na Mashirika ya Kujitolea katika utoaji wa huduma za afya kwa kuingia makubaliano na Halmashauri zao, ili zitumike kama Hospitali Teule. Hospitali hizo ni Seliani - Arusha, Turiani - Mvomero, St. Joseph - Moshi, Dareda - Babati na Nyangao - Lindi. Hii inafikisha hospitali 26 ambazo zinatumika kama hospitali teule za Halmashauri.

120 ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina changamoto za kuwabakiza wataalam walio katika hospitali za Mashirika ya Kujitolea wasihamie katika huduma za umma na kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kuzimudu gharama za huduma za afya zitolewazo na watoa huduma wa Sekta Binafsi. Katika kukabiliana na changamoto hizi, Wizara inaendelea kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa afya walioshikizwa na Serikali katika vituo vya Mashirika ya Kujitolea. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeandaa mkataba wa huduma ambao utaziwezesha Halmashauri na hospitali za Mashirika ya Kujitolea kuingia katika makubaliano ya kutoa huduma za afya kwa niaba ya Halmashauri na inaendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kupunguza gharama ya huduma wanazozitoa kwa vile Serikali inagharamia huduma ambazo Serikali inazihudumia ili kukinga magonjwa yanayoweza kuambukizwa.

**Huduma ya Matibabu Nje ya Nchi**

121 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, idadi ya wagonjwa waliopendekezwa (*referred*) kutibiwa nje ya nchi ni zaidi ya 2,000, uwezo wa Wizara ni kuwadhamini wagonjwa 400. Wizara ilipeleka wagonjwa 321 kutibiwa nje ya nchi ambayo ni asilimia 80 ya lengo. Hata hivyo, juhudi za Serikali za kutumia Taasisi zake kuhudumia wagonjwa wake ni kama ifuatavyo: Taasisi ya Mifupa Muhimbili iliwezeshwa kupata wataalamu na vifaa maalum na hivyo kuwezesha wagonjwa 52 kufanyiwa upasuaji wa kuwekewa viungo vya bandia vya nyonga, wagonjwa 14 kuwekewa viungo vya bandia vya goti, wagonjwa 81 wa Saratani ya Ubongo na wagonjwa 13 walioumia Uti wa Mgongo kupatiwa huduma ya upasuaji na kuimarisha Uti wa Mgongo. Hospitali ya Taifa Muhimbili iliwezeshwa kupata wataalam na vifaa maalum vya uchunguzi na upasuaji wa Moyo na tiba ya Figo. Mpaka sasa hospitali ilifanikiwa kufanya upasuaji mkubwa wa Moyo kwa wagonjwa 105. Aidha, Wizara iliingia makubaliano na hospitali tano za India ambazo zitatumia wataalam wake kuja hapa nchini kuwajengea uwezo wataalam wetu kutoa huduma za upasuaji kwa wagonjwa wenye matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa ya Moyo, Figo, Ubongo na Uti wa Mgongo na kuwekewa viungo bandia. Hospitali nne kati ya hizo ni za Apollo na moja ni ya Taasisi ya Madras Medical Mission. Pia, wataalam wetu watapata fursa ya kwenda India kupata mafunzo zaidi na kushiriki katika upasuaji wa wagonjwa wetu wakiwa India.

122 ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina changamoto ya ongezeko la wagonjwa wanaohitaji huduma za

ubingwa maalum nje ya nchi. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali inaendelea kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, kuimarisha hospitali za rufaa, wilaya na mikoa kwa kuzipa uwezo wa kutoa huduma bora za utambuzi na kutibu, kuwa na wataalam waliobobea na hivyo kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi kwa matibabu.

## MAFUNZO NA MAENDELEO YA WATUMISHI WA SEKTA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

***123*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara iliendesha mafunzo katika vyuo vyake 74 na iliratibu mafunzo katika vyuo 42 vya afya vya Binafsi na Mashirika ya Dini. Wanafunzi 2,311 walidahiliwa katika vyuo vya Uuguzi na wanafunzi 1,520 walidahiliwa katika vyuo vya Sayansi Shiriki na hivyo, kuvuka lengo la kudahili wanafunzi 1,827 katika vyuo vya Uuguzi na 1,273 katika vyuo vya Sayansi Shiriki katika kipindi cha mwaka mmoja. Aidha, mitaala minane inaendelea kupitiwa katika utaratibu wa kuimarisha ubora wa mafunzo vyuoni. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Mashirika ya Dini, inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya afya nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza ruzuku kutoka shilingi 30,000.00 hadi 40,000.00 kwa mwanafunzi mmoja, kuhamasisha mashirika hayo kufungua vyuo kama Murugwanza – Ngara na Lugala - Ulanga ambao wako katika kuanzisha shule za uuguzi na kupewa walimu kwa njia ya kuazimwa (*Secondment*). Mafunzo kwa kada 10 za uuguzi na 12 za sayansi shiriki yamefanyika. Kada hizo ni

Wauguzi Walimu, Wauguzi Wakunga, Wauguzi Afya ya Jamii, Wauguzi Afya ya Akili, Wauguzi Upasuaji, Wauguzi Macho, Wauguzi Watoto, Wauguzi daraja A, Wauguzi daraja B na Wauguzi ngazi ya shahada. Pia, kada 12 za sayansi shiriki ambazo Wizara ilitoa mafunzo ni Madaktari Wasaidizi, Matabibu, Matabibu Wasaidizi, Mafundi Sanifu Maabara, Mafundi Sanifu Maabara Wasaidizi, Tabibu Meno, Mafundi Sanifu Maabara (Meno), Maafisa Afya, Tabibu Msaidizi Meno, Macho na Viungo.

***124*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilitoa mafunzo katika ngazi ya uzamili kwa wataalam 494, kati ya hao 170 ni wanafunzi wapya na 324 wanaoendelea. Wanafunzi hao wapo katika hatua mbalimbali za muda wa mafunzo. Mwaka wa kwanza wanafunzi 170, mwaka wa pili wanafunzi 146, mwaka wa tatu wanafunzi 132 na mwaka wa nne wanafunzi 46. Mafunzo haya yanajumuisha fani mbalimbali za utaalam ukiwemo upasuaji wa magonjwa ya moyo. Daktari mmoja anamaliza mafunzo ya uzamivu katika taaluma ya moyo. Aidha, Wizara iliendelea kuimarisha ushirikiano na nchi za China, Cuba na India katika kutoa mafunzo kwa utaratibu wa kupeleka wanafunzi katika nchi hizo na wao kuleta wataalam hapa nchini. Pia mazungumzo na nchi ya Israel kuhusu kupeleka wanafunzi wa uzamili na uzamivu yanaendelea.

***125*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hapa nchini ilifanya tathmini ya mafunzo ya kujiendeleza kwa masafa. Hadi sasa kozi tatu za Elimu ya Masafa zimeandaliwa na zinaendeshwa, ambazo ni; kozi ya Matabibu Wasaidizi kuwa

Matabibu "Stashahada", kozi ya Wauguzi ngazi ya cheti kuwa Wauguzi ngazi ya Stashahada kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Aga Khan. Aidha, hadi kufikia mwezi Juni, 2009, jumla ya wanafunzi 1,625 walidahiliwa na wanaendelea na masomo katika hatua mbalimbali katika kozi hizo. Mchanganuo wa waliodahiliwa ni kama ifuatavyo; Matabibu Wasaidizi kuwa Matabibu 879, Wauguzi ngazi ya cheti kuwa Wauguzi ngazi ya Stashahada 169 na waliojiunga na mafunzo ya Uuguzi ngazi ya cheti 577. Vilevile, Wizara iliendelea kutoa mafunzo ya Stashahada ya Menejimenti ya Huduma za Afya ngazi ya Wilaya.

***126 Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *International Training and Education Centre on HIV (ITECH)* ilifanya tathmini ya mafunzo ya masafa. Matokeo ya tathmini hiyo yatatumika kuandaa mipango ya kuboresha na kueneza mafunzo ya masafa ili yaweze kupatikana kwa wahitaji wengi zaidi. Aidha, tathmini hii inalenga kubaini maeneo ya kuimarishwa kwa mafunzo haya yanayotoa nafasi kwa watumishi kujiendeleza wakiwa katika vituo vyao vya kazi katika kupunguza uhaba wa watumishi wa afya uliopo nchini. Jumla ya Wauguzi Wakunga Wasaidizi Vijijini 639, Waganga Wasaidizi Vijijini 877 na Wauguzi ngazi ya cheti 71 walidahiliwa kujiendeleza kwa njia ya mafunzo ya masafa. Vilevile, Wizara iliendelea na maandalizi ya awali ya kuanzisha vyuo vya Madaktari Wasaidizi katika hospitali za mikoa ya Tabora na Mtwara pamoja na hospitali ya Peramiho mkoani Ruvuma. Zabuni ya ujenzi wa chuo cha Madaktari Wasaidizi cha Tabora ilitangazwa, Chuo cha mafunzo ya

Waganga Wasaidizi cha Mtwara kimepanuliwa na taratibu za Maandalizi ya ukarabati wa chuo cha Maafisa Ustawi Wasaidizi Kisangara yanaendelea.

**Kielelezo Na. 6: Udahili wa Wanafunzi katika vyuo vya afya nchini.**




**127** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina changamoto ya namna ya kupata rasilimali watu katika Sekta ya Afya wenye ujuzi na wa kutosha ili waweze kutekeleza malengo ya Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa III, MMAM, kuhimili ongezeko la kazi kunakotokana na kuongezeka kwa magonjwa yanayowakabili wananchi na mabadiliko ya Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) yanayoendelea.

**128 Mheshimiwa Spika,** katika kutatua changamoto hii, Wizara imetenga fedha katika bajeti ili kutoa mafunzo yanayoendana na wakati ili kukidhi mahitaji yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa III na MMAM. Aidha, Wizara inaendelea kupeleka watumishi wa kada mbalimbali za Afya katika Halmashauri. Vilevile, Wizara inaendelea kupanua, kukarabati na kufufua vyuo mbalimbali vya kutoa mafunzo katika Sekta ya Afya. Wizara pia, inahamasisha wadau mbalimbali pamoja na Mashirika ya Dini na Watu Binafsi kufungua vyuo vya kutoa mafunzo ya fani za afya.

**HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII**

**129 Mheshimiwa Spika,** Idara ya Ustawi wa Jamii, inatoa huduma kwa makundi maalum katika vitengo vifuatavyo: Kitengo cha Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu na Wazee; Huduma kwa Familia na Watoto; Malezi, Makuzi na Maendeleo kwa Watoto na Huduma ya Marekebisho ya Tabia na Haki za Watoto na Vijana. Muundo huu umefuatia mabadiliko yaliyoidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ya kuunda kitengo kipya cha kushughulikia masuala ya watoto walio katika mkinzano na sheria kinachojulikana kama Marekebisho ya Tabia na Haki za Watoto na Vijana "*Juvenile Justice and Correctional Services*". Aidha, Huduma ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia ilihamia Wizara ya Mambo ya Ndani.

**130 Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na wadau kupitia Mpango wa kujenga uwezo kuhusu huduma kwa watoto

walio katika mazingira hatarishi, ilitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa mkoa wa Dodoma kuhusu majukumu ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi ya Halmashauri. Mafunzo hayo yalijumuisha viongozi na watendaji 70 kutoka katika Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri tano za mkoa wa Dodoma.

***131*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilikamilisha rasimu ya Sera ya huduma za ustawi wa jamii. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mikoa iliziwezesha Halmashauri 81 kuendeleza mpango shirikishi jamii wa utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi. Jumla ya watoto 611,150 walitambuliwa, wa kike ni 293,352 sawa na asilimia 48 na wa kiume ni 317,798 sawa na asilimia 52. Watoto hao wanapatiwa huduma katika jamii ikiwa ni pamoja na huduma za afya, msaada wa chakula, mahitaji ya shule na ushauri wa kisaikolojia. Vilevile, Wizara ilisambaza nakala 6,000 za mpango kazi wa Taifa wa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi kwenye Halmashauri zote na wadau wengine.

***132*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilitoa huduma za chakula, malazi, afya na elimu kwa makundi maalum katika makazi, makao, vyuo, mahabusi za watoto na shule ya maadilisho Irambo Mbeya. Jumla ya wahudumiwa 2,000 walipatiwa huduma hizi, ambao ni wazee wasiojiweza na watu wenye ulemavu 885, watoto 140 kutoka makao ya Taifa ya watoto na kituo cha ustawi wa mama na mtoto Ilonga, mahabusu 799 na waadiliwa 176 kutoka shule ya maadilisho Irambo. Aidha, Wizara iliwawezesha vijana 230

kutoka makao ya watoto Kurasini, Mahabusi za watoto na Shule ya Maadilisho kupata mafunzo ya ufundi stadi. Vilevile, Wizara iliboresha mafunzo yanayotolewa katika vyuo vitatu vya ufundi kwa watu wenye ulemavu kwa kugharamia vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Jumla ya vijana 133 walihitimu mafunzo ya ufundi stadi katika fani mbalimbali.

**133** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliendelea na ujenzi wa maktaba ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Mahabusi ya watoto ya Mtwara. Aidha, Wizara ilikamilisha taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ukarabati wa madarasa na mabweni katika vyuo vya ufundi kwa watu wenye ulemavu vya Luanzari – Tabora, Mbeya na chuo cha wasioona Singida. Vilevile, Wizara iliboresha huduma katika shule ya maadilisho Irambo kwa kufanya ukarabati wa mabweni na bwalo la chakula pamoja na kuweka vifaa vya malazi kwa waadiliwa 70.

**134** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika mwaka 2008/09, Wizara ilikuwa na changamoto ya ongezeko la makundi mbalimbali yenye mahitaji maalum, yanayoishi katika mazingira hatarishi kutokana na sababu za kiuchumi, kijamii na matokeo ya VVU/UKIMWI.

**135** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutatua changamoto hii, Wizara inaendelea kutenga fedha katika bajeti yake ili kuyahudumia makundi hayo. Aidha, Wizara inahamasisha jamii iwatambue na kuwatunza watu walio katika mazingira hatarishi

katika familia zao na jamii wanayotoka kwa kuzingatia misingi ya haki na usawa. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane katika kuhamasisha jamii katika majimbo yetu.

**WAKALA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII**

**WAKALA**

**Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali**

***136*** ***Mheshimiwa Spika***, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ulichangia katika kulinda afya ya jamii, mazingira na utoaji haki kwa kufanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli mbalimbali na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya kemikali za viwandani na majumbani ili kuhakiki ubora na usalama kwa watumiaji na mazingira.

***137*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wakala ilinunua mitambo mitatu ya kisasa, vifaa, vitendanishi na kemikali ambazo zilifanikisha kufanya uchunguzi wa ubora na usalama wa sampuli 837 zinazohusu vyakula, dawa, kemikali, maji, maji taka na bidhaa zingine za viwandani. Aidha, Wakala uligharamia mafunzo ya mtumishi mmoja nchini Uingereza kujifunza matumizi ya mitambo na matengenezo kinga ili kupunguza gharama ya kuwalipa wataalam kutoka nje ya nchi.

***138*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wakala kwa kutumia teknolojia ya vinasaba ulichunguza sampuli 7,718 zinazohusu matatizo ya kijamii na makosa ya kijinai zikijumuisha

mzazi halali wa mtoto, mimba kwa wanafunzi ili kutambua wahusika, watoto wanaozaliwa na jinsia mbili ili kutambua jinsia iliyo na nguvu, ubakaji, mauaji na ujambazi. Pia, dawa za kulevya na aina mbalimbali za sumu zilichunguzwa.

***139*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, wataalam wa Wakala walishiriki katika kikosi kazi kinachojumuisha wataalam kutoka vyombo vya dola kilichoundwa na Serikali kufanya uhakiki wa majalada ya kesi zenye utata na kuchukua sampuli za watuhumiwa wanaohusishwa na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi "*Albino*", vikongwe, majambazi na dawa za kulevya kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara katika mikoa minne ya Kanda ya Ziwa ili kusaidia vyombo vya dola kutenda haki.

***140*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wakala uliimarisha usimamizi wa Sheria ya kemikali za viwandani na majumbani kwa kufanya ukaguzi katika viwanda na maghala 206, vituo vyote vya mipakani, bandarini na viwanja vya ndege. Aidha, Wakala ulitoa vibali 5,260 kwa wafanyabiashara wanaoingiza kemikali kutoka nje na wafanyabiashara wawili walifikishwa mahakamani kwa kusafirisha kemikali hatari aina ya "cyanide" kwenda migodini bila ya kufuata taratibu na kuhukumiwa kulipa faini ya shilingi milioni 36. Mafunzo ya ukaguzi yalitolewa kwa Maafisa 57 wa Forodha, Maafisa Afya na Polisi wanaokagua kemikali kupitia vituo 11 vya mipakani.

***141*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wakala uliendelea kuimarisha ushirikiano na

Taasisi za ndani na nje ya nchi zinazoshughulikia usimamizi wa kemikali hususan kupitia mradi wa "*Strategic Approach to International Chemicals Management - SAICM*" ili kulinda afya ya binadamu na mazingira. Aidha, Wakala ulishiriki katika miradi ya ubunifu katika Utumishi wa Umma Barani Afrika "*All Africa Public Service Innovation Award*" mwaka 2008 na Tanzania ilipata zawadi ya mshindi wa kwanza kwa usimamizi mzuri wa kemikali nchini.

***142*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wakala uliendelea na ujenzi wa Maabara ya Kanda ya Kaskazini mjini Arusha na kupata eneo/kiwanja cha ujenzi wa Maabara ya Nyanda za Juu Kusini jijini Mbeya ili kupeleka huduma karibu na wananchi na kuokoa gharama za usafiri kufuata matokeo ya uchunguzi na huduma zingine jijini Dar es Salaam.

***143*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wakala uliendelea na mchakato wa kupata hati ya ithibati katika njia za uchunguzi kwenye maikrobaiolojia na viuatilifu ili matokeo yanayotolewa yatambulike kimataifa. Aidha, Wakala uliboresha baadhi ya miongozo na kutoa mafunzo ya uzamili, shahada, cheti na kozi za muda mfupi kwa watumishi 18 wa kada mbalimbali ili kuwaongezea ujuzi na kukidhi mahitaji ya Shirika la Kusimamia Ithibati la Afrika Kusini "*SANAS*" linalotoa hati ya ithibati. Vilevile, Wakala ulipitia Miundo ya Watumishi na Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kuwasilisha kwenye Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa Wakala "*MAB*" na kupitishwa.

**Mamlaka ya Chakula na Dawa**

***144*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka inasimamia ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa kufanya ukaguzi wa majengo ya kufanyia biashara na viwanda vya kutengeneza bidhaa hizo ndani na nje ya nchi, kuzifanyia tathmini na kuzisajili kabla ya kuruhusiwa kwa matumizi. Aidha, Mamlaka inashirikiana na wakaguzi wa chakula na dawa walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na wale walioko katika vituo vya mipakani kwa kufanya ukaguzi wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba, kabla ya kuviidhinisha kuingizwa nchini.

**145** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Mamlaka, ilisajili jumla ya dawa za binadamu 410, dawa za mifugo 43, aina 34 za vipodozi na dawa za majaribio 5. Aidha, majengo 1,934 yakufanyia biashara ya dawa na vipozozi yalikaguliwa, kati ya hayo 470 ni famasi, 750 Maduka ya dawa baridi, 504 Maduka ya Dawa Muhimu na 210 ya vipodozi. Vilevile, maeneo 20 ya majaribio ya dawa yalikaguliwa. Mamlaka pia ilikagua viwanda 39 vya kutengeneza dawa nje ya nchi na viwanda 7 vya kutengeneza dawa ndani ya nchi. Katika kupambana na bidhaa bandia na zenye kiwango duni, Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi nchini na Polisi wa Kimataifa "*INTERPOL*" iliendesha misako ya kushitukiza katika maeneo mbalimbali nchini na kubaini dawa bandia zikiwemo dawa aina ya *Metakelfin, Celestamine, Gentrisone,* dawa za mifugo aina ya *Broiler Boost Formula, Egg boost formula 500 gm, Chick mycin 100 gm, cocci vet na piper zine citrate* na hatua zilichukuliwa kwa kuitahadharisha jamii.

Pia, dawa na vipodozi vyenye uzito wa tani 38.5 viliteketezwa kwa kutokidhi viwango.

146 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Mamlaka ilipokea na kufanyia tathmini taarifa 133 za madhara yatokanayo na dawa na matukio makali "*Serious adverse events*" 120 yatokanayo na majaribio ya dawa. Madhara hayo yalionekana kuwa ni ya kawaida ambayo mtengenezaji ameyaorodhesha kama madhara tarajiwa kwa watumiaji wa dawa husika.

147 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Mamlaka ilikagua majengo 402 ya kufanyia biashara za vyakula na kusajili jumla ya vyakula vilivyofungashwa 175. Aidha, Mamlaka ilifanya msako na kupiga marufuku uingizaji wa Maziwa aina ya NIDO 1 toleo namba 8179018S 02 E 1M na Lactogen 1 toleo namba 82050179L baada ya kugundulika kuwa yalikuwa yamechafuliwa kwa kutiwa kemikali ya "*melamine".* Tani 33.9 za maziwa aina ya "*Golden Bell*" kutoka China yalizuiwa kuingizwa sokoni baada ya kugundulika kuwa yamechafuliwa na kemikali aina ya *melamine* na taratibu za kuyaharibu zinaendelea. Vilevile, chakula chenye uzito wa tani 3,057 kiliteketezwa kwa kutokidhi viwango na hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu. Mamlaka pia, iliendelea na utekelezaji wa mfumo wa majaribio wa ukusanyaji taarifa za magonjwa yatokanayo na kula chakula "*Food Borne Diseases*" katika Halmashauri 17 za Mikoa ya Singida, Dodoma na Manyara.

148 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Mamlaka iliendelea kuratibu na kusimamia

utekelezaji wa Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu "*ADDO*" katika Mikoa ya Mbeya, Kigoma, Singida, Lindi, Pwani na Tanga na hivyo kufikia jumla ya mikoa kumi ambayo mpango wa ADDO tayari umeshaenezwa. Aidha, Mamlaka ilifanya uchunguzi wa kimaabara wa jumla ya sampuli 709, kati ya sampuli hizi, 422 za vyakula, 268 za dawa na 19 za vipodozi. Vilevile, Mamlaka ilikagua jumla ya shehena 343 za vyakula na 600 za dawa katika vituo vya forodha vya Uwanja wa Ndege wa J.K. Nyerere, Bandari ya Dar es Salaam na Namanga na kuruhusu kuingizwa nchini baada ya kukidhi viwango. Mamlaka pia, ilikamilisha hatua za awali za mchakato wa kupata ithibati ya kimataifa ya Maabara yake ili iweze kutambulika kimataifa.

***149*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Mamlaka ilifanya usimamizi na ufuatiliaji wa kazi za maabara ndogo 10 za dawa na 13 za kupima madini joto kwenye chumvi ikiwa ni pamoja na kutoa kemikali, vitendanishi na mafunzo kwa watendaji wa maabara hizi. Aidha, Mamlaka iliandaa na kurusha jumla ya vipindi 10 vya Radio na matangazo mafupi 10 ya radio na ilishiriki katika vipindi vinne maalumu vya televisheni. Vipindi vyote vililenga kuielimisha jamii juu ya kazi na majukumu ya Mamlaka. Vilevile, Mamlaka ilishiriki katika maonesho mbalimbali ikiwa ni pamoja na Maonesho ya 32 ya Kimataifa ya Biashara "Maonesho ya Saba Saba" yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Maonesho katika viwanja vya Bunge na Maonesho katika Sikukuu ya Wakulima yaliyofanyika Mkoani Dodoma, lengo likiwa ni kutoa elimu kwa jamii.

**TAASISI**

**Taasisi ya Chakula na Lishe**

***150*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Chakula na Lishe ilitoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri na ilishirikiana na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali pamoja na Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa afua za lishe zinazolenga kuboresha lishe ya wananchi hasa makundi yanayoathirika zaidi na lishe duni. Makundi hayo ni pamoja na watoto wachanga na walio chini ya miaka mitano, wanawake wajawazito, wanaonyonyesha na wazee.

***151*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi kwa kushirikiana na wadau wengine iliendeleza juhudi za kuratibu uongezaji wa virutubishi kwenye vyakula vitatu vilivyochaguliwa ambavyo ni mafuta ya kula, unga wa ngano na mahindi. Aidha, Taasisi ilishirikiana na wadau mbalimbali kutengeneza Mpango wa Maendeleo wa Kitaifa wa kuongeza virutubishi kwenye vyakula. Vilevile, Taasisi iliratibu utayarishaji wa miongozo na vijitabu vya maelekezo ya uongezaji virutubishi kwenye vyakula viwandani na kanuni za kitaifa za uongezaji virutubishi kwenye vyakula vilivyochaguliwa. Taasisi pia, ilishiriki katika utayarishaji wa viwango vya kuongeza virutubishi kwenye vyakula.

***152*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilitoa mafunzo ya kuboresha uzalishaji wa chumvi yenye madini joto kwa wakufunzi 136 ambao ni wazalishaji chumvi wadogo nchini. Wazalishaji hao wadogo wa chumvi walitoka katika

Halmashauri za Wilaya za Kigoma, Iramba, Singida, Manyoni, Bahi, Chamwino, Meatu, Hanang, Babati, Korogwe, Muheza, Pangani, Bagamoyo, Mkuranga, Rufiji, Kilwa, Manispaa za Singida, Kinondoni, Temeke, Dodoma, Lindi, Mtwara na Jiji la Tanga. Aidha, Taasisi ilisimamia mafunzo yaliyotolewa na wakufunzi hao kwa wazalishaji chumvi wadogo 1,567 kwenye maeneo hayo. Vilevile, Taasisi iliielimisha jamii kupitia vyombo vya habari ikiwemo radio kuhusu madhara ya upungufu wa madini joto mwilini na umuhimu wa kutumia chumvi yenye madini joto.

**153** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilitoa mafunzo kuhusu huduma na matunzo ya lishe kwa watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (VVU) kwa wanasihi na watoa huduma majumbani 88 katika Halmashauri za Wilaya za Hai na Moshi na Manispaa ya Moshi na Wilaya nane za Mkoa wa Mbeya na sita za Mkoa wa Iringa. Mafunzo hayo yalihusisha ugawaji wa machapisho mbalimbali 3,200 kuhusu matunzo kwa watu wanaoishi na VVU. Aidha, Taasisi ilitoa elimu ya lishe kwa jamii kwa ujumla kupitia vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo magazeti, radio na televisheni.

**154** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilitoa mafunzo ya wakufunzi kuhusu ulishaji wa watoto wachanga na wadogo walio katika maambukizi ya VVU yaliyofanyika kwa wafanyakazi wa afya katika Halmashauri za Wilaya na Manispaa 11 za majaribio Tanzania Bara. Halmashauri za Wilaya hizo ni Magu, Ngara, Kasulu, Kibondo, Kigoma, Hai, Siha, Makete, Bagamoyo na Manispaa za Temeke na Mtwara. Jumla ya

watoa huduma wa afya 26 walihudhuria na kufuzu mafunzo hayo. Aidha, mafunzo ya wasimamizi wa sheria inayohusu uuzaji na usambazaji wa vyakula vya watoto wachanga yalitolewa kwa Maafisa Afya 20 kutoka vituo vya Bandarini, Viwanja vya ndege na Mipakani pamoja na wahariri na waandishi wa habari 22 kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza uwezo wa kusimamia uingizwaji wa maziwa na vyakula vya watoto nchini ili kuhakikisha vyakula hivyo vinazingatia vigezo vya ubora na usalama kwa afya ya watoto.

**155** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi iliandaa Mwongozo wa ulaji na mitindo ya maisha inayofaa ili kupunguza magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile Kisukari, Shinikizo Kubwa la Damu, Ugonjwa wa Moyo na aina mbalimbali za Saratani. Aidha, mwongozo wa ufuatiliaji na tathmini ya hali ya lishe kwa watu wanaoishi na VVU ulikamilika. Miongozo hiyo itasambazwa katika vituo vya tiba na taasisi mbalimbali nchini.

**156** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Taasisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea na juhudi za kutatua tatizo la upungufu wa Vitamini A. Aidha, Taasisi iliratibu ugawaji wa matone ya Vitamini A na dawa za Minyoo. Jumla ya watoto 6,110,533 kati ya watoto walengwa 6,416,647 (sawa na asilimia 95.9) walipata matone ya Vitamini A na watoto 5, 145,467 kati ya watoto walengwa 5,661,598 (sawa na asilimia 91) walipata dawa za Minyoo katika zoezi lililofanyika Desemba 2008.

**157** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi iliendelea kuhamasisha jamii na kusisitiza juu ya usindikaji na matumizi ya zao la muhogo. Mradi wa kuongeza thamani ya zao la muhogo unaotekelezwa katika nchi tano za Africa zikiwemo Ghana, Nigeria, Malawi, Uganda na Tanzania ulizinduliwa. Kwa hapa Tanzania tafiti muhimu zilifanyika katika kanda za Kusini, Mashariki na Ziwa Victoria na kuchagua Kanda ya Kusini kuwa eneo ambalo mradi utaanza kutekelezwa.

**158** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Taasisi iliandaa mwongozo wa tiba ya utapiamlo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Mwongozo huo utatumiwa na watoa huduma wa hospitali na katika ngazi ya jamii. Aidha, Taasisi ilitoa mafunzo ya tiba ya utapiamlo kwa watoa huduma wa afya katika Halmashauri 17 za mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Morogoro, Kagera, Pwani na Kigoma. Lengo likiwa kuwawezesha kutekeleza ipasavyo tiba ya utapiamlo ili kuboresha kwa haraka afya za watoto wenye utapiamlo. Mafunzo hayo yalifanyika sambamba na uhamasishaji wa viongozi katika Halmashauri husika.

**Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu**

**159** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu ina majukumu ya kusimamia, kuratibu na kukuza utafiti nchini. Jukumu hili linatekelezwa kupitia vituo vya Muhimbili, Muheza, Bombo - Tanga, Mwanza na Tabora vikisaidiwa na vituo vidogo vya Mbeya, Tukuyu, Kilosa na Hydom. Aidha, jukumu hili la kufanya utafiti wa afya ya jamii hapa nchini

linapata mwongozo wake kutoka Mpango Mkakati wa Taasisi wa Miaka Mitano 2008/2009 hadi 2012/2013.

**160** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilishiriki katika utafiti wa awali wa chanjo ya Malaria ambayo ilionekana kuwa na nguvu ya kinga ya asilimia 55. Hii ni chanjo ya kwanza kuonyesha nguvu ya kinga ya juu kiasi hicho hapa nchini. Aidha, Taasisi ilifanya utafiti wa njia bora zaidi ya kutibu wagonjwa wa Kifua Kikuu na UKIMWI. Utafiti huu uliwahusisha wadau kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Mwanza na Morogoro. Utafiti huu kwa sasa unaendelea kwa lengo la kutoa majibu sahihi na bora zaidi. Vilevile, Taasisi ilishirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili, katika kutafiti chanjo ya UKIMWI hapa nchini. Matokeo ya utafiti huu bado yanaendelea kukusanywa na kuchambuliwa hatua kwa hatua kabla ya kutoa majibu rasmi.

**161** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Taasisi ilifanya mafunzo ya uongozi kwa kamati za afya za Halmshauri za Wilaya 16 za Sumbawanga, Kyela, Mbinga, Kilolo, Ilemela, Musoma, Kasulu, Bariadi, Kondoa, Hanang, Manyoni, Same, Kilwa, Tandahimba, Liwale na Rufiji. Jumla ya washiriki 115 kutoka Halmashauri hizo walishiriki mafunzo hayo. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa kuzijengea uwezo wa kufanya tafiti ndogo ndogo kwenye maeneo yao ili kuikinga jamii kutokana na majanga mbalimbali ya kiafya.

**162** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi kwa kushirikiana na kituo cha Tanga *AIDS*

*Working Group*, ilifanya utafiti wa dawa asilia zinazotumiwa na waathirika wa UKIMWI. Tangu mwaka 2005 hadi sasa waathirika wa UKIMWI 5,600 wametumia tiba kutoka kituo hiki. Utafiti huu umeonesha kuwa tiba hii imepunguza na kuzuia magonjwa nyemelezi kama Vidonda Midomoni na kwenye Ngozi, Homa, Kuhara, Mkanda wa Jeshi na Magonjwa ya njia ya hewa *(pneumonia).* Vilevile, tiba hii imeonesha kuzuia kupungua uzito kwa waathirika na kwamba chembechembe za CD4+ zimeonekana kuongezeka kwa wagonjwa walio katika tiba. Mradi huu umeombewa fedha kutoka mfuko wa Bill Gates kwa utafiti zaidi.

***163*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilikamilisha utafiti wa mgawanyo wa dawa na huduma mbalimbali za afya kwa jamii hapa nchini, *"Integrated Community-Directed Interventions"*. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kukubalika na jamii mfumo wa usambazaji wa vyandarua kwa mama wajawazito na ugawaji wa dawa za matone ya Vitamini-A. Aidha, Taasisi ilichukua sampuli 85 za ugonjwa wa Malale kutoka kwa wananchi wa Halmashauri za Wilaya za Kasulu, Kibondo na Urambo kwa ajili ya kufanya utafiti na kutathmini usugu wa dawa za tiba ya Malale katika Kanda ya Magharibi. Vilevile, Taasisi ilishirikiana na Asasi nyingine kusambaza dawa za Matende na Ngiri Maji katika mikoa sita ya Pwani, Tanga, Lindi, Mtwara, Morogoro na Dar es Salaam na kunufaisha jumla ya wananchi milioni 9.4. Pia, jumla ya wananchi 200 walifanyiwa upasuaji wa Ngiri Maji chini ya Mfuko Maalumu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kutokomeza Matende.

**164 Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2008/09, Taasisi ilifanya majaribio ya Chanjo dhidi ya virusi vya *Papilloma* vinavyosababisha Saratani ya Shingo ya Uzazi kwa wanawake jijini Mwanza. Aidha, washiriki 252 kati ya walengwa 333, wamechanjwa dawa mara tatu kwa hatua tatu tofauti na kufuatiliwa kwa kipindi cha miezi 12 tangu walipopata chanjo ya kwanza, ili kuangalia usalama wa chanjo hiyo na kubaini ubora wake kwa afya ya jamii. Vilevile, Taasisi ilitoa mafunzo ya namna ya kujaza takwimu za upimaji na utumiaji wa kipimo cha maambukizi ya Kaswende *"Rapid Syphillis Test"* katika kliniki zote za akina mama wajawazito Wilayani Geita. Lengo ni kuwa ifikapo mwezi Agosti 2009 kipimo hicho kiwe kinatumika katika kliniki zote Wilayani Geita.

**165 Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008/09, Taasisi ilifanya utafiti wa kuoanisha uhusiano uliopo kati ya tohara kwa wanaume na maambukizi ya UKIMWI. Utafiti huu ulifanyika katika Halmashauri za Wilaya za Bukoba, Ileje na Tarime, na Manispaa za Musoma na Bukoba na Jiji la Mbeya. Aidha, Taasisi ilifanya utafiti wa kuainisha changamoto zilizopo katika kuwashirikisha ghariba ili kutoa tohara salama katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Jumla ya wananchi 591 kutoka Halmashauri za Wilaya za Monduli, Bahi na Mkuranga walishiriki utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yatasaidia kutoa dira itakayowashirikisha ghariba katika kupiga vita maambukizi ya UKIMWI vijijini.

**166 Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008/09, Taasisi kupitia Mfuko wa Utafiti *"Health Research Users' Trust Fund"* iliwalipia watafiti chipukizi

gharama za rasimu zao 21 walizowasilisha zikiwa ni maombi ya ufadhili. Aidha, hali ya utoaji vibali kwa rasimu za utafiti uliboreshwa baada ya kuwapo kikao kimoja kila mwezi cha kutoa idhini kwa rasimu hizo kufanya utafiti uliokusudiwa na hivyo Taasisi ilipitisha jumla ya rasimu 111 na kutoa vibali vya utafiti kwa watafiti wa ndani na nje ya nchi.

***167*** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa maabara ya kisasa ya utafiti na utengenezaji wa dawa asili katika viwango vinavyokubalika katika tiba ya kisasa ulikamilika. Maabara hii inatarajiwa kukabidhiwa rasmi kwa Taasisi mwishoni mwa mwaka 2009. Aidha, Taasisi ilianzisha ushirikiano na wataalam wa Tiba Asili na waliainisha Tiba Asili zinazohitaji utafiti wa kina zaidi na zile ambazo utengenezaji wa dawa zake unatakiwa uanze mara moja.

**Taasisi ya Ustawi wa Jamii**

***168*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliongeza idadi ya udahili wa wanafunzi katika fani mbalimbali za Ustawi wa Jamii, Menejimenti ya Rasilimali Watu, Uongozi Kazi na Ushauri Nasaha zinazotolewa na Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Aidha, wanafunzi waliodahiliwa waliongezeka kutoka 2,098 mwaka 2007/08 hadi kufikia 2,448 mwaka 2008/09. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 20 na linalenga kukidhi mahitaji katika fani hizo. Vilevile, Taasisi kwa mara ya kwanza imetoa wahitimu 501 wa shahada ya kwanza katika fani za huduma za Ustawi wa Jamii, Uongozi Kazi na Rasilimali Watu kwa mwaka wa masomo 2008/09.

***169*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara iliendelea na awamu ya tatu ya ujenzi wa

maktaba ya kisasa, ambapo ujenzi wa nguzo hadi ghorofa ya pili umekamilika. Aidha, Wizara ilipata eneo lenye ukubwa wa ekari 169 katika eneo la kijiji cha Msoga,- Chalinze, Wilaya ya Bagamoyo ambalo litaendelezwa ili kupanua utoaji wa mafunzo ya Ustawi wa Jamii katika fani za Ushauri Nasaha, Ustawi wa Jamii na Maendeleo, Masuala ya UKIMWI, Sera za Kijamii, Huduma za Watoto, Huduma za Wazee, Makundi yaliyokuwa katika Mazingira Hatarishi na Utafiti.

**Bohari ya Dawa**

***170*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Bohari iliongeza upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kutoka asilimia 70 hadi asilimia 80. Aidha, Bohari iliboresha utendaji na ufanisi kwa kukasimu baadhi ya madaraka kwa Bohari za Kanda ili kuimarisha mfumo wa usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa lengo la kufikisha huduma karibu na wateja wake. Vilevile, Bohari ilianzisha mfumo unaojulikana kama "*Total Quality Management System*". Mfumo huu unaweka vigezo maalum vya kuhakiki ubora wa bidhaa na utoaji wa huduma.

***171*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Bohari ilikamilisha ujenzi wa maghala mawili katika Bohari za Kanda za Iringa na Moshi. Ujenzi wa maghala hayo uliongeza uwezo wa kuhifadhi na kufungasha dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Bohari ya Kanda ya Moshi iliongeza uwezo wake kwa mita za mraba 700 na Bohari ya Kanda ya Iringa kwa mita za mraba 1,100. Aidha, Bohari iliendesha mikutano na wadau wake katika Bohari za Kanda za Moshi, Tanga, Iringa, Mbeya, Mtwara,

Dodoma na Tabora. Lengo la mikutano hiyo ilikuwa kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja wake. Washiriki wa mikutano hiyo walikuwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa, Waganga Wafawidhi wa Hospitali na Wafamasia wa Wilaya na Mikoa.

**MIRADI YA MAENDELEO**

***172*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilitengewa **shilingi 242,067,318,100.00**. Kati ya fedha hizo, Serikali ya Tanzania ilitenga jumla ya **shilingi 13,029,173,000.00** na Wahisani wanaosaidia sekta ya afya walitenga **shilingi 229,038,145,100.00**. Hadi kufikia Mei 2009, Wizara ilikuwa imeshapokea **shilingi 183,305,846,518.00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 10,000,000,000.00** zilitolewa na Serikali na **shilingi 173,305,846,518.00** zilitolewa na Wahisani. Fedha zilizotolewa zilitumika kutekeleza kazi zifuatazo:

***173*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kutumia fedha zilizotolewa na Awamu ya Pili ya Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma, ilitoa mafunzo juu ya ujazaji wa fomu za Upimaji wa Utendaji Kazi wa Mtumishi kwa watumishi wote wa Wizara. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya kuboresha mfumo wa utunzaji kumbukumbu kuwa wa ki-elektroniki kwa watunza kumbukumbu 14.

***174*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilikarabati jengo la meno, iligomboa na kufunga vifaa vya huduma na kufundishia, pia ilifunga vifaa vya kusafishia figo na CT Scan

katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Aidha, Wizara iliendelea kukarabati hosteli za wanafunzi wa Uuguzi na Sayansi Shiriki katika hospitali hiyo. Vilevile, ilikarabati jengo la Taasisi ya Mifupa Muhimbili – "*MOI*" na kufanya matengenezo kinga ya mitambo, vyumba vya wagonjwa mahututi na vifaa vya upasuaji. Wizara pia, ilikarabati jengo katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road kwa ajili ya huduma ya *Telemedicine,* kuandaa michoro na makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa wodi na kuimarisha huduma za mkoba mikoani.

***175*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilinunua samani kwa ajili ya jengo la mihadhara chuo cha MUHAS. Jengo hili sasa linaweza kuchukua wanafunzi 700 wakiwa wameketi badala ya wanafunzi 350 wa hapo awali.

***176*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilijenga uzio wa wodi ya wanawake katika hospitali ya Mirembe na tanuru la kuchomea taka katika Taasisi ya Isanga. Aidha, iliendeleza ujenzi wa kituo cha Itega kwa ajili ya watu walioathirika na dawa za kulevya na ilikarabati nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Mirembe. Vilevile, Wizara ilijenga jengo la kuhifadhi maiti na ilikarabati nyumba ya Mganga Mkuu na Daktari Mfawidhi. Wizara pia, ilikarabati wodi tatu za wagonjwa wa akili na majengo matatu yaliyo katika eneo la Mirembe *Annex* ili yatumike kama mabweni ya wanafunzi na ilinunua samani za hospitali hiyo.

***177*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilikamilisha ujenzi wa uzio wa Hospitali ya Kibong'oto na ilinunua samani za hosteli ya

madaktari wanafunzi na za maabara ya Hospitali ya Rufaa Mbeya. Aidha, Wizara ilikarabati jengo la Hospitali ya Bugando.

***178 Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara ilianza maandalizi ya michoro na makabrasha ya zabuni ya Hospitali Maalum Kanda ya Kusini - Mtwara. Michoro hiyo inajumuisha majengo ya hospitali pamoja na uzio kuzunguka eneo lililopangwa. Katika kuimarisha huduma za ngazi ya rufaa, Wizara imezipandisha hadhi hospitali zote za mikoa ili kutoa huduma za ngazi ya rufaa "*tertiary care*". Hospitali za rufaa nazo zinaongezewa uwezo wa kutoa huduma maalum "*super specialized care*" na kuzifanya ziwe hospitali maalum.

***179 Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliiwezesha Mamlaka ya Chakula na Dawa kuendeleza Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu. Aidha, Wizara imeuwezesha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuboresha huduma katika kanda zote zilizoanzishwa pamoja na kufanya tathmini ya Uhai wa Mfuko. Vilevile, Wizara iliendelea na ujenzi wa Maabara ya Tiba Asili – Mabibo kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu. Wizara pia, iliimarisha huduma za chanjo, afya ya uzazi na mtoto, kinga dhidi ya UKIMWI, magonjwa ambayo hayakupewa msukumo unaostahili, Kifua Kikuu na Ukoma.

***180 Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) kwa hatua, kwa kuongeza idadi ya wanafunzi watarajali kufikia 3,831 ambayo

ni asilimia 60 ya lengo la kudahili wanafunzi 6,450 kwa mwaka. Aidha, ukarabati wa vyuo 29 vilivyopo na kuvifufua vyuo vilivyofungwa vya Mpanda, Nachingwea, Nzega na Kibondo umeendelea vizuri ikiwa ni mkakati mmojawapo wa kuongeza udahili wa wanachuo. Vyuo hivi vinategemewa kuanza kupokea wanafunzi mwezi Januari 2010. Vilevile, Mashirika ya Dini na Sekta Binafsi kwa ujumla yanahamasishwa kupanua au kufungua vyuo vya afya nchini.

***181*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Kanda zote nane za Mafunzo nchini ziliandaa Mpango Mkakati unaotoa kipaumbele katika kuongeza wataalam ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM). Mpango Mkakati huo utaziwezesha Kanda za Mafunzo kusimamia na kuratibu mafunzo ya kujiendeleza na vyuo vya afya katika ngazi za mikoa na wilaya.

***182*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara iliendelea na ujenzi wa maktaba ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Mahabusi ya watoto ya Mtwara. Aidha, Wizara ilikamilisha taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ukarabati wa madarasa na mabweni katika vyuo vya ufundi kwa watu wenye ulemavu vya Luanzari – Tabora, Mbeya na Chuo cha Wasioona, Singida.

**Mabadiliko katika Sekta ya Afya**

***183*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2008/09, Wizara iliendelea na uraghibishaji wa jamii kuhusu mabadiliko yanayoendelea katika Sekta ya Afya kupitia programu za Afya, Mambo

Mapya na Afya katika Radio na Televisheni. Hadi Juni 2009 jumla ya programu za uraghibishi 132 zilitangazwa na Shirika la Utangazaji Tanzania - "*TBC*" Taifa kwa kushirikiana na $TBC_1$. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na watangazaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania ilitembelea Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mikoa, Hospitali na vituo mbalimbali vya huduma katika mikoa ya Singida, Dodoma, Mara, Mwanza, Shinyanga, Mbeya, Mtwara, Lindi, Kilimanjaro, Pwani na Morogoro. Zoezi hilo lilihusu kudodosa, kufanya majadiliano na kurekodi vipindi vipya vinavyoakisi hali halisi na mwelekeo wa utoaji huduma za afya katika ngazi mbalimbali za utekelezaji. Vipindi vilivyorekodiwa vinaendelea kurushwa katika programu za TBC na maandalizi ya kusambazwa kwenye redio na televisheni zilizoko mikoani yamekamilika.

***184 Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara ilipitia mabango matatu, bango kitita moja, vijitabu viwili, vipeperushi vinne vya uraghabishi wa mabadiliko na kuoanisha ujumbe na maudhui yake na Sera ya Afya ya mwaka 1990 iliyopitiwa mwaka 2007, MMAM 2007 – 2017 na Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya 2009 – 2015. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilifanyia majaribio nyenzo hizo, kwa lengo la kuhakikisha kuwa zinakidhi mahitaji ya walengwa kabla ya kuchapishwa na kusambazwa. Vilevile, Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) ulizinduliwa mwezi Machi mwaka huu kwenye mkutano wa mwaka wa Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya uliofanyikia mkoani Mbeya. Pia, Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa tatu, 2009 – 2015 ulizinduliwa

tarehe 30 mwezi Juni 2009 na Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na umeanza kutekelezwa kuanzia tarehe 1 Julai, 2009.

**Uendeshaji wa Huduma za Afya katika Halmashauri**

185 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliendelea kusimamia na kuboresha huduma za afya katika Halmashauri na Mikoa. Wizara ilitoa mafunzo yaliyolenga kuziwezesha Timu za Uendeshaji za Afya za Mikoa na Maafisa wa Sekretariati za Mikoa ili ziweze kufanya uchambuzi wa kina wa Mipango na Taarifa za utekelezaji wa Mipango Kabambe ya Afya kutoka Halmashauri. Aidha, Wizara iliandaa taarifa ya kina itakayokidhi matakwa ya Serikali na Wadau wa Maendeleo wa Mfuko wa Pamoja wa Afya. Vilevile, kwa kupitia taarifa itakayotolewa na mikoa tutaweza kuangalia mwenendo wa utoaji huduma katika ngazi za Halmashauri na pia kuidhinisha kutolewa fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya kwenda Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji na hivyo kuboresha huduma za afya.

186 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliandaa, ilisambaza na kutoa maelekezo ya matumizi ya Mwongozo kwa vituo vya afya na zahanati. Mwongozo huu unaelekeza namna ya kuandaa mipango ya afya kwa kushirikiana na Jamii katika ngazi hizo. Lengo ni kupeleka madaraka zaidi kwa wananchi ya kupanga na kutekeleza mipango yao.

Aidha, mafunzo ya Mwongozo huu yalitolewa kwa wakufunzi katika ngazi ya Mikoa, Halmashauri na Vyuo vya Mafunzo vya Afya vya Kanda ili waweze kutoa mafunzo kwa ngazi ya chini ya Halmashauri.

***187*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliandaa Mkakati na Mwongozo wa utekelezaji wa Malipo kwa Ufanisi Bora "*Payment for Performance - P4P*". Aidha, Mkakati huu unalenga kuimarisha utekelezaji wa Mkakati wa kupunguza vifo vya wanawake wajawazito, watoto wachanga na watoto wenye umri chini ya miaka mitano ili kuweza kufikia Malengo ya Maendeleo ya Millenia.

***188*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilifanya tathmini ya utendaji kazi wa Bodi na Kamati za Afya kwa kutumia Kituo cha Ifakara cha Utafiti. Aidha, matokeo ya utafiti yaliiwezesha Wizara kupitia Mwongozo wa uanzishaji wa Bodi za Huduma za Afya na Kamati za vituo. Nia ni kuhahikisha kuwa jamii inashiriki kikamilifu katika usimamizi na upokeaji taarifa za utekelezaji wa huduma za afya. Hii itasaidia uwajibikaji zaidi kwa watendaji ili kuinua kiwango na ubora wa huduma za afya.

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

***189*** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilianzisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kuboresha utaratibu wa uchangiaji huduma za matibabu nchini. Lengo ni kutoa unafuu wa gharama na

kumpa uhakika mtumiaji wa kupata huduma hizo pindi anapozihitaji, hata kama wakati huo hana fedha mfukoni. Kitaifa, Mfuko huu umekuwa ni chanzo imara cha mapato kinachojitegemea nje ya fedha za Bajeti ya Serikali kwa ajili ya kuhudumia na kuendeleza Sekta ya Afya.

**190** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Juni, 2009 Mfuko huu ulikuwa na wanachama 331,594, wanufaika milioni 1.8 na salio la akiba la shilingi bilioni 177.78. Mfuko uliendesha programu za elimu ya Kata kwa Kata kwenye Kata 732 Vijijini na kutunukiwa Cheti cha Heshima na Taasisi ya Kimataifa ya Hifadhi ya Jamii Duniani. Aidha, Mfuko uliendelea kuyafanyia kazi maagizo ya Serikali yaliyoutaka uwasilishe mapendekezo ya kitaalamu kuhusu namna bora ya kuisimamia Mifuko ya uchangiaji wa huduma za afya nchini ikiwemo Mfuko wa Afya ya Jamii. Hatua hii ina lengo la kuwalinda wachangiaji kwa kuwianisha huduma na uhalisia wa gharama wanazotozwa.

***191*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilianza kutoa huduma kwa wanachama wenye ulemavu zinazojumuisha *fimbo nyeupe* kwa wasioona, *shimesikio* kwa viziwi na *magongo* ya kutembelea kwa watu wenye ulemavu wa maungo. Huduma hizi zilizinduliwa rasmi tarehe 30 Juni, 2008 na utoaji wake kwa sasa unafanyika kupitia Kasma ya Misaada na shughuli za kijamii za Mfuko. Hatua hii hata hivyo ni ya muda wakati taarifa ya tathmini ya uhai wa Mfuko inayoendelea kufanyiwa kazi na Shirika la Kazi Duniani ikisubiriwa. Taarifa hii itawezesha kuingiza huduma hizi kwa

makundi haya kwenye Kanuni za Mfuko baada ya kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi wa Mfuko.

***192*** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Juni, 2009 Mfuko ulishatoa jumla ya mikopo 45 ya vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi 968,481,920 kwa watoa huduma wa mikoa 14 ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Mwanza, Rukwa, Dodoma, Mtwara, Mbeya, Kagera, Lindi, Kilimanjaro, Singida, Mara na Tabora. Vifaa vilivyokopeshwa vimechangia katika kuboresha huduma ya vipimo na kuwapunguzia wanachama umbali wa kuzifuata huduma hizo hasa maeneo ya vijijini. Aidha, jumla ya shilingi 428,096,010 zilitolewa kama mikopo nafuu kwa ajili ya kukarabati sehemu za kutolea huduma kwa wanachama wa Mfuko katika vituo tisa vya matibabu katika mikoa ya Mara, Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Lindi, Kagera, Mbeya na Ruvuma.

***193*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2008/09, maandalizi ya kujenga kituo cha matibabu cha Mfano "*Centre of Execellence*" cha Dodoma yaliendelea ikiwa ni pamoja na kumpata Mkandarasi mwenye sifa wa kujenga kituo hicho. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma iliainisha mahitaji yote muhimu ya ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Uchunguzi wa Magonjwa "*Diagnostic Centre*". Makisio ya gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 17, na unakadiriwa kuchukua miezi 30 baada ya kuidhinishwa. Maombi rasmi kwa ajili ya kupata dhamana ya Serikali yalikwisha fanywa ili utekelezaji wake uanze.

## MIPANGO, MAJUKUMU, MALENGO NA MAOMBI YA FEDHA YA BAJETI KWA MWAKA 2009/10

## MATUMIZI YA KAWAIDA

**194** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2009/10, Wizara inaomba kiasi cha shilingi **218,393,211,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya hizo shilingi **104,831,750,600.00** zinaombwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Taasisi zilizo chini yake. Kiasi cha shilingi **113,561,460,400.00** kinaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha hii itatumika kutekeleza kazi zifuatazo:

## UTAWALA NA UTUMISHI

**195** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kutoa ajira kwa watumishi wa kada mbalimbali za afya na ustawi wa jamii wa ndani na nje ya nchi. Wizara itaajiri wataalam 234 na kuwapangia vituo vya kazi na kuwapandisha vyeo watumishi 731. Aidha, Wizara itawapangia wataalamu wapatao 6,000 vituo vya kazi katika mamlaka mbalimbali za ajira.

## USIMAMIZI WA FEDHA ZINAZOELEKEZWA KATIKA SEKTA YA AFYA

**196** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi itaanza utekelezaji wa utaratibu wa kulipa baadhi ya malipo kwa kupitia Mfumo wa Malipo kwa Mtandao (*e-Payment System*) badala ya malipo kwa hundi. Utekelezaji huo utaanza baada

ya kukamilika kwa uunganishaji wa mitandao ya malipo kati ya Benki Kuu na Wizara ya Fedha na Uchumi. Utaratibu huu utapunguza ucheleweshaji wa malipo na kupunguza gharama kwa Serikali.

**197** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaweka mfumo utakaomwezesha Afisa Mhasibu kufuatilia mwenendo wa akaunti zote na kutoa taarifa kwa Wizara ya Fedha na Uchumi na wadau wa maendeleo kwa urahisi zaidi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wanaohusika na akaunti za miradi misonge itaainisha akaunti zinazotakiwa kufungwa.

## UNUNUZI NA UGAVI

**198** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea na utaratibu wa kutumia Bodi za Zabuni za Halmashauri na Mikoa kusimamia taratibu za kufanya ununuzi ikiwa ni pamoja na kuwapata wakandarasi wa kazi za ukarabati na ujenzi katika vituo vya huduma za afya na ustawi wa jamii. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi itakamilisha daftari la mali za Serikali ili kuonesha idadi na thamani ya mali. Vilevile, Wizara itashirikiana na Wadau wa Maendeleo wa Mfuko wa pamoja katika kuboresha huduma zitolewazo na Kitengo cha Ununuzi kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi wafanyakazi na Wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya Wizara.

## UKAGUZI WA NDANI

**199** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo

ya udhibiti na usimamizi wa fedha, ununuzi na usalama wa mali za Serikali kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali iliyopo. Aidha, Wizara itaendelea kufuatilia usambazaji na matumizi ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyotolewa na Bohari ya Dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii.

**MAWASILIANO**

***200*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kuielimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii ikiwa ni pamoja na kutoa ufafanuzi wa matukio mbalimbali yanayohusu huduma za afya na ustawi wa jamii. Wizara itaimarisha ushirikiano na vyombo vya habari ili kuiwezesha jamii kupata na kuelewa taarifa mbalimbali zinazohusu huduma za afya na ustawi wa jamii.

**KITENGO CHA SHERIA**

**Sheria za Kusimamia Utoaji wa Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii**

***201*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itapitia sheria mbalimbali zinazosimamia huduma za afya na ustawi wa jamii nchini kwa lengo la kuziboresha. Sheria hizo zinajumuisha; sheria zinazosimamia huduma zitolewazo na Sekta Binafsi, sheria zinazosimamia taaluma za afya na sheria iliyoanzisha Taasisi ya Chakula na Lishe. Aidha, Wizara itakamilisha mapendekezo ya sheria ya huduma za afya nchini "*National Health Services Act*" ili muswada husika uweze kuwasilishwa Bungeni katika mwaka huu wa fedha. Vilevile,

Wizara itakamilisha kanuni za Sheria mbalimbali za sekta ya afya zilizopitishwa mwaka 2007/08 na mwaka 2008/09 zitaandaliwa.

***202 Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya kurekebisha Sheria itaandaa mapendekezo ya Sheria ya kuunganisha Mabaraza yote ya Taaluma yaliyo chini ya Wizara. Aidha, Wizara itandaa Mpango wa Utekelezaji wa Sheria za Afya "*Health Legislation Implementation Support Plan*". Mpango huu utaainisha mkakati wa utekelezaji wa Sheria mbalimbali za afya na ustawi wa jamii.

**OFISI YA MGANGA MKUU WA SERIKALI**

***203 Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali itaratibu na kusimamia huduma za Kinga, Tiba, Mafunzo na Utengamao katika Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii. Aidha, Ofisi itasimamia maadili na ubora wa viwango vya huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyoandaliwa na Wizara. Vilevile, Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali itasimamia na kuimarisha huduma za uuguzi na ukunga, ukaguzi na ubora wa huduma za afya, dharura na maafa na mabaraza ya kitaaluma.

**Uuguzi na Ukunga**

***204 Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itafuatilia utekelezaji wa Mwongozo wa Uuguzi wa kutoa huduma za msingi kwa wagonjwa na Mwongozo wa Viwango vya Ubora wa huduma za uuguzi zinazotolewa kwa jamii katika hospitali za Mikoa na Rufaa. Aidha, Wizara itachapisha nakala

7,000 za miongozo hiyo na kuisambaza kwa wadau nchi nzima. Vilevile, Wizara itaandaa Mpango Mkakati wa uuguzi wa miaka mitatu 2009-2012, ambao utakuwa ndiyo dira ya utekelezaji wa kazi za uuguzi na hivyo kusaidia uboreshaji wa huduma za uuguzi kwa ujumla.

**Ukaguzi wa Ubora wa Huduma za Afya**

***205*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itafanya ukaguzi wa ubora wa huduma katika hospitali 27, zikiwemo hospitali za ubingwa maalum tano, ubingwa maalum ngazi ya kanda tatu na hospitali za rufaa za mikoa 19. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa watumishi 1,500 wa hospitali hizo 27 yanayohusu kukinga na kudhibiti maambukizi katika utoaji wa huduma za afya na utoaji wa sindano salama. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa wakufunzi 50 wa vyuo vya mafunzo vya afya kutoka kanda zote nane za mafunzo nchini. Mafunzo hayo yanahusu kukinga na kudhibiti maambukizi katika utoaji wa huduma za afya, utoaji wa sindano salama, uboreshaji wa huduma za afya, usimamizi shirikishi na ukaguzi wa huduma za afya.

**Dharura na Maafa**

***206*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kutoa huduma za dharura nchini dhidi ya majanga mbalimbali yanayojumuisha mafuriko, ajali za viwandani pamoja na vyombo vya usafiri, tetemeko la ardhi, njaa na magonjwa ya milipuko ukiwemo ugonjwa wa Mafua Makali ya Nguruwe "*Swine Flu*". Aidha, Wizara itatoa mafunzo maalum kwa Timu za Dharura za Mikoa minane ya Morogoro, Dodoma, Iringa, Mbeya,

Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Pwani; mikoa hii ina matukio mengi ya dharura na ajali.

**Mabaraza ya Kitaaluma**

***207*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itakagua hospitali za mikoa kwa nia ya kuongeza vituo vya mafunzo kwa vitendo kwa Madaktari na Wafamasia. Aidha, Wizara itaboresha taarifa za usajili wa madaktari na famasia kwa lengo la kuwa na kumbukumbu sahihi juu ya idadi, viwango vyao vya elimu na ujuzi.

***208*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaandaa Mwongozo wa Mafunzo kwa vitendo kwa madaktari wanaomaliza mafunzo ili kuboresha mafunzo hayo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu na Baraza la Ithibati itavikagua vyuo, vyuo vikuu na vituo vya mafunzo kwa vitendo vinavyotoa mafunzo ya Udaktari ili kuhakiki ubora wa elimu itolewayo.

***209*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Maadili, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma itatoa mafunzo ya maadili kwa Wauguzi na wanafunzi wa uuguzi nchi nzima na zoezi hilo litakuwa endelevu.

***210*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mionzi nchini, itafanya ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma ya radiolojia kwa lengo la kuboresha huduma hizo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Maabara Binafsi za Afya itaendelea kukagua vituo vya kutolea huduma za maabara nchini.

211 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaanza kusajili Waganga, Wakunga, Wauza dawa, Dawa za tiba asili na Vituo vya Tiba Asili na Tiba Mbadala. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na vyombo vya habari katika kuelimisha jamii kuhusu sheria, kanuni za tiba asili na tiba mbadala na taratibu za usajili.

**HUDUMA ZA KINGA**

**Udhibiti wa Magonjwa**

212 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itatoa elimu juu ya magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza ikiwa ni pamoja na kuelimisha jamii juu ya kujikinga na magonjwa mapya yanayojitokeza kama vile Ebola, Marburg, Homa ya Bonde la Ufa na Homa ya Mafua Makali ya Nguruwe. Aidha, Wizara itatoa chanjo za kuzuia magonjwa ya Homa ya Uti wa Mgongo na ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa katika mikoa na wilaya ili kukabiliana na magonjwa hayo. Vilevile, Wizara itatoa dawa, vifaa na vifaa tiba ili kukabiliana na magonjwa ya milipuko nchini ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa Kipindupindu, Homa ya Matumbo na magonjwa ya Kuhara.

213 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Wadau itafanya ufuatiliaji wa ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege katika maeneo maalumu yaliyoko katika mikoa ya Kigoma (Kibondo), Dar es Salaam (Mwananyamala), Manyara (Mbulu – Hospitali ya Dini ya Hydom), na hospitali za mikoa ya Mwanza (Sekou Toure)

na Dodoma. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Wadau, itaendesha mradi wa kudhibiti ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa na kwa kuanzia Mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Mtwara na Ruvuma itahusishwa. Vilevile, Wizara itafanya utafiti nchini kuhusu vigezo hatarishi katika jamii juu ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambao matokeo yake yataimarisha utoaji wa elimu ya afya kwa umma yanayolenga katika kubadilisha tabia hatarishi.

**Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria**

***214*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaboresha huduma za kinga na tiba ya Malaria nchini. Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa Waganga, Wauguzi, Fundi Sanifu Maabara na Wafamasia kuhusu uchunguzi na tiba sahihi ya Malaria. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau itahamasisha wananchi kuwahi kupata tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya wanapohisi au kuona dalili za ugonjwa wa Malaria.

***215*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kugawa vyandarua bila malipo kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano. Aidha, Wizara itagawa bila malipo jumla ya vyandarua milioni 14.6 ambapo kila Kaya itapata wastani wa vyandarua viwili ili kuhakikisha kuwa kila Kaya inatumia chandarua.

***216*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendeleza matumizi ya dawa ya ukoko aina ya ICON ndani ya

nyumba baada ya kuonesha mafanikio makubwa katika wilaya za Muleba na Karagwe mkoani Kagera ilikofanyiwa majaribio. Wilaya zote za mikoa ya Mwanza na Mara pamoja na zilizobaki katika mkoa wa Kagera zitahusishwa. Wilaya hizi zina milipuko mikubwa ya Malaria. Aidha, Wizara itapuliza dawa ya ukoko aina ya DDT ndani ya nyumba katika wilaya ya Mkuranga kwa majaribio kabla ya kuanza kuitumia maeneo mengine nchini.

**Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma**

***217*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa dawa sahihi na za kutosha za ugonjwa wa Kifua Kikuu, ikiwemo Kifua Kikuu sugu, zinapatikana na kusambazwa nchi nzima. Aidha, Wizara itahakikisha dawa zinapatikana kwa wakati muafaka na wagonjwa wanatibiwa bila malipo na bila usumbufu. Vilevile, Wizara itapanua wigo wa huduma za wagonjwa wa Kifua Kikuu kwa kuvihusisha vituo vingi zaidi hususan vya Sekta Binafsi. Wizara pia, itaimarisha huduma za maabara ili kubaini wagonjwa wenye Kifua Kikuu sugu kwa haraka zaidi na kuimarisha uwezo wa kufuatilia kwa karibu mwenendo wa Kifua Kikuu sugu nchini.

***218*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaboresha huduma shirikishi za Kifua Kikuu na UKIMWI kwa kuweka mkazo katika kuchunguza Kifua Kikuu kwa wagonjwa wa UKIMWI. Aidha, Wizara itawapatia matibabu sahihi pale itakapobainika wana ugonjwa wa Kifua Kikuu. Vilevile, Wizara itatoa Mwongozo mpya wa kudhibiti maambukizi ya pamoja ya Kifua Kikuu na UKIMWI katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

219 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kutoa dawa za kutibu Ukoma nchini kote na viatu maalum kwa walioathirika na ugonjwa huu bila malipo. Aidha, Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali kukamilisha kampeni ya kupambana na Ukoma katika Wilaya za Kilombero, Morogoro Vijijini na Kilosa.

**Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI**

220 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wadau wengine itasambaza huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa watumiaji wote wa huduma za afya "*Provider Initiated Counselling and Testing*" katika hospitali zote na vituo vyote vya afya nchini. Huduma hizi zitatolewa na mtumishi wa afya kwa kila mgonjwa/mteja atakayefika kupata huduma katika kituo. Aidha, Wizara itaimarisha na kuboresha vituo vya ushauri nasaha vilivyopo 1,732 na kuongeza vingine 268 hasa katika maeneo ya vijijini.

**Mpango wa Taifa wa Huduma za Macho na Udhibiti wa Ugonjwa wa Usubi**

221 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itafuatilia utekelezaji wa Mipango ya Dira 2020 ya kutokomeza upofu unaozuilika katika mikoa ya Tanga, Morogoro, na Pwani.

**Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto**

222 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itasimamia na kufuatilia utekelezaji wa huduma zilizomo katika mpango maalum wa kuboresha huduma za afya ya uzazi na mtoto.

Huduma hizi ni pamoja na Uzazi wa Mpango, Uzazi salama, Kumudu magonjwa ya uwiano ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, Afya shuleni, Chanjo, Afya ya jamii na Afya ya uzazi kwa vijana. Aidha, Wizara itaongeza kasi ya kupunguza vifo vya watoto wachanga, watoto wenye umri chini ya miaka mitano na vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi.

***223*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itashirikiana na vituo vya mafunzo vya kanda na mashirika ya kimataifa yanayosaidia kutoa huduma za uzazi wa mpango, katika kuendesha mafunzo ya uzazi wa mpango kwa njia za muda mfupi, muda mrefu na za kudumu. Mafunzo haya yatatolewa kwa wakufunzi, watoa huduma na wasimamizi wa ngazi zote nchini, ikiwa ni pamoja na wale wa vituo vya Serikali, vya mashirika ya kujitolea na binafsi. Aidha, uhamasishaji na uraghibishi kuhusu uzazi wa mpango utafanyika katika ngazi zote. Vilevile, Wizara itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kuwa huduma za uzazi wa mpango zinatolewa katika viwango vinavyostahili na bila malipo. Wizara pia, itaendelea kupanua huduma ya kutambua Saratani ya shingo ya kizazi ikiwa ni sehemu muhimu ya huduma za afya ya uzazi na mtoto.

***224*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itatoa mafunzo mbalimbali ya stadi za kuokoa maisha na huduma ya dharura kwa wenye matatizo yatokanayo na uzazi, huduma kwa mama wakati wa ujauzito, baada ya kujifungua na katika siku arobaini za uzazi. Mafunzo na huduma

hizo zitatolewa katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Kigoma, Ruvuma, Iringa, Mara, Mtwara, Lindi, Tabora na Arusha. Aidha, Wizara itanunua pikipiki maalumu 370 kwa ajili ya vituo vya afya ili kuboresha rufaa ya dharura kwa wanawake wajawazito na watoto.

**Udhibiti wa Magonjwa ya Watoto kwa Uwiano**

***225*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika 2009/10, Wizara itatekeleza mkakati wa udhibiti wa magonjwa ya watoto kwa uwiano ili kupunguza vifo vya watoto pamoja na watoto wachanga kwa kusambaza dawa ya zinki kwa ajili ya magonjwa ya kuharisha kwa mikoa yote nchini. Mafunzo ya kuboresha huduma kwa watoto na mafunzo ya huduma ya dharura ngazi ya hospitali yatatolewa kwa watoa huduma 168 kutoka mikoa ya Mara, Shinyanga, Singida, Kilimanjaro, Manyara, Ruvuma na Rukwa. Mafunzo ya huduma kwa watoto wachanga na huduma kwa watoto wenye uzito pungufu ikiwemo kumkumbatia mtoto kifuani "*Kangaroo Mother Care*" yatatolewa kwa walimu wa walimu 40 kutoka mikoa ya Lindi, Morogoro na Pwani kwa kuanzia.

**Mpango wa Taifa wa Chanjo**

***226*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaimarisha huduma za chanjo kwa kutoa chanjo kwenye kliniki za Afya ya Uzazi na Mtoto na kupitia huduma za mkoba na kliniki tembezi "*mobile clinics*". Aidha, katika kutekeleza lengo la kumfikia kila mtoto anayestahili kupata chanjo katika kila wilaya, Wizara itatekeleza mpango maalum wa "R*each Every Child"* kwa wilaya 23 ambazo zimeonekana kuwa na kiwango cha chini cha chanjo ili kuinua kiwango cha utoaji chanjo kwenye wilaya

hizo. Vilevile, Wizara itaendeleza awamu ya tatu ya utoaji chanjo ya pepopunda kwa wanawake wenye umri wa kuzaa katika Halmashauri 14 za Bariadi, Bunda, Bukombe, Hanang, Kahama, Kibondo, Kiteto, Meatu, Mpanda Vijijini, Mpanda Mjini, Ngara, Rorya, Simanjiro na Tarime. Wizara pia, itaanzisha utoaji wa chanjo mpya ya kuwakinga watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja dhidi ya ugonjwa wa kichomi utokanao na vimelea aina ya "*streptococcal pneumonia*". Pia itatoa chanjo mpya ya "*Haemophilus Influenza type B - HIB*" kwa watoto wapatao 1,723,240.

**Afya Shuleni**

***227*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itahamasisha watendaji na wadau mbalimbali kutoka katika mikoa minne ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Dodoma kuhusu uboreshaji wa huduma za afya shuleni. Huduma hizi zinajumuisha utoaji wa chakula cha mchana, uchunguzi wa afya za wanafunzi, upatikanaji wa huduma ya kwanza na matatizo ya mimba kwa wasichana shuleni.

**AFYA YA MAZINGIRA**

**Usafi wa Mazingira**

***228*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itachapisha Sheria ya Afya ya Jamii na kuisambaza katika mikoa na wilaya zote na kuandaa kanuni kwa ajili ya utekelezaji wake. Aidha, Wizara itaunda Baraza la usajili wa wataalamu wa afya ya mazingira ili kusimamia utekelezaji wa sheria hii. Vilevile, Wizara itaanzisha mashindano ya usafi shuleni katika masuala ya afya na usafi wa mazingira ili kuinua kiwango cha usafi shuleni.

**Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira**

***229*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10**,** Wizara itatoa mafunzo ya udhibiti taka zinazotokana na huduma za afya kwa watumishi wa afya katika ngazi za mikoa na wilaya. Aidha, Wizara itachapisha na kusambaza Mwongozo wa kudhibiti taka katika Halmashauri zote nchini. Vilevile, Wizara itafanya tathmini ili kupata hali halisi ya athari za afya zitokanazo na uchafuzi wa mazingira katika mikoa mitano ya Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Tanga na Shinyanga. Mikoa hiyo ina idadi kubwa ya viwanda, mashamba makubwa, shughuli za uvuvi na uchimbaji wa madini. Wizara pia, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo itachunguza na kuandaa mikakati dhidi ya matatizo ya kiafya yatokanayo na uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

**Afya Bandarini na Mipakani**

***230*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itakamilisha mchakato wa utekelezaji wa kanuni za afya za kimataifa *"International Health Regulations"* ambazo ni nyenzo muhimu katika kupambana na magonjwa mbalimbali kwa mfano Mafua makali ya Ndege na Mafua makali ya Nguruwe yanayoenea kimataifa. Aidha, Wizara itaimarisha ufuatiliaji wa magonjwa mipakani kwa kutoa vitendea kazi na mafunzo yatakayowaongezea uwezo watendaji katika vituo vya afya vilivyopo mipakani.

**Usalama wa Vyakula**

***231*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itakamilisha Sera ya Chakula Salama na kusambaza kwa wadau ili watoe maoni yao.

**Elimu ya Afya kwa Umma**

**232** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itakamilisha Mwongozo wa Promosheni na Elimu ya Afya, itaandaa Mpango Mkakati wa Promosheni na Elimu ya Afya wa mwaka 2009 - 2015 na Mpango Mkakati wa Udhibiti wa Matumizi ya Bidhaa za Tumbaku wa mwaka 2009 - 2015. Aidha, Wizara itaelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kubadili tabia na mienendo hatarishi kwa afya ili kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Vilevile, Wizara itashirikisha wadau na jamii katika kuelimisha wananchi kuhusu maradhi ya milipuko, majanga na matukio mengine ya dharura ambayo yanazidi kujitokeza katika jamii yetu na kusababisha majeruhi, upotevu wa maisha na mali.

**HUDUMA ZA TIBA**

**Vituo vya Kutolea Huduma za Afya**

**233** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za tiba zinajumuisha mfumo mzima wa utoaji matibabu, uchunguzi na rufaa kuanzia ngazi ya kaya, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya hadi hospitali za rufaa za mikoa na hospitali maalum "*super speciality*" katika Sekta za Umma na Binafsi. Katika ngazi ya Kaya, huduma zinatolewa na Serikali na Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kwa mfumo wa mkoba "*outreach/home based care*". Huduma za afya ya msingi zinatolewa na zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya. Huduma za rufaa zinatolewa na Hospitali za Mikoa.

**234** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inajenga na kupanua Hospitali za Mikoa kwa kuongeza vifaa na

wataalam ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake ya rufaa katika mikoa. Hospitali zinazojengwa mpya ni pamoja na za Mikoa ya Pwani na Manyara. Hospitali za Mikoa ya Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga zinapanuliwa ambapo majengo na maabara mpya zinajengwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

***235*** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za ubingwa maalum zinatolewa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Taasisi ya Mirembe na Isanga na Hospitali ya Kibong'oto. Hospitali nyingine za ubingwa maalum ngazi ya kanda ni pamoja na Hospitali ya Rufaa Mbeya, Bugando Medical Centre na Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC). Aidha, Serikali itaendelea kujenga Hospitali za Kanda ya Kusini, Mtwara na Kanda ya Kati, Dodoma. Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kati, Dodoma unatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Huduma za ubingwa maalum zitapunguza rufaa ya matibabu ya wagonjwa nje ya nchi. Maeneo maalum yanayotiliwa mkazo ni Upasuaji wa moyo, Usafishaji figo, Upasuaji wa ubongo, Mgongo na Viungo, Tiba ya saratani na Wagonjwa wa akili.

**Huduma za Afya ya Kinywa**

***236*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itanunua dawa na vifaa tiba ya meno kwa ajili ya vituo vya kutolea tiba vya mikoa na wilaya zote nchini na kufunga mitambo ya kutibia meno

katika vituo 37. Aidha, itaboresha vifaa vya tiba ya meno katika hospitali za rufaa za mikoa ya Ruvuma na Dodoma. Vilevile, itanunua mashine za x-ray kwa ajili ya hospitali za rufaa za mikoa ya Mwanza - Sekou Toure, Tanga - Bombo na Kilimanjaro - Mawenzi.

### Hospitali za Rufaa na Hospitali Maalumu

### Hospitali Maalumu "*Super speciality hospitals*"

### Hospitali ya Taifa Muhimbili

**237** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Hospitali itaboresha uchunguzi wa magonjwa na tiba kwa wagonjwa waliopata rufaa nchini. Hospitali itaongeza idadi ya wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji wa moyo toka wagonjwa 100 mpaka 156 kwa mwaka. Hospitali itaanza ujenzi wa kituo cha tiba ya magonjwa ya moyo pamoja na mafunzo. Kituo hicho kitajengwa kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya watu wa China. Aidha, hospitali itaanza kutoa huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo na kutoa mafunzo zaidi kwa wataalam wanaotoa huduma hiyo.

**238** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Hospitali itaanza kutoa huduma za dharura "*Emergency Medicine*" na upasuaji kwa kupitia tundu dogo sana "*Laparascopic surgery*" kufikia sehemu yenye ugonjwa. Huduma hii itapunguza muda ambao mgonjwa anatakiwa kukaa hospitalini. Aidha, Hospitali itaanzisha huduma ya mkoba kwa wagonjwa wa macho kwa kutumia gari maalum. Vilevile, Hospitali itaanzisha huduma ya mazoezi ya viungo kwa watoto.

**Hospitali ya Bugando**

***239*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Hospitali itaboresha huduma za wagonjwa na mafunzo kwa watumishi. Aidha, Hospitali itaendelea na ujenzi wa jengo la huduma kwa wagonjwa wa Saratani na kwa kushirikiana na wadau itajenga Kituo cha Mfano cha Huduma kwa Watoto wenye UKIMWI na kituo cha kuhudumia watu wazima wenye UKIMWI. Vilevile, Hospitali kwa kushirikiana na wadau itakarabati maabara na itaanzisha huduma za upasuaji wa moyo.

**Hospitali ya KCMC**

***240*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Hospitali itaendelea kuboresha huduma za kibingwa za uchunguzi na matibabu, utafiti na kutoa elimu kwa wanafunzi wa kada mbalimbali wanaotumia hospitali kwa mafunzo ya vitendo. Aidha, Hospitali itaendeleza azma yake ya kutoa huduma za upasuaji mkubwa wa moyo, ili kuchangia katika juhudi za Serikali za kupunguza wagonjwa wanaolazimika kupelekwa nje ya nchi kwa matibabu ya moyo. Vilevile, Hospitali itakamilisha ujenzi wa wodi mbili zitakazokuwa na vitanda 42 kwa ajili ya wagonjwa wenye matatizo ya ngozi, na pia itakamilisha ujenzi wa kitengo cha kuhudumia wagonjwa waliopata madhara ya kuungua na moto. Hospitali pia, itaanza ujenzi wa wodi ya upasuaji wa mifupa na viungo pamoja na kitengo cha tiba rekebishi.

**Hospitali ya Rufaa Mbeya**

***241*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2009/10, Hospitali itatoa huduma za uchunguzi na tiba kwa wagonjwa waliopata rufaa kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, pamoja na kutoa

mafunzo kwa watumishi. Hospitali itanunua vifaa kwa ajili ya Maabara ya rufaa kwa VVU/UKIMWI. Aidha, Hospitali itashiriki katika kuhamasisha na kufanya tohara kwa wanaume ili kupunguza maambukizi ya VVU na itanunua mashine mpya za kufulia nguo za wagonjwa.

**Taasisi ya Mifupa Muhimbili - MOI**

**242** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Taasisi itaboresha huduma za wagonjwa na mafunzo kwa watumishi. Aidha, kwa kushirikiana na Vyuo na Taasisi mbalimbali za Marekani, itaboresha upasuaji wa ubongo na uti wa mgongo. Taasisi itatoa mafunzo kwa wataalamu wa fani hii nchini na nchi za jirani. Vilevile, Taasisi itaimarisha huduma za upasuaji wa majeruhi na upasuaji wa kuweka viungo bandia vya nyonga na goti ili wagonjwa wengi zaidi wapate huduma hii. Pia, Taasisi itapeleka wataalamu masomoni ili wapate utaalam zaidi unaotakiwa kuboresha huduma za upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu.

**Taasisi ya Saratani Ocean Road**

***243*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Taasisi itaendelea kutoa huduma za kinga, uchunguzi na matibabu ya Saratani. Aidha, Taasisi itatoa mafunzo kwa wataalamu wa afya 140 kutoka katika hospitali za mikoa na wilaya ili kuhakikisha elimu ya kinga na huduma za uchunguzi wa Saratani zinawafikia wananchi wengi zaidi nchini. Mafunzo hayo yatatolewa katika mikoa ya Singida, Rukwa, Kagera, Mara na Tabora. Lengo ni kutoa mafunzo haya kwa mikoa yote. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Taasisi itaboresha huduma za tiba shufaa katika hospitali za rufaa na nyingine

ambazo zinatoa huduma hii. Taasisi pia, itaendelea kutoa mafunzo ya wataalamu wa afya kuhusu tiba shufaa.

***244*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Taasisi itaendelea kuimarisha matibabu ya Saratani za watoto hususan "*Burkitt's lymphoma*". Aidha, Taasisi kwa uhisani wa Serikali ya India itazindua kituo cha matibabu kwa njia ya mawasiliano ya mtandao "*telemedicine*". Kituo hicho kitasaidia Taasisi kupata msaada wa kitalamu moja kwa moja kutoka kwa wataalamu wa ndani na nje. Vilevile, Taasisi itaanza ujenzi wa jengo jipya litakalokuwa na nafasi kubwa ya wodi, vyumba vya madaktari, vyumba vya matibabu ya mionzi na dawa na vyumba vya upasuaji. Taasisi pia, itaandaa mkutano wa saba wa kimataifa wa "*African Organisation for Research and Training in Cancer - AORTIC*" ambao kauli mbiu yake ni **Udhibiti wa Saratani Barani Afrika – Inawezekana.** Taasisi na Kamati Teule ya Waziri itakamilisha na kuwasilisha Wizarani Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Saratani.

**Hospitali ya Mirembe na Taasisi ya Isanga.**

**Hospitali ya Mirembe**

***245*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Hospitali itaendelea kutoa huduma za uchunguzi, matibabu kwa wagonjwa wa akili na walioathirika na dawa za kulevya. Aidha, itatoa elimu shuleni na vyuo vya elimu ya juu kuhusu athari na jinsi ya kupambana na dawa za kulevya. Hospitali itaimarisha udhibiti wa maambukizi ya VVU miongoni mwa watumishi wa hospitali. Vilevile, Hospitali itaimarisha matumizi ya vitofali

vya mkaa wa mawe na gesi asilia badala ya kuni ili kuhifadhi mazingira. Hospitali pia, itaendelea na ujenzi wa awamu ya tatu ya Kituo cha Matibabu ya waathirika wa dawa za kulevya kilichopo Itega.

**Taasisi ya Isanga**

***246*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Taasisi itaendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba kwa wagonjwa wa akili waliofanya makosa ya jinai. Aidha, Taasisi itaimarisha udhibiti wa maambukizi ya VVU miongoni mwa watumishi wake. Vilevile, itaboresha mfumo wa matengenezo kinga ya vifaa na miundombinu ya Taasisi na nyumba za watumishi.

**Hospitali ya Kibong'oto**

***247*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Hospitali itaendelea kutoa huduma za tiba na uchunguzi kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu na Kifua Kikuu sugu pamoja na wagonjwa walioathirika na VVU. Aidha, Hospitali itatoa mafunzo kwa watumishi wa ngazi mbalimbali kuhusu tiba ya Kifua Kikuu. Hospitali itaendeleza ujenzi wa uzio awamu ya nne, stoo, ukarabati wa jengo la utawala, mfumo wa maji pamoja na kuweka mfumo wa umeme.

**Uchunguzi wa Magonjwa**

***248*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaimarisha na kusimamia huduma za uchunguzi wa magonjwa za maabara na radiolojia ili huduma hizo ziweze kukidhi ubora wa viwango vinavyokubalika. Aidha, Wizara itaimarisha karakana za ufundi wa vifaa tiba za kanda katika

hospitali ya Taifa Muhimbili, hospitali ya Bugando, KCMC, hospitali ya Rufaa Mbeya, hospitali ya Mtwara na Tabora. Vilevile, Wizara itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi na wadau wengine kuimarisha karakana za ufundi wa vifaa tiba katika mikoa ya Tanga, Mtwara, Mbeya na Kagera ili ziweze kutoa huduma hiyo katika maeneo yao husika.

***249*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau itakamilisha ujenzi wa maabara za mikoa ya Pwani, Morogoro, Singida na Manispaa ya Temeke. Maabara za mikoa ya Lindi, Mtwara, Rukwa, Kigoma, Shinyanga na Mwananyamala katika Manispaa ya Kinondoni zitafanyiwa ukarabati. Aidha, Wizara itaingia mkataba na Serikali ya Uholanzi wa kuzipatia "*x-ray*" na "*ultrasound*" hospitali za wilaya mpya na kuziboresha hospitali za rufaa za mikoa na maalum kwa kuzipatia vifaa vya kitaalam na mawasiliano ya "*internet*". Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na wadau wengine, itaboresha vituo vya afya vitatu, kimoja kwa kila Manispaa ili viweze kutoa huduma ya uchunguzi yenye ubora unaotakiwa sawa na ngazi ya hospitali ya wilaya.

**Mpango wa Damu Salama**

***250*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, awamu ya kwanza ya ujenzi wa kituo cha Damu Salama Kanda ya Kati - Dodoma, kwa msaada wa Serikali ya Norway utaanza kwa kutumia fedha ambazo tayari zimepatikana.

**Huduma za Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**

***251*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara imetenga shilingi **130,262,702,200.00** kwa ajili ya kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma. Kati ya fedha hizo, Serikali imetenga shilingi **36,308,058,400.00,** Wadau wa Mfuko wa Pamoja shilingi **14,898,692,000.00** na ***Global Fund*** **shilingi 79,055,951,800.00**

***252*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itanunua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika zahanati 3,754, vituo vya afya 413, hospitali za wilaya na Teule 134, Mikoa 20, Manispaa tatu, Rufaa nne, Maalum nne, Jeshi la Wananchi mbili na Polisi moja. Zahanati 388 na vituo vya afya 62 ni vipya vilivyojengwa na Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi pamoja na TASAF.

***253*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itatoa mafunzo kwa watumishi wa zahanati, vituo vya afya, Hospitali za Serikali, za Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, na Mashirika ya Dini katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Shinyanga na Mtwara. Mafunzo hayo yatahusu matumizi ya mfumo wa uagizaji dawa na vifaa tiba kulingana na mahitaji na mgawo wa fedha na utunzaji wa kumbukumbu "*Integrated Logistic System – ILS*". Baada ya mafunzo hayo, zahanati, vituo vya afya na Hospitali zote za umma nchini zitatumia mfumo huo katika kuagiza mahitaji yake kutoka Bohari ya Dawa.

**Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza, Afya ya Akili, na Dawa za Kulevya**

***254*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itakamilisha mpango wa utekelezaji wa miaka mitano wa Magonjwa yasiyoambukiza, Afya ya Akili na Dawa za Kulevya. Mpango huu utabainisha vipaumbele katika huduma na mahitaji ya rasilimali watu na fedha. Aidha, Wizara itakamilisha mwongozo wa kisera kuhusu pombe katika jamii. Vilevile, Wizara itakamilisha kanuni za utekelezaji wa sheria mpya ya afya ya akili.

**Huduma za Hospitali za Mashirika ya Kujitolea, Makampuni na Watu Binafsi**

***255*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kuhamasisha wamiliki wa vituo vya huduma za afya vya Mashirika ya kujitolea waingie makubaliano na Halmashauri ili vituo vyao vitoe huduma kwa niaba ya Halmashauri hizo. Hospitali nne zinategemewa kuingia Makubaliano na Halmashauri husika ili zitumike kama Hospitali Teule. Hospitali hizo ni; St. Elizabeth (Manispaa ya Arusha), Kolandoto (Manispaa ya Shinyanga), Machame (Wilaya ya Siha) na Shirati (Wilaya ya Rorya).

**Huduma ya Matibabu Nje ya Nchi**

***256*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo hospitali za rufaa ili ziweze kutoa huduma zinazopatikana nje ya nchi. Aidha, Madaktari Bingwa kutoka India wataanza kuja kutoa huduma kwa wagonjwa hapa hapa nchini katika utekelezaji wa makubaliano yaliyokwishafanyika. Kwa kuanzia wataalam hao watakuja kuangalia vifaa vilivyopo na kujadili na

wataalamu wetu kuhusu wagonjwa wa kutibiwa hapa nchini na wale wa kupelekwa India. Hali hii itapunguza gharama za matibabu na hivyo kufanya wagonjwa wengi zaidi kutibiwa. Mpango huu unahusu hospitali za Apollo nne katika miji minne ya New Delhi, Hyderabadi, Chennai na Ahmedabad na moja chini ya Taasisi ya Madras Medical Mission katika mji wa Chennai. Utekelezaji wa Mpango huu utashirikisha Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili – "*MOI*" na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road. Hospitali hizo za India, zitapokea makundi ya mchanganyiko wa wataalam kutoka nchini watakaokwenda kupata ujuzi zaidi na watashiriki katika kuwahudumia wagonjwa wanaopelekwa huko kwa matibabu. Hata hivyo, ili huduma kwa Watanzania iwe endelevu, Serikali kwa kuutumia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii – "*NSSF*" imeingia makubaliano ya kujenga hospitali ya kisasa yenye huduma za ubingwa kwenye eneo la Chuo Kikuu ukanda wa Mlimani City wakati wo wote kuanzia sasa.

**Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala**

***257*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kusimamia na kuendeleza Tiba asili na Tiba mbadala nchini, ili kuboresha afya ya jamii nchini Tanzania. Aidha, Wizara itaandaa kitabu cha mafunzo kwa ajili ya Waganga wa Tiba Asili na Tiba mbadala na mpango wa kuwashirikisha Matabibu wa tiba asili waliosajiliwa katika mpango na Kamati za Afya ya Msingi ngazi ya Kijiji na Mtaa ili waweze kutoa mchango wao katika kuboresha afya ya wananchi. Vilevile, Wizara itasambaza fomu za usajili wa Waganga wa Tiba Asili katika mikoa na wilaya.

## MAFUNZO YA WATUMISHI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII

**258** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara inatarajia kuanzisha utaratibu wa ukusanyaji takwimu za rasilimali watu kupitia Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya nchini "*MTUHA*". Utaratibu huu utarahisisha upatikanaji wa taarifa za rasilimali watu katika ngazi mbalimbali za utoaji huduma za afya. Aidha, mafunzo ya utunzaji, uimarishaji na matumizi ya takwimu hizi yatatolewa katika ngazi mbalimbali za utoaji huduma. Vilevile, takwimu kuhusu uendeshaji wa vyuo vya afya nchini zitaboreshwa ili kurahisisha maamuzi ya kuboresha mafunzo yatolewayo vyuoni.

**259** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaboresha mafunzo yatolewayo katika vyuo vya afya nchini, kwa kupitia mitaala minne ya kada za afya ili kuendana na mahitaji ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi "*NACTE*". Mahitaji ya Baraza hili yanazingatia mwanafunzi kupata umahiri unaotokana na kuweka mkazo katika mazoezi ya vitendo ili aweze kutoa huduma bora mara anapohitimu mafunzo yake. Aidha, vyuo 86 viko katika ngazi mbalimbali za kupata ithibati.

**260** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) kwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kwa mwaka kufikia wanafunzi 4,300. Ongezeko hili la wanafunzi litakwenda sambamba na kuwaajiri walimu wapya, kuongeza vifaa vya kufundishia

na vitabu vyuoni. Vilevile, ukarabati wa vyuo utaendelea ili kuviwezesha kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

***261*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kuziimarisha Kanda nane za Mafunzo ili ziweze kusimamia na kuimarisha vyuo vya mafunzo ya afya katika mikoa na wilaya zinazozisimamia. Aidha, Kanda hizi za mafunzo zitatoa ushauri wa kitaalamu kwa wilaya ili kuziwezesha kuandaa na kuitekeleza mipango endelevu ya masuala mbalimbali ya afya kama ilivyo kwenye Mipango Kabambe ya Afya ya Halmashauri.

***262*** ***Mheshimiwa Spika***, kwa hivi sasa kuna vyuo vya kufundisha Madaktari Wasaidizi - "*Assistant Medical Officers*" vitano ambavyo vinaingiza wastani wa wanafunzi 200 kwa mwaka. Vyuo hivyo viko Bugando, Ifakara, KCMC, Mbeya na Tanga. Katika mwaka huu wa fedha, mafunzo ya Madaktari Wasaidizi yataanzishwa katika Hospitali ya Arusha Lutheran Medical Centre na Hospitali ya Peramiho, Songea. Aidha, mradi wa ujenzi wa chuo cha Madaktari Wasaidizi katika Hospitali ya Tabora utaanza kutekelezwa mwaka huu baada ya usanifu wa majengo kukamilika na wazabuni kupatikana.

***263*** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia ziara ya Kiserikali iliyofanyika nchini Cuba ambapo Mheshimiwa Makamu wa Rais aliongoza ujumbe wa Tanzania, makubaliano yalifikiwa ya kuanzisha mafunzo ya udaktari hapa nchini ambayo yataendeshwa na Chuo Kikuu cha Matanzas

cha nchini Cuba. Mafunzo kama hayo tayari yameanzishwa Unguja na Pemba. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ikishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pia inajiandaa kuanzisha mafunzo hayo Tanzania Bara. Kwa kuanzia, wanafunzi wa udaktari 30 watadahiliwa katika muhula wa mafunzo unaotarajiwa kuanza mwezi Septemba 2009. Kwa kuanzisha mafunzo haya, tutaweza kuongeza idadi ya wanafunzi wa udaktari wanaodahiliwa nchini kufikia 575 kwa mwaka. Madaktari watakaohitimu katika mafunzo haya yanayoendeshwa kwa kushirikiana na Cuba watapewa nafasi za kusomea udaktari bingwa katika vyuo vikuu vya nchini Cuba.

***264*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuboresha taaluma katika vyuo na hasa katika kufundisha stadi za kutoa huduma, Wizara itaanzisha maabara za kujifundishia katika vituo vya kanda vya Morogoro, Kigoma na Mwanza kwa kushirikiana na Shirika la Nuffic la Uholanzi. Maabara kama hiyo pia itaanzishwa katika Chuo cha Madaktari Wasaidizi cha Ifakara.

**HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII**

***265*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera ya utoaji huduma za Ustawi wa Jamii. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuziwezesha Halmashauri kutekeleza mpango shirikishi jamii wa utambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Vilevile, ili kuharakisha upatikanaji wa haki kwa watoto walio katika mkinzano na sheria, Wizara itatoa mafunzo kwa Maafisa Ustawi wa

Jamii katika Halmashauri 50. Mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wa kusimamia na kuratibu huduma kwa watoto na vijana walio katika mkinzano na sheria. Wizara pia, itaanza ujenzi wa mahabusi ya watoto katika Jiji la Mwanza na kufanya ukarabati katika mahabusi ya Tanga.

266 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kuboresha huduma za chakula, malazi na afya katika makazi 17 ya wazee na watu wenye ulemavu, vyuo vitatu vya ufundi kwa watu wenye ulemavu, Mahabusi tano za watoto, Shule ya Maadilisho, makao ya watoto Kurasini na Kituo cha Ustawi wa Mama na Mtoto cha Ilonga. Aidha, Wizara itaimarisha mafunzo ya ufundi stadi katika vyuo vya watu wenye ulemavu na kuwawezesha vijana kutoka mahabusi za watoto, makao ya watoto na shule ya maadilisho kupata mafunzo ya ufundi stadi.

***267*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau itafanya utafiti ili kubaini sababu za kijamii zinazo sababisha mauaji ya albino na kupanga mipango endelevu ya kukomesha ukatili na unyanyasaji huu. Aidha, Wizara itahamasisha jamii juu ya umuhimu wa kushiriki kikamilifu katika kutoa huduma za malezi, matunzo na ulinzi kwa makundi maalum. Ili kuboresha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii katika Halmashauri, Wizara itatoa mafunzo kwa Maafisa Ustawi wa Jamii na watendaji wengine jinsi ya kutoa huduma katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

***268*** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuboresha huduma za utengamao kwa watu wenye ulemavu, Wizara kwa

kushirikiana na Halmashauri itaandaa utaratibu utakaowezesha upatikanaji wa vifaa vya kujimudu kwa watu wenye ulemavu vikiwemo shimesikio, fimbo nyeupe, magongo, dawa na mafuta ya ngozi kwa albino. Aidha, Wizara itahamasisha utekelezaji wa sheria mpya kuhusu haki kwa watu wenye ulemavu.

**WAKALA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII**

**Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali**

***269*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wakala utaendelea kuimarisha utoaji huduma bora za uchunguzi wa sampuli mbalimbali na kutoa matokeo kwa wakati, kwa kuzipatia maabara zake mashine, vifaa, vitendanishi na kemikali za kutosha na zenye ubora. Aidha, Wakala utafanya matengenezo kinga kwa mitambo ya uchunguzi ili iweze kutoa matokeo sahihi na kudumu kwa muda mrefu.

***270*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Wakala utaandaa kanuni na miongozo ya utekelezaji wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu ya mwaka 2009. Aidha, utaendelea kushiriki katika kikosi kazi, kuchukua sampuli za uchunguzi, kukusanya na kuandaa mfumo wa kutunza taarifa kitaifa za watuhumiwa wa mauaji ya albino na vikongwe, wabakaji, majambazi na watumiaji wa dawa za kulevya.

***271*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wakala utaimarisha usimamizi wa Sheria

ya Usajili wa Kemikali za Viwandani na Majumbani kwa kufanya ukaguzi katika viwanda, maghala, vituo vyote vya mipakani, bandarini na viwanja vya ndege. Aidha, Wakala utaendelea kushirikiana na Taasisi za ndani na nje katika kutekeleza mikataba ya kimataifa ya usimamizi wa kemikali, kufanya tathmini ya mradi wa "SAICM" na kuandaa ripoti itakayowasilishwa Serikalini na nakala kutumwa Shirika la Kimataifa la Mafunzo na Utafiti "*United Nation Institute for Training and Research – UNITAR*" ambalo linafadhili mradi.

***272*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Wakala itagharamia mafunzo na kazi zingine za utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji Utumishi wa Umma awamu ya pili "*Public Sector Reform Programme II – PSRP II*".

***273*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wakala utaendeleza hatua za kupata hati ya ithibati chini ya usimamizi wa "*South African National Accrediting System - SANAS*" kwa baadhi ya njia za uchunguzi baada ya kuongeza nafasi ya kufanyia kazi za kimaabara kufuatia kukamilika kwa jengo la kisasa kwenye Ofisi ya Mkemia Mkuu, Dar es Salaam. Aidha, Wakala utaendelea na mchakato wa kufufua mafunzo ya Ufundi Sanifu Kemia ambayo yalisitishwa mwaka 1984. Vilevile, Wakala utashiriki kuandaa miswada ya Sheria ya Wakemia na Sheria ya Mkemia Mkuu.

**Mamlaka ya Chakula na Dawa**

***274*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Mamlaka itaendelea kusimamia ubora wa vyakula,

dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa kufanya usajili na ukaguzi wa viwanda vya kutengeneza vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Aidha, Mamlaka itaendelea kuimarisha ushirikiano na Halmashauri katika kufanya ukaguzi wa majengo na sehemu nyingine zinazotoa huduma ya vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Vilevile, Mamlaka itaendelea kubaini na kuondoa bidhaa bandia katika soko kwa kufanya misako ya kushtukiza. Mamlaka pia, itaendelea kudhibiti dawa zinazoingizwa nchini kwa majaribio kwa kuzifanyia tathmini na kukagua maeneo ya majaribio.

**275** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Mamlaka itatekeleza mpango wa ufuatiliaji wa madhara yatokanayo na dawa ujulikanao kama "*Cohort Event Monitoring*". Aidha, Mamlaka itaendelea kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa. Vilevile, Mamlaka itaendelea na utekelezaji wa mfumo wa majaribio wa ukusanyaji taarifa za magonjwa yatokanayo na kula chakula –"*Food Borne Diseases*" katika Halmashauri 17 za mikoa ya Singida, Dodoma na Manyara. Mfumo huu utasambazwa nchini kote baada ya kufanyiwa tathmini.

**276** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Mamlaka itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji na uenezaji wa Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu katika mikoa 10 iliyobaki ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mara, Kilimanjaro, Manyara, Arusha, Tabora, Dodoma na Iringa. Aidha, Mamlaka itaendelea kuboresha mifumo yake ya utendaji kazi kwa kuandaa na kuboresha

miongozo mbalimbali ya utoaji huduma. Vilevile, Mamlaka itaboresha mkataba wake na wateja ili iweze kutoa huduma bora zaidi.

***277 Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Mamlaka itaendelea kufanya uchunguzi wa vyakula, dawa na vipodozi vilivyo sokoni na vinavyoingizwa nchini kupitia vituo vya forodha ili kuzuia uingizwaji wa bidhaa bandia na hafifu. Aidha, Mamlaka itaendelea na usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utendaji kazi wa maabara ndogo za dawa na kupima madini joto kwenye chumvi kwa kuzipatia kemikali na kutoa mafunzo ya rejea kwa watendaji. Vilevile, Mamlaka itafungua ofisi moja ya kanda itakayosimamia utekelezaji wa majukumu yake katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Lengo ni kusogeza huduma zilizo bora karibu na wananchi.

**TAASISI**

**Taasisi ya Chakula na Lishe**

***278 Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa 2009/10, Taasisi itaendelea na juhudi za kutatua tatizo la upungufu wa vitamini A kwa kuratibu ugawaji wa matone ya vitamini A na dawa za minyoo zinazotolewa mara mbili kwa mwaka yaani mwezi Juni na Desemba. Aidha, Taasisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa mpango wa kitaifa wa kuongeza virutubishi kwenye unga wa mahindi, unga wa ngano na mafuta ya kula kwa kuhimiza viwanda husika kuanza kutekeleza jukumu hilo. Vilevile, Taasisi itakamilisha miongozo na vijitabu vya maelekezo kwa viwanda juu ya uongezaji wa virutubishi hivyo. Taasisi pia, itafuatilia

ukamilishaji wa kanuni za kuongeza virutubishi hivyo kwenye vyakula.

***279*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa 2009/10, Taasisi itaendelea kuhimiza jamii hasa kwenye ngazi ya Kaya kutengeneza chakula cha mchanganyiko wa unga wa mahindi na soya, madini na vitamini ili kiweze kutumiwa na watu waishio na virusi vya UKIMWI na wenye VVU majumbani. Aidha, Taasisi itahamasisha matumizi ya muhogo kwa kusimamia kwa karibu zaidi utekelezaji wa mradi wa miaka mitatu wa kuongeza thamani ya muhogo katika vijiji vitakavyochaguliwa katika mkoa wa Mtwara.

***280*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Taasisi itaendelea kutoa mafunzo kwa watoa huduma wa afya juu ya tiba ya utapiamlo katika wilaya za mikoa ya Singida, Dodoma, Iringa, Mbeya na Kilimanjaro. Aidha, Taasisi itaendelea kuhamasisha viongozi wa wilaya na wakaguzi wa chumvi katika wilaya za Mwanga, Same, Tanga, Muheza na Mafia na kusambaza vifaa vya kuchanganyia chumvi na madini joto ili kuboresha uzalishaji wa chumvi yenye madini joto. Vilevile, Taasisi itaendelea kuelimisha jamii kuhusu tatizo la upungufu wa madini joto mwilini kupitia vyombo vya habari na namna ya kulikabili.

***281*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2009/10, Taasisi itaendelea kutoa mafunzo kuhusu huduma na matunzo ya lishe kwa watu wanaoishi na VVU kwa watoa huduma ya afya katika wilaya 16 za mikoa ya Dodoma, Singida, Kigoma na Ruvuma. Aidha, Taasisi itasimamia utekelezaji wa

programu ya kutoa chakula kwa watu wanaoishi na VVU wenye hali mbaya ya lishe pamoja na watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira hatarishi. Programu hii itatekelezwa katika vituo vinane katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Shinyanga, Iringa na Mbeya.

***282*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Taasisi itatoa mafunzo kwa wanasihi 230 wa sekta ya afya walio katika hospitali na vituo vya afya vinavyotoa huduma ya hospitali rafiki wa mtoto, kuhusu ulishaji wa watoto wachanga na wadogo na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Mafunzo hayo yatawezesha jamii kunyonyesha na kulisha watoto wachanga na wadogo kwa ufanisi na hivyo kuimarisha hali zao za lishe hasa katika kipindi hiki cha janga la UKIMWI. Aidha, Taasisi itatoa mafunzo kwa wasimamizi 22 wa utekelezaji wa hospitali kuwa rafiki wa mtoto katika hospitali za wilaya na vituo vya afya katika wilaya za Ngara, Magu, Kigoma, Kasulu, Kibondo, Siha, Hai, Makete, Mtwara, Bagamoyo na Temeke.

***283*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2009/10, Taasisi itasambaza kititA cha afua muhimu za lishe katika wilaya 11 kwa kuanzia. Wilaya hizo ni Temeke, Magu, Mtwara, Bagamoyo, Makete, Siha, Hai, Kigoma, Ngara, Kibondo na Kasulu. Lengo la kitita hicho ni kutoa mwongozo wa kuwawezesha watendaji wa wilaya kutambua na kutoa kipaumbele masuala ya lishe katika mipango ya maendeleo na kutekeleza kulingana na rasilimali walizonazo, hatimaye kuboresha lishe ya jamii husika.

**Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu**

***284*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Taasisi itashiriki katika majaribio ya awamu ya tatu katika kupima chanjo ya Malaria. Matokeo ya utafiti huo yatasaidia kuijulisha Serikali ubora na kubaini uwezo wa chanjo hiyo kutumika nchini. Aidha, Taasisi itatafuta fedha za ujenzi wa ofisi kituo cha Muhimbili na pia kuongeza uwezo zaidi wa watumishi katika kufanya tafiti pana zaidi za Kifua Kikuu na UKIMWI. Vilevile, Taasisi itafundisha na kusimamia uandishi wa rasimu ndogo ndogo kwenye Halmashauri za Wilaya ili kuwasaidia kupata fedha za kuendeshea tafiti kuhusu masuala yahusuyo rasilimali watu katika maeneo yao ya kazi wilayani.

***285*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Taasisi itaendelea kufanya majaribio ya chanjo dhidi ya virusi vya *Papilloma* vinavyosababisha Saratani ya Shingo ya Kizazi kwa wanawake. Lengo la majaribio haya ni kutathmini matokeo ya kinga na usalama wa chanjo hiyo iitwayo "*HPV-16/18 L1 ASO4*" kwa wanawake wenye umri wa kuanzia miaka 10 hadi 25. Aidha, Taasisi itaendelea kufanya tathmini ya ubora wa kipimo cha maambukizi ya Kaswende *"Rapid Syphilis Test"* ili kubaini uwezekano wa kujumuisha huduma hii katika mpango wa kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

***286*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Taasisi itashirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira "*NEMC*" na Chuo Kikuu

cha Dar es Salaam katika kutafiti njia bora zaidi ya kutibu maji kwa gharama nafuu katika maeneo ya Kaya hapa nchini. Aidha, mbinu za kutibu maji zitakazofanyiwa uchambuzi wa kina ni pamoja na kuchemsha, kutumia klorini *"waterguard"*, kutumia mchanganyiko wa shabu na klorini *"water purifier - PUR"*, kutumia kichuja maji cha kawaida "*water filter"*, kutumia kichuja maji chenye shanga za bromine *"Halopure filter"*, na pia kutibu maji kwa kutumia mionzi ya jua "*solar disinfection"*. Utafiti huu utasaidia kutoa mwongozo sahihi wa kutibu maji kwa manufaa ya jamii nzima ya Tanzania, kwa lengo la kupunguza na kuzuia magonjwa ya Kuhara, Kipindupindu na Homa ya Matumbo.

**Taasisi ya Ustawi wa Jamii**

***287*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2009/10, Taasisi itaendelea kukamilisha ujenzi wa awamu ya nne wa maktaba ya kisasa kwa kukamilisha ujenzi wa nguzo na kuta kwa ghorofa nne. Aidha, Wizara itaendelea kukamilisha taratibu za umilikishwaji wa eneo la Msoga – Chalinze, kuandaa mipango ya kuendeleza eneo hilo, ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango wa matumizi wa eneo hilo na kuainisha gharama na awamu za utekelezaji wa mpango huu. Vilevile, Taasisi itaendelea kutoa kozi fupi fupi kuhusiana na huduma kwa waathirika wa maafa, huduma ya matunzo kwa watoto yatima, huduma za ushauri nasaha na ushauri wa kisaikolojia kwa watu wanaoathirika kutokana na matatizo mbalimbali katika jamii.

***288*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa Taasisi itaanza kutoa wahitimu wa shahada ya kwanza katika fani za Ustawi wa Jamii na kwa kuwa

hakuna chuo cho chote nchini kinachotoa mafunzo ya shahada ya uzamili katika fani hiyo, Taasisi itaanza mchakato wa kuanzisha mafunzo ya shahada za uzamili yaani "*Masters in Social Work*" katika mwaka 2009/10. Hata hivyo, ili kukamilisha mchakato wa kuanzisha mafunzo haya, Wizara itaendelea kuisaidia Taasisi ili kuhakikisha kuwa wahadhiri wake wanapata nafasi za masomo ya shahada za uzamivu.

**Bohari ya Dawa**

***289*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Bohari itaongeza upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kutoka asilimia 80 ya sasa hadi 90 kwa kuingia makubaliano maalum na wazabuni ili kupunguza muda wa kuagiza na kupokea bidhaa. Aidha, Bohari itaimarisha mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kuwawezesha wateja kupata taarifa za upatikanaji dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Vilevile, Bohari itatoa taarifa ya matumizi na salio la fedha za vituo kila baada ya miezi mitatu. Bohari pia, itafuatilia upatikanaji wa mahitaji ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma.

***290*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Bohari itafunga mitambo ya kufungasha dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika Bohari zote za kanda ili kutekeleza mfumo wa "*Integrated Logistics Systems – ILS*" nchi nzima. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itatoa mafunzo ya ziada kwa watumishi wa vituo vya afya na zahanati ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mfumo huo.

**291** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Bohari itakasimu madaraka ya maamuzi ya kiutendaji kazi kwa Bohari za Kanda kama ilivyoainishwa kwenye Mpango Mkakati. Aidha, Bohari itapanua uwezo wa maghala yake katika Bohari za Kanda za Dodoma, Mwanza, Tabora na Mtwara na kuongeza wafanyakazi wenye ujuzi zaidi kwa lengo la Bohari za Kanda kujitosheleza katika utoaji wa huduma. Hatua zote hizo zimelenga katika kuimarisha usambaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa vituo vya kutolea huduma za afya vya umma.

**MIRADI YA MAENDELEO**

**292** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara inaomba kiasi cha shilingi **260,599,867,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi **13,029,173,000.00** ni fedha za ndani na shilingi **247,570,693,900.00** zinatoka kwa Taasisi za Kimataifa na Wadau wa Maendeleo wanaochangia Mfuko wa Pamoja wa Afya na wale walioko nje ya Mfuko. Fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:-

**293** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kuimarisha Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali Maalum na za Rufaa, kama ifuatavyo; Katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Wizara itanunua na kusimika mitambo na vifaa vya wodi ya watoto pamoja na upasuaji wa moyo, na itanunua vifaa na vitendanishi kwa ajili ya matibabu ya figo. Wizara itatoa mchango wa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji wa

moyo ambalo litajengwa kwa msaada wa Serikali ya Watu wa China. Aidha, Wizara itaendelea kufanya matengenezo kinga ya vifaa tiba, ununuzi wa vifaa tiba vipya, gari maalum la kubebea wagonjwa na maandalizi ya ujenzi wa kituo cha upasuaji wa magonjwa ya ubongo na mishipa ya fahamu katika Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili-MOI. Vilevile, Wizara itanunua, itafunga na kuzindua vifaa vya upasuaji wa moyo na ununuzi wa gari la wagonjwa kwa hospitali ya rufaa ya KCMC. Wizara pia, itajenga wodi, chumba cha upasuaji, chumba cha mionzi, ofisi na madarasa kwa ajili ya Taasisi ya Saratani ya Ocean Road. Lengo ni kupunguza rufaa ya wagonjwa nje ya nchi na kuhakikisha Watanzania walio wengi wanapata huduma bora na kwa wakati.

***294*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea na ujenzi wa hospitali maalum ya rufaa kanda ya kusini-Mtwara kwa kuandaa michoro na kujenga uzio.

***295*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kukarabati majengo ya huduma za mpango wa chanjo, mama na mtoto, vituo vya kutolea huduma za afya katika mikoa ya Mara, Tabora na Mtwara na majengo ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kanda ya kaskazini-Arusha. Aidha, Wizara itaendelea na ujenzi wa kituo cha utengamao wa magonjwa ya Ubongo na Uti wa Mgongo Mbweni na kumalizia upembuzi yakinifu na ujenzi wa majengo ya damu salama kituo cha Dodoma.

***296*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa Maabara

ya Ubora wa Dawa na ununuzi wa vifaa vya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali na Maabara ya Tiba Asili ya Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu-Mabibo.

***297*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kutoa mchango wa Serikali kwa ajili ya Mradi wa Kupunguza Vifo vya Wanawake Wajawazito ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa na samani. Wizara pia, itatoa mchango wa Serikali kwa kulipia kodi ya ongezeko la thamani inayotokana na ununuzi unaotokana na Mfuko wa Pamoja na Mchango wa Tele kwa Tele wa Mfuko wa Afya ya Jamii. Aidha, Serikali imetenga fedha ili kuziimarisha hospitali maalum za Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ili ziwe na uwezo wa kutoa huduma ambazo zimeendelea kupatikana nje ya nchi.

***298*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea na uboreshaji wa huduma za Ustawi wa Jamii kwa kufanya yafuatayo; ujenzi na ukarabati wa mahabusi za Mtwara na Mbeya; chuo cha maadilisho cha Luanzari; kituo cha kulelea watoto mchana cha Kisangara; makazi ya wazee ya Sukamahela; chuo cha watu wenye ulemavu wa kuona cha Singida na ukarabati wa Ofisi ya Idara ya Ustawi wa Jamii, Dar es Salaam. Aidha, Wizara itakarabati na kuweka vifaa na samani katika jengo la mahabusi ya watoto, Dar es Salaam.

***299*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea na uboreshaji wa Vyuo vya Mafunzo ya Afya kama ifuatavyo: itaendelea na

ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa na samani kwa vyuo vya afya vya uuguzi vya Kahama, Njombe, Mtwara, Korogwe, Tanga, Tukuyu, Mbulu, Mirembe, Bagamoyo, Kondoa, Same, Tarime, Nzega na Mbozi na Kituo cha kudhibiti uenezaji wa wadudu dhurifu cha Muheza. Vyuo vingine ni pamoja na Chuo cha CEDHA-Arusha; Chuo cha ufundi cha afya cha Kagemu; Chuo cha afya ya mazingira cha Ngudu na Tanga. Vilevile, Wizara itaendelea na ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa na samani kwa vyuo vya Matabibu vya Mafinga, Kilosa, Masasi, Musoma, Kibaha na Maswa; Vyuo vya Waganga Wasaidizi vya Mbeya na Ifakara; chuo cha Mafundi Sanifu wa Maabara cha Singida; chuo cha PHCI-Iringa na chuo cha kanda cha Kigoma. Wizara pia, itaendelea na ukarabati na upanuzi wa majengo ya vyuo vinne vya Mpanda, Tunduru, Kibondo na Nachingwea.

**SERA NA MIPANGO**

**Mabadiliko katika Sekta ya Afya**

***300 Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea na uraghibishi wa jamii kuhusu Sera ya Afya ya mwaka 1990 iliyopitiwa 2007, Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa Tatu (2009 – 2015), MMAM (2007 – 2017) na miongozo mbalimbali kulingana na mabadiliko yanayoendelea katika sekta ya afya kwa kupitia vipindi vya afya vinavyotangazwa kila wiki katika radio na televisheni za TBC. Aidha, Wizara itaandaa vipindi na matangazo yanayotokana na maendeleo ya utekelezaji wa mabadiliko na hali halisi ya utoaji wa huduma za afya katika Halmashauri na hospitali za mikoa. Lengo ni kutoa fursa kwa mikoa

kuendelea kuhamasishana na kubadilishana uzoefu wa mafanikio na namna ya kukabiliana na changamoto zinazowakabili kwa kutangaza vipindi hivyo kwenye radio za kanda. Vilevile, Wizara itaandaa kitita maandiko cha uraghibishi wa Sera ya Afya, Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya III na MMAM ili, kuziwezesha Kanda na mikoa kutafsiri Sera ya Afya kwa njia rahisi na kuoanisha mikakati na miongozo inayotokana na Sera hiyo katika mtiririko utakaowezesha ngazi ya Halmashauri na vituo vya huduma kuelewa utekelezaji wake haraka zaidi.

**Uendeshaji Huduma za Afya katika Halmashauri**

**301** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itaendelea kusimamia na kufuatilia upangaji na utekelezaji wa mipango ya afya katika Halmashauri. Aidha, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kitalaamu na wa kiufundi katika maeneo ya utekelezaji wa mkakati wa malipo kwa watoa huduma kwa ubora wa utendaji kazi na kuhakikisha kuwa mipango kabambe ya afya ya Halmashauri inakuwa mipango shirikishi inayotokana na mipango ya zahanati na vituo vya afya. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imejipanga kupitia upya Mwongozo wa upangaji mipango ya Afya ya Halmashauri kwa madhumuni ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi.

**Mfuko wa Afya ya Jamii**

**302** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kuhusu

uendeshaji, usimamizi na matumizi ya mfumo wa taarifa wa Mfuko kwa wakufunzi wa vyuo vya kanda na mikoa. Ujuzi watakaoupata, utawasaidia kutoa mafunzo kwa waratibu wa Mfuko kwenye Halmashauri mbalimbali za wilaya, miji, manispaa na majiji ili kuziwezesha kuwa na mipango endelevu ya mfuko na kuwawezesha wananchi wengi zaidi kujiunga na Mfuko. Aidha, Wizara itakamilisha mchakato wa uundwaji wa chombo cha usimamizi wa huduma za bima ya afya nchini "*reguratory mechanisms for health insurance schemes*". Chombo hicho kitaisaidia Wizara kuratibu mifuko yote ya bima za afya nchini kwa kutoa usajili, kuangalia viwango vya wanachama, ubora wa huduma zinazotolewa kulingana na michango. Hii itatoa fursa kwa wananchi wengi zaidi kupata kinga bora ya matibabu na haki yao ya msingi ya huduma bora.

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

**303** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya inakusudia kuanza kutoa huduma za matibabu kwa Waheshimiwa Madiwani na kwa wanachama Wastaafu wa Mfuko na kuongeza Ofisi mbili za kanda ili kusogeza huduma karibu na wanachama.

**304** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara kupitia Mfuko itaboresha huduma hasa Vijijini, kwa kutengeneza na kusambaza nakala 500 za ramani inayoonesha mtandao wa vituo vya matibabu na mahali vilipo ki-Wilaya. Ramani hizi zitasaidia sana Halmashauri katika mipango yao ya ujenzi wa vituo vipya vya matibabu hasa zahanati

na vituo vya afya. Aidha, Mfuko utatenga jumla ya shilingi bilioni 3 kwa ajili ya vifaa tiba na shilingi bilioni 2 kwa ajili ya mikopo nafuu ya ukarabati wa sehemu za kutoa huduma za matibabu kwa wanachama wa Mfuko.

**305** ***Mheshimiwa Spika***, katika zoezi la kutoa elimu kwa wamiliki wa maduka ya dawa baridi kuhusu Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu - "*ADDO*", katika mwaka 2009/10, Mfuko kwa kushirikiana na Mamlaka ya Chakula na Dawa nchini utatoa elimu ya Kata-Kwa-Kata kwa jumla ya Kata 900. Aidha, Mfuko utazihamasisha Halmashauri zitumie mapato yanayotokana na malipo kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, kununulia dawa. Vilevile, Mfuko umepewa jukumu la kuunganisha na kuratibu huduma zinazotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na ile ya Afya ya Jamii kwa lengo la kupunguza malipo ya papo kwa papo ili ifikapo mwaka 2015 idadi ya Watanzania wanaohudumiwa na Mifuko hii ifikie asilimia 45 ya Watanzania wote.

**306** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Mfuko utaifanyia marekebisho Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kuuwezesha Mfuko kushiriki kikamilifu katika uboreshaji wa huduma na kuufanya uwekeze zaidi katika sekta ya Afya ili uweze kuwa na uwezo zaidi wa rasilimali katika kusimamia shughuli zake hasa huduma maeneo ya vijijini. Vilevile, Mfuko ukiwa ni Mwenyekiti wa kamati ya Kitaalamu ya Mifuko ya Bima ya Afya Duniani iliyo chini ya Taasisi ya kimataifa ya Hifadhi ya Jamii – *"International Social Security Association-ISSA"* utaipatia msaada wa ushauri wa

kitaalam Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu uanzishwaji wa Bima ya Afya ya kijamii, na nchi mbalimbali zinazokusudia kuanzisha Mifuko ya Bima ya Afya barani Afrika.

**USHIRIKIANO WA NDANI NA NJE YA NCHI**

***307*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara itaendelea kuwa na ushirikiano mzuri na wa karibu na nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa yanayosaidia sekta ya afya na ustawi wa jamii. Wizara pia, itaendeleza ushirikiano mzuri na sekta nyingine ambazo zinachangia katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii.

***308*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Mikoa itaendelea kuadhimisha siku mbalimbali za Afya zinazoadhimishwa Kitaifa na Kimataifa. Baadhi ya siku hizo ni za Afya, UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma, Malaria Afrika, Tiba Asili ya Mwafrika, Watu Wenye Ulemavu, Wazee, Fimbo Nyeupe na Kutotumia Tumbaku.

***309*** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Denmark, Uswisi, Uholanzi, Norway na Ujerumani na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ya; Benki ya Dunia, UNFPA, Ireland Aid, CIDA - Canada na Shirika la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa kutoa misaada yao katika Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Afya ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii. Pia napenda kuzishukuru nchi nyingine za China, Cuba, Canada, Hispania, India, Ireland, Italia,

Japan, Korea Kusini, Marekani, Misri, Sweden, Ufaransa na Uingereza ambazo zimeendelea kuisaidia sekta ya afya kwa njia mbalimbali.

**310** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuchukua nafasi hii pia kushukuru mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao mzuri na Wizara. Mashirika haya yanajumuisha Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Kimataifa la Maendeleo (UNDP), DFID, FINIDA, GAVI, Shirika la Umoja wa Mataifa la Uzazi wa Mpango (UNFPA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI (UNAIDS), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Benki ya Dunia (World Bank), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Benki ya Nchi za Kiarabu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi ya Nchi za Afrika (BADEA), Overseas Related Export Trade (ORET), Umoja wa Nchi zinazotoa Mafuta kwa wingi Duniani (OPEC), na Madaktari Wasio na Mipaka (Medicins Sans Frontieres – MSF). Wengine ni CUAMM, DANIDA, GTZ, JICA, KOICA, Baylor College of Medicine ya Marekani, KfW, MISERIOR, EED, SAREC, SDC, CDC, SIDA (Sweden), Abbott Fund, Engender Health (USA), CORDAID (Netherlands), BASIC NEED (UK), HelpAge International, ILO, Family Health International (FHI), Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF), Shirika la Upasuaji la Spain, Good Samaritan Foundation (GSF) na USAID. Aidha, tunawashukuru pia Wadau wa Maendeleo wa mradi wa kudhibiti magonjwa ya Usubi na Vikope ambao ni African Programme for Orchorcerciasis Control, International Eye Foundation, Sight Savers International, Merck & Company, Pfizer, Helen Keller

International, Christoffel Blinden Mission (CBM) na International Trachoma Initiative. Taasisi nyingine za Kimataifa ni Axios International, President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR), Clinton Foundation, Bill and Melinda Gates Foundation, Abbot Laboratories, London School of Hygiene and Tropical Medicine, Johns Hopkins University, Global Fund, University of Columbia, CMB, Germany Leprosy Relief Association, Gabriel Project ya Marekani, Citi Bank, General Electric (GE – USA), Havard University na Duke University za Marekani, Community of Saint Egidio (DREAM), Supply Chain Management System (SCMS), NOVARTIS, Saint Thomas Hospital- London, Management Science for Health (MSH), GlaxoSmithKline (GSK) na Military Advancement for Medical Research, Department of Defence ya Marekani.

***311 Mheshimiwa Spika***, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na William Mkapa HIV/AIDS Foundation, Aga Khan Foundation, AMREF, Lions Club, Rotary Club International, BAKWATA, CCBRT, CSSC, CCT, ELCT, TEC, Msalaba Mwekundu, Shree Hindu Mandal, TPHA, USADEFU, NSSF, PASADA, PSI, TPRI, PACT, Women Dignity Project, Tanzania Diabetic Association, MEHATA, APHFTA, TANESA, MEWATA, MUKIKUTE, White Ribbon Alliance, Mabaraza yote ya Kitaaluma, Mashirika, hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii nchini pamoja na vyama vyote vya kitaaluma vya Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii.

**312** ***Mheshimiwa Spika***, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuvishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hubert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, Dodoma, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Arusha pamoja na Vyuo vyote vya Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma.

**MWISHO**

**313** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi chote cha mwaka wa fedha 2008/09, nimefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na viongozi wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Awali ya yote napenda kumshukuru Mheshimiwa Dk. Aisha Omar Kigoda, (Mb.), kwa ushirikiano mkubwa alionipa katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara. Aidha, nachukua fursa hii ya pekee kumpongeza Bibi Blandina S.J. Nyoni kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mwezi Novemba 2008, na kumshukuru kwa kunipa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru wafuatao; Dk. Deodatus Michael Mtasiwa, Mganga Mkuu wa Serikali, Bwana George Akim Kameka, Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Wakurugenzi wa Idara zote katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Nawashukuru pia, Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Sekta ya Afya na Ustawi wa

Jamii, Mashirika ya Dini, ya Kujitolea na Binafsi. Natoa shukrani kwa Sekta nyingine ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaomba waendelee kufanya kazi kwa manufaa ya wananchi na taifa letu kwa ujumla.

***314*** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu wao. Kipekee namshukuru mke wangu mpendwa Margaret Mwakyusa na watoto wetu kwa kuwa karibu nami muda wote ninapotekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Wamenisaidia, wamenitia moyo na kunipa ushirikiano mkubwa. Kwa wananchi wa Jimbo la Rungwe Magharibi, nawashukuru kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipa na nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa moyo mkunjufu.

**Maombi ya Fedha kwa kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2009/10.**

**Mapato.**

***315*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2009/10, Wizara imekadiria kukusanya mapato ya kiasi cha shilingi **2,029,436,000.00**. Kiasi hiki kinatokana na makusanyo ya uchangiaji gharama kutoka kwenye vyuo vya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Usajili wa hospitali binafsi na maabara binafsi.

**Matumizi ya Kawaida**

***316*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2009/10, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha shilingi **218,393,211,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo,

kiasi cha shilingi **113, 561,460,400.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Kati ya hizo shilingi **94,477,947,164.00** ni kwa ajili Matumizi Mengineyo ya Wizara na kiasi cha shilingi **19,083,513,236.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Taasisi. Kiasi cha shilingi **104,831,750,600.00** ni kwa ajili ya Mishahara. Kati ya hizo kiasi cha shilingi **22,432,587,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara ambazo zitatumika kulipa Mishahara ya Watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Makao Makuu, Hospitali za Rufaa Mbeya, Mirembe na Kibong'oto na Vyuo vyote vya Serikali vya Mafunzo ya Afya. Jumla ya shilingi **82,399,163,600.00** zimetengwa kwa ajili ya Mishahara ya Taasisi. Taasisi hizo ni pamoja na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Hospitali za Rufaa za KCMC na Bugando, Hospitali Teule (District Designated Hospitals-DDH), Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Seriakali na Hospitali za Mashirika ya Kujitolea (Voluntary Agencies-VA's), Chuo cha Ustawi wa Jamii na Hospitali ya Mkoa wa Dar es Salaam.

**Mgawanyo wa fedha za bajeti ya matumizi ya kawaida mengineo mwaka 2009-10 kulingana na maeneo ya kipaumbele**




** Bajeti ya huduma za Tiba inajumuisha fedha za Dawa kwa ajili ya hospitali za rufaa, mikoa, Halmashauri, Vituo vya afya na Hahanati zote nchini. Pia fedha za matumizi ya Kawaida ya Taasisi – Hospitali za rufaa (Muhimbili, Mbeya, KCMC, Bugando, Mirembe, Kibong'oto ruzuku ya Hospitali za Teule za Halmashauri na Ruzuku ya Kitanda kwa hospitali za Mashirika ya kujitolea)

* Mganga Mkuu; inajumuisha fedha za ruzuku za matumizi ya Kawaida ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Chakula, Dawa na vipodozi

+ Hivi ni vitengo vipya vilivyopewa vifungu kuanzia mwaka huu, ambavyo awali vilikuwa chini ya Idara ya Utumisha na Utawala pamoja na Sera na Mipango.

**Miradi ya Maendeleo**

***317*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/10, Wizara inakadiria kutumia jumla ya shilingi **260,599,867,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo Serikali ya Tanzania itachangia kiasi cha shilingi **13,029,173,000.00.** Fedha kutoka kwa Wahisani wanaoisaidia Sekta ya Afya ni shilingi **247,570,693,900.00.** Kati ya fedha hizo shilingi **50,331, 143,000.00** zitatolewa na Wahisani wanaochangia Mfuko wa Pamoja na shilingi **197,239,550,900.00** zitatolewa na Wahisani walio nje ya Mfuko.

***318*** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuiwezesha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutekeleza kazi zilizopangwa mwaka 2009/10 naliomba Bunge lako Tukufu litafakari, lijadili, na kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Asasi zake yenye jumla ya shilingi **478,993,078,000.00.** Kati ya fedha hiyo, shilingi **218,393,211,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na matumizi ya kawaida. Shilingi **260,599,867,000.00** ni kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi **13,029,173,000.00** ni fedha ya ndani na shilingi **247,570,693,900.00** ni fedha ya nje.

***319*** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

# VIAMBATISHO

***Kiambatisho Na.1***

**VIREFU VYA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA NDANI**

| | | |
|---|---|---|
| ADB | - | African Development Bank |
| ADDO | - | Accredited Drug Dispencing Outlet |
| AMREF | - | African Medical and Research Foundation |
| ALu | - | Artemether /Lumefantrine |
| APHFTA | - | Association of Private Health Facilities in Tanzania |
| AIDS | - | Acquired Immuno-Defficincy Syndrome |
| AORTIC | - | African Organization for Research and Training in Cancer |
| ARV | - | Anti-Retro Viral |
| BADEA | - | Bangue Arabe pour Development Economique en Afrique |
| BAKWATA | - | Baraza Kuu la Waislamu Tanzania |
| CBM | - | Christoffel Brinden Mission |
| CCBRT | - | Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania |
| CCM | - | Chama Cha Mapinduzi |
| CCT | - | Christian Council of Tanzania |
| CDC | - | Centres for Disease Control and Prevention, Atlanta Georgia-USA |
| CHF | - | Community Health Fund |
| CIDA | - | Canadian International Development Agency |
| CSSC | - | Christian Social Services Commission |
| CUAMM | - | International College for Health Cooperation in Developing Countries |
| DANIDA | - | Danish International Development Agency |
| DDT | - | Dichloro-Diphenyltrichloroethane |
| DFID | - | UK Department for International Development |
| DNA | - | Deoxyribo NucleicAcid |
| DPT-HB | - | Diptheria, Pertussis Tetanus, Hepatitis B |
| DSE | - | Deusche stiftung fur Internationale Entwicklung |
| EEG | - | Electro Encephalogram |
| ECG | - | Echocardiogram |
| EGPAF | - | Elizabeth Glaser Paediatric AIDS Foundation |
| ELCT | - | Evangelical Lutheran Church of Tanzania |
| EU | - | European Union |
| FHI | - | Family Health International |
| FINIDA | - | Finish International Development Agency |
| GAVI | - | Global Alliance for Vaccine and Immunisation |

| | | |
|---|---|---|
| GE-USA | - | General Electric- United States of America |
| GSF | - | Good Samaritan Foundation |
| GSK | - | Glascow Smith Kline |
| GTZ | - | Gesellschaft fuer Technische Zusammenarbeit |
| HAM | - | Huduma ya Afya ya Msingi |
| HAI | - | HelpAge International |
| HIB | - | Haemophilus Influenza Type B |
| HIV | - | Human Immuno Deficiency Virus |
| IAEA | - | International Atomic Energy Agency |
| IARC | - | International Agency on Research for Cancer |
| ICU | - | Intensive Care Unit |
| IFMS | - | Integrated Financial Management System |
| ILS | - | Integrated Logistic System |
| ILO | - | International Labour Organisation |
| IMA | - | International Missionary Association |
| IMCI | - | Integrated Management of Childhood Illness |
| IMTU | - | International Medical and Technology University |
| ISSA | - | International Social Security Association |
| IPSAS | - | International Public Sector Accounting Standards |
| ITECH | - | International Training and Education Centre on HIV |
| JICA | - | Japan International Cooperation Agency |
| KCMC | - | Kilimanjaro Christian Medical Centre |
| KfW | - | Kredit feur Wiederaufbau |
| KIA | - | Kilimanjaro International Airport |
| KOICA | - | Korea International Cooperation Agency |
| MAB | - | Ministerial Advisory Board |
| MDP | - | Mectizan Donation Programme |
| Mb | - | Mbunge |
| MEHATA | - | Mental Health Association of Tanzania |
| MEWATA | - | Medical Women Association of Tanzania |
| MUKIKUTE | - | Mapambano ya UKIMWI na Kifua Kikuu – Temeke |
| MMAM | - | Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi |
| MNRI | - | Magnetic Nuclear Resonance and Imaging |
| MOI | - | Muhimbili Orthopaedic Institute |
| MSF | - | Medicine Sans Frontiers |
| MTUHA | - | Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji Huduma za Afya |
| MUHAS | - | Muhimbili University of Health and Allied Sciences |
| NACTE | - | National Accreditation Council for Technical Education |
| NEMC | - | National Environmental Management Council |
| NORAD | - | Norwegian Agency for Development |

| | | |
|---|---|---|
| NSSF | - | National Social Security Fund |
| OPEC | - | Organisation of Petroleum-Producing Countries |
| ORET | - | Overseas Related Export Trade |
| P 4 P | - | Pay for Performance |
| PASADA | - | Pastoral Activities and Services for People with AIDS |
| PEPFAR | - | President's Emergency Plan for AIDS Relief |
| PSI | - | Population Service International |
| PSRP-II | - | Public Sector Reform Programme II |
| RDT | - | Rapid Diagnostic Test for Malaria |
| SAICM | - | Strategic Approach to International Chemicals Management |
| SANAS | - | South Africa National Accreditation System |
| SAREC | - | Swedish Agency for Research Cooperation in Development Countries |
| SDC | - | Swiss Agency for Development and Cooperation |
| SIDA | - | Swedish International Development Authority |
| STI | - | Sexual Transmitted Infections |
| TACAIDS | - | Tanzania Commission for AIDS |
| TAMISEMI | - | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANESA | - | Tanzania Netherlands Support to AIDS Control |
| TBC | - | Tanzania Broadcasting Cooperation |
| TEC | - | Tanzania Episcopal Conference |
| TIKA | - | Tiba kwa Kadi |
| TPHA | - | Tanzania Public Health Association |
| TPRI | - | Tanzania Pesticides Research Institute |
| TPI | - | Tanzania Pharmaceutical Industry |
| TRA | - | Tanzania Revenue Authority |
| TUGHE | - | Tanzania Union of Government and Health Employees |
| UK | - | United Kingdom |
| UICC | - | International Union Against Cancer |
| UKIMWI | - | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNAIDS | - | Joint United Nations Programme on AIDS |
| UNDP | - | United Nations Development Programme |
| UNFPA | - | United Nations Fund for Population Activities |
| UNHCR | - | United Nations High Commission for Refugees |
| UNICEF | - | United Nations Children Fund |
| UNITAR | - | United National Institute for Training and Research |
| USA | - | United States of America |
| USADEFU | - | Usambara Development Fund |
| USAID | - | United States Agency for International Development |
| VVU | - | Virusi Vya UKIMWI |
| WHO | - | World Health Organisation |

## Kiambatisho Na. 2.

Watumishi wa Kada za Afya 3,010 na sehemu walizopangiwa katika mamlaka mbalimbali za ajira mwaka 2009.

| MKOA | KITUO | AMO/ ADO | MEDICAL ATTEND. | CLINIC. OFFICER | NURS. OFFICER | NURSES | MED.TECH. | HEALTH OFFIC. | MEDICAL DOCTOR | HEALTH SECRETARY | PHYSIOTHERAPIST | PHARMACIST | RECORD MANAGEMENT | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **ARUSHA** | DED - Ngorongoro | | ***1*** | **1** | **4** | **6** | **3** | **2** | **1** | | | **1** | | **19** |
| | RAS - Arusha | **4** | | | **5** | **16** | **2** | **3** | **7** | | | | | **27** |
| | DED-Monduli | | | | **2** | **3** | | | | | | | | **3** |
| | DED - Meru | **9** | | | **1** | **17** | **5** | **3** | | | | | | **30** |
| | DED - Karatu | **1** | **9** | **11** | **7** | **25** | **5** | **2** | | | | | | **60** |
| | CD-Arusha | | **7** | **2** | **3** | | | | **1** | | | **1** | | **3** |
| | DED - Longido | | | **2** | **1** | | **1** | **2** | **7** | | | **1** | | **9** |
| **DAR ES SALAAM** | MD-Ilala | **2** | **14** | **20** | **7** | **21** | **13** | **2** | **15** | | | | | **94** |
| | MD - Kinondoni | **5** | **4** | | | | | **7** | **1** | | | | | **17** |
| | MD- Temeke | | **12** | **21** | **10** | **27** | **13** | **1** | **4** | | | | **2** | **90** |
| | City Council -DSM | | | | | | | | | | | | | **0** |
| **DODOMA** | DED-Kondoa | | | | **6** | **4** | **2** | | | **2** | | **1** | | **15** |
| | DED - Dodoma | **2** | **5** | **7** | | **15** | **2** | **1** | | **1** | | | | **33** |
| | DED - Mpwapwa | | | **1** | **3** | **7** | **3** | | **1** | | | | | **15** |
| | MD - Dodoma | | | | | **6** | | | | | | | | **6** |

| MKOA | KITUO | AMO/ ADO | MEDICAL ATTEND. | CLINIC. OFFICER | NURS. OFFICER | NURSES | MED.TECH. | HEALTH OFFIC. | MEDICAL DOCTOR | HEALTH SECRETARY | PHYSIOTHERAPIST | PHARMACIST | RECORD MANAGEMENT | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | RAS - Dodoma | | | | **1** | | **3** | | **5** | **1** | | | | **10** |
| | DED - Kongwa | | **7** | | **1** | **4** | | | | | | **1** | | **13** |
| | DED - Chamwino | **2** | **5** | **7** | | **19** | **2** | **1** | **1** | | | | | **37** |
| | DED - Bahi | **1** | **19** | **5** | **2** | **5** | **1** | | **1** | **1** | | **1** | | **36** |
| **IRINGA** | DED- Iringa | | **10** | **11** | **5** | **10** | **2** | **1** | | | | **1** | | **40** |
| | DED - Makete | | | **1** | **2** | | | | | | | | | **3** |
| | DED - Mufindi | | **6** | **3** | **2** | **10** | | | | | | **1** | | **22** |
| | MD- Iringa | | | | | | | | | | | | | **0** |
| | DED - Njombe | **1** | **9** | **6** | **1** | **11** | **3** | | **1** | | | | | **32** |
| | RAS-Iringa | **4** | **1** | | **11** | **36** | **5** | **1** | **5** | | | **1** | | **64** |
| | DED - Ludewa | | | | | **2** | **1** | | | | | | | **3** |
| | DED - Kilolo | **3** | **5** | **7** | | **4** | **2** | **1** | | | | | | **22** |
| | TC- Njombe | | **7** | **2** | | **1** | **1** | | | **1** | | | | **12** |
| **KAGERA** | DED-Chato | | | **4** | **5** | **2** | **1** | | | | | | | **12** |
| | DED-Karagwe | **2** | **2** | | **5** | **1** | | **2** | | | | | | **12** |
| | RAS - Kagera | | **1** | | **2** | | | | | | | | | **3** |
| | DED- Muleba | | **4** | **4** | | **8** | | **3** | | | | | | **19** |

| MKOA | KITUO | AMO/ ADO | MEDICAL ATTEND. | CLINIC. OFFICER | NURS. OFFICER | NURSES | MED.TECH. | HEALTH OFFIC. | MEDICAL DOCTOR | HEALTH SECRETARY | PHYSIOTHERAPIST | PHARMACIST | RECORD MANAGEMENT | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | DED - Ngara | **2** | **8** | **4** | **3** | **5** | **2** | | **1** | | | | | **25** |
| | DED- Bukoba | | | **1** | **5** | **9** | **1** | **3** | **1** | | | | | **20** |
| | DED - Biharamulo | | **1** | **1** | **2** | | | **3** | | | | | | **7** |
| | DED - Misenyi | **1** | **4** | **1** | | **9** | **1** | | **1** | | | | | **17** |
| **KIGOMA** | DED - Kasulu | | **1** | **4** | | **1** | | | | | | | | **6** |
| | DED-Kibondo | | | **2** | | **1** | **3** | **1** | | | | | | **7** |
| | DED - Kigoma | | **4** | **3** | **3** | **5** | | | | | | | | **15** |
| | RAS - Kigoma | | | | **2** | **5** | **3** | | **2** | | | | | **12** |
| | MC - KIGOMA | | **4** | **3** | **3** | **4** | | | | | | | | **14** |
| **KILIMANJARO** | RAS - Kilimanjaro | | **4** | | | | **2** | | **1** | | | | | **7** |
